**1 FEBRUARI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 1 Februari, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

### MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu kwa heshima na taadhima. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kushiriki Kikao hiki cha Tatu cha Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge lako Tukufu tukiwa buheri wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023 zimetoa fursa ya uwepo wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu kwa siku ya Alhamis. Vilevile Kanuni hiyo hiyo katika kipengele cha 44(4) imeruhusu Waziri Mkuu kutumia kipindi

cha maswali ya papo kwa papo kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo nimeona ni vema kutumia kipindi cha leo kutoa taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 na Mtaala wa Elimu ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine nitakayoyaeleza ni pamoja na uandikishaji wanafunzi wa kidato cha kwanza, hali ya ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne na mikakati iliyowezesha Serikali kupata mafanikio katika ufaulu na uandikishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 2 Novemba, 2023 katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako Tukufu, nilitoa taarifa kuhusu kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu ya Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023 na mitaala ya elimu ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu. Utoaji wa taarifa hiyo ulitokana na umuhimu wa sera hiyo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake juu ya Taifa hili hususan katika suala la elimu. Tutakumbuka wote kwamba Tarehe 22 Aprili, 2021 ndani ya Bunge hili Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ya kufanya mabadiliko katika mfumo wa elimu uliopo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limeakisi mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiishauri Serikali. Kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Serikali imechukua hatua mbalimbali. Kwanza kwa kupokea maoni, pili kuyachambua na tatu, kuanza utekelezaji baada ya kufanya maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka katika Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako tukufu, Serikali iliwasilisha taarifa kuhusu kuidhinishwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 na Mitaala ya Elimu ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa ya utekelezaji wa mabadiliko ya Sera ya Elimu kama tulivyowasilisha. Utekelezaji kwa mtaala mpya umeanza katika ngazi ya awali, elimu ya msingi, darasa la kwanza na la tatu, elimu ya sekondari kidato cha kwanza katika baadhi ya fani za amali katika shule 96 za Serikali na binafsi ambazo zina miundombinu wezeshi kama karakana na walimu wa fani hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji huu umeenda sambamba na kutoa mafunzo katika Kata zote kwa Walimu wa Elimu ya Awali na Msingi kote nchini. Vilevile kwa lengo la kuhakikisha mabadiliko haya yanatekelezwa bila kuathiri ubora wa elimu, Serikali pia imetoa mafunzo kwa Wadhibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu 178 kati ya 184 wa Halmashauri pamoja na Maafisa Elimu wote ngazi ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa sera utaendelea kufanyika kadri ya mkakati na utekelezaji wake ambao unajumuisha uandaaji wa walimu katika fani mpya zitakazofundishwa ikihusisha maandalizi ya miundombinu mingine yenye lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu hususan katika mafunzo ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imekamilisha maandalizi ya mfumo wa Tuzo ya Taifa – *National Qualification Framework*. Vilevile Serikali inaendelea na uandaaji wa nyenzo muhimu za kuwezesha utekelezaji wa sera ikiwa ni pamoja na mapitio ya Sheria ya Elimu na baadhi ya sheria za taasisi, mikakati na programu za maendeleo ya sekta ya elimu pamoja na mipango ya utekelezaji

wake katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo ikiwemo nyenzo za udhibiti ubora wa shule na elimu ya ualimu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maboresho ya sera na mitaala na muelekeo wake kupitia njia mbalimbali ikiwemo redio za kitaifa, kijamii, televisheni, magazeti, mitandao ya kijamii, mikutano na makundi mbalimbali ya wadau, makongamano na machapisho mbalimbali yanayohusu elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Serikali imefanya mikutano na Waandishi wa Habari kutoka vyombo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwaelimisha na kuwawezesha kuelimisha jamii kuhusu mabadiliko haya ya Sera ya Elimu na mitaala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya mapokeo ya wananchi, wazazi na jamii wameonyesha kuwa na matumaini na muelekeo mpya wa elimu na mafunzo hususan eneo la upatikanaji wa fursa za elimu amali ambayo ina uhusiano wa moja kwa moja katika kuwapatia wanafunzi maarifa na ujuzi wa kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii inatarajiwa kupunguza tatizo la ajira kwa wahitimu kwa kuwapa nafasi ya kujiajiri na hivyo kuondoa dhana ya kuwa Serikali ndiye muajiri mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maboresho ya Sera ya Elimu yamepokelewa vema na watekelezaji wake ambao ni pamoja na Walimu, hasa walimu wa awali, darasa la kwanza, la tatu na shule za amali ambazo zimeanza kutekeleza mtaala mpya mwaka 2024. Maafisa Elimu ni miongoni mwa watu waliopokea vizuri, wadhibiti ubora wa shule, wamiliki wa shule binafsi ambao wameguswa na maeneo mengine na utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na uwezeshaji wa utekelezaji wa mtaala mpya. Aidha, maboresho ya sera na mitaala yamewagusa Walimu kwa kuimarisha ajira za baadhi ya Walimu ambao walisomea fani za mafunzo ya amali lakini zikawa hazitumiki, kuendeleza taaluma ya ualimu na usimamizi

wake, mafunzo haya yanaendelea kutolewa kwa walimu wa shule za Serikali na binafsi kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ushirikishwaji wa wazazi na jamii katika mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mitaala umefanyika katika hatua zote za uandaaji wa sera na mitaala. Aidha, katika kuwezesha wanafunzi kujiunga na shule za amali, wazazi wamekuwa wakishiriki katika kushauri fani ambazo watoto wao wangependa kusoma. Ili kuendana na muitikio mkubwa wa jamii kuhusu mabadiliko, Serikali itaendelea kuongeza fursa za upatikanaji wa fursa za elimu hususan kwenye shule za amali kadri ya maandalizi ya rasilimali za utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na Walimu wa fani mpya ambazo zitaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na jitihada za kuboresha elimu nchini kwa kutekeleza mikakati mbalimbali. Kutokana na juhudi hizo, tumeweza kuona mafanikio katika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi na kidato cha nne mwaka hadi mwaka. Matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne ya Kitaifa yanaonyesha kuwepo kwa ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaofaulu kutoka elimu ya msingi na kuendelea elimu ya sekondari. Vilevile, kidato cha nne na kuingia kidato cha tano nayo pia inaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuandikisha wanafunzi wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza kwa kutumia maoteo yanayotokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Hadi kufikia tarehe 26 Januari, mwaka huu 2024 idadi ya wanafunzi wa darasa la awali walioandikishwa ni 1,268,917 wakiwemo wavulana 642,979 na wasichana 625,938 pamoja na wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,366 wakiwemo wavulana 1,244 na wasichana 1,122.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi waliondikishwa darasa la kwanza ni 1,549,743 wakiwemo wavulana 772,019 na wasichana 777,724 pamoja na wenye mahitaji maalum 3,311 wakiwemo

wavulana 1,781 na wasichana 1,530. wanafunzi wa darasa la kwanza walioandikishwa ni sawa na asilimia 89.6 ya maoteo ya uandikishaji wanafunzi waliokadiriwa kuwa ni 1,729,180 wenye umri wa miaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, udahili wa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza unaotokana na takwimu za wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza wapatao 1,092,984 wakiwemo wavulana 507,933 na wasichana 585,051, udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa elimu ya awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza yanatokana na jitihada za serikali za kutekeleza mpango wake wa Sera ya Elimu bila ada ambao umewaondolea wanafunzi vikwazo vya kujiunga na elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine mafanikio haya yanatokana na jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishajii ambayo yanawavutia wanafunzi kudahiliwa na kuendelea na masomo ya elimu ya msingi na sekondari vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka miwili imetumia jumla ya shilingi trilioni 1.29 kupitia miradi mbalimbali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya shilingi bilioni 484.3 zimetolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu wa shule za elimu ya awali na msingi ambapo jumla ya shule mpya zilizojengwa ni 342. Vyumba vya madarasa vilivyojengwa 9,189, nyumba za walimu zilizojengwa 346, mabweni 28 na ukarabati wa shule kongwe 45.

(ii) Jumla ya shilingi bilioni 837.8 zimetolewa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo zimejenga shule za sekondari mpya 486 hadi sasa. Vyumba vya madarasa 21,990, nyumba za Walimu 280, mabweni 221, ukarabati wa shule kongwe 21, maabara 151 na mabwalo 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha hizo zilizoboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia shuleni ambapo sote tumeshuhudia kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na sekondari pamoja na kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne. Serikali kwa kushirikiana na walimu na wadau wa elimu nchini ilijiwekea mikakati ya kuboresha elimu ya msingi na sekondari ambapo vigezo mbalimbali viliwekwa na vilianza kutekelezwa mwezi Januari 2023 ili kuboresha elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuwapongeza sana viongozi wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kubuni na kusimamia utekelezaji wa mikakati hii ya kuboresha elimu ya msingi na sekondari ambayo imeanza kuonyesha mwelekeo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nawapongeza sana viongozi wa ngazi za mikoa, Wilaya, Halmashauri, Kata na shule pamoja na walimu na wazazi kwa kushirikiana vema katika kutekeleza mikakati hii ya kuboresha elimu likiwemo suala la upatikanaji wa chakula cha wanafunzi shuleni kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kuhamasisha vizuri wananchi katika shughuli zote za maendeleo ya elimu, pamoja na kuunga mkono kwa dhati jitihada za kuboresha elimu nchini

zinazofanywa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha naomba kutumia fursa hii kuzielekeza Ofisi za Rais TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuzingatia masuala yafutayo:-

(i) Kuzingatia wanafunzi wote wenye rika lengwa wanaandikishwa shuleni kwa wakati.

(ii) Kuendelea kusimamia udhibiti wa michango holela mashuleni.

(iii) Kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya mafunzo ya utekelezaji wa mtaala mpya zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia taarifa yangu kwa kutoa wito kwa Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wenye umri wa kujiunga na elimu ya awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza wanadahiliwa na kuanza masomo mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa viongozi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa walimu wetu kwa upendo na uadilifu ili kuwatia moyo na kuongeza ari ya uwajibikaji na kuleta matokeo chanya ya ufundishaji na ujifunzaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana hoja imeungwa mkono. Sasa nitaruhusu hoja, maswali, mtu anataka maelezo, ufafanuzi kwa hoja hii aliyoisema hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi inavyojitahidi kuboresha elimu nchini, hongereni sana. Nina swali dogo tu, Serikali sasa mtuambie mna mkakati gani wa kuweza kutosheleza walimu wenye weledi kufundisha masomo haya ya amali ukichukulia tuna upungufu wa walimu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly Ntate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwamba tunao upungufu wa Walimu kwenye shule zetu kwa ngazi mbalimbali na hii inatokana na kuwepo kwa Walimu wanaostaafu, wanaotangulia mbele za haki na wagonjwa ambapo tunajua yapo mapengo ya ufundishaji hasa kwenye eneo hili la elimu ya amali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kwenye mpango huu ni kuhakikisha kwanza, tunaendelea kupokea vibali vya ajira kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyotoa vibali vya kuajiri walimu, miongoni mwa Walimu ambao tunawaajiri hasa tunaangalia zaidi kwenye eneo hili la elimu ya amali ili kuwezesha utekelezwaji mzuri wa Sera hii mpya inayogusa kwenye maeneo ya amali ili kuwezesha ufundishaji na wanafunzi waweze kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati wetu ni kuongeza ajira kwenye sekta ya elimu ili kuwa na walimu wa kutosha, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza swali moja. Tumekuwa na tatizo sugu la upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi katika

Shule za Sekondari na huu wimbo umekuwa wa muda mrefu sana: Je, ni nini sasa mkakati wa kudumu wa Serikali, kuondoa upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule za Sekondari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Baba Askofu, Mheshimiwa Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vilevile tunao upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi kwenye Shule zetu za Sekondari. Tunapoelekea kutekeleza Sera hii mpya ya Elimu, eneo hili tumeliangalia. Tumeanza kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi kutoka Shule za Msingi na kuelekea Sekondari na kuhakikisha kuwa tunapata wafaulu ambao pia na wao tunawapeleka kwenye Vyuo vya Ualimu ili kupata taaluma ya ufundishaji wa masomo ya sayansi tuweze kupata walimu ambao watakuja kufundisha tena elimu hii kuanzia ngazi zote za msingi na sekondari ili tuweze kuongeza idadi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, mkakati uliopo ni ule ambao nimeueleza awali kwamba kupitia vibali tunavyopata kutoka kwa Ofisi ya Rais, tunatoa nafasi zaidi ya ajira za walimu wa masomo ya sayansi. Kwa mfano, ajira ya mwisho ya walimu 4,000, nafasi 2,500 zilikuwa za walimu wa masomo ya sayansi na nafasi 1,500 zilikuwa za walimu wa masomo ya *Arts*. Kwa hiyo, hii ilikuwa inatoa mwanya kwa mwalimu yeyote aliyehitimu mafunzo ya ualimu wa masomo ya sayansi kupata ajira ili kuongeza nguvu ya ufundishaji kule kwenye shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati huu utaendelea na utakuwa endelevu. Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa pamoja na Wizara ya Elimu wanaendelea kusimamia hili kwa karibu ili kuondoa upungufu mkubwa uliopo kwenye masomo ya sayansi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, elimu, hasa kwa upande wa mtaala mpya kwa maana ya amali, ni jambo mtambuka. Baada ya utekelezaji wa mtaala, wanafunzi watakaohitimu watahitaji kuwezeshwa kwenye sekta nyingine, kwenye maeneo kama TAMISEMI, kilimo, afya na maeneo mengine hasa ya ufundi: Ni kwa vipi Serikali inajiandaa kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya watoto watakaohitimu upande huo wa amali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sekiboko, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili, kwanza nataka kutoa uelewa kwamba tunapotekeleza Sera yetu mpya ya Mitaala, hatuendi moja kwa moja na madarasa yote, tunaanza na makundi machache. Wanaoanza kufundishwa mwaka huu wa 2024 kama tulivyosema tunaanza mwezi Januari, ni darasa la awali, darasa la kwanza na darasa la tatu. Kwa sababu kwenye Elimu ya Msingi tuna makundi matatu; tuna awali, halafu darasa la kwanza na la pili; kundi la tatu, ni darasa la tatu na darasa la sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wanaoanza kufundishwa mtaala mpya ni awali, darasa la kwanza na darasa la tatu. Tunaanza nao mwaka huu. Hiyo ni kwa Shule za Msingi. Kwa upande wa Sekondari, tunaanza na Kidato cha Kwanza. Pia kwa Sekondari, tunajua tuna elimu jumla na kuna zile shule za ufundi. Kwa hiyo, tumechagua Shule za Ufundi, siyo zote, chache ambazo tayari zina miundombinu na walimu wa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huu, utawezesha sasa Serikali kujipanga kupitia Bajeti yetu kuweza kumudu kuongeza pia

hata idada ya walimu, kununua vifaa ili kufanya utekelezaji huu wa sera kuwa endelevu. Mwaka huu tunapoanza na awali na darasa la kwanza, darasa la pili hawahudhurii, wanaanza darasa la tatu, tunamfanya kijana wa awali anapohitimu, anapokwenda darasa la kwanza, anaendelezwa. Darasa la pili hapati, lakini anaanzia darasa la tatu, huyu wa darasa la kwanza anakuwa darasa la pili. Kwa hiyo, utakuta awali mpaka darasa la pili itakuwa endelevu kuanzia mwakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila mwaka tutakuwa tunaenda hivyo. Yule wa darasa la tatu anaenda la nne, la tano, mpaka la sita, mwisho wa Elimu ya Msingi. Utakuta sasa tunaweza ku-*cover* maeneo yote, kila mwanafunzi anapata elimu hiyo vizuri. Wizara ya Elimu sasa itajitahidi, itapangilia mtihani kulingana na muda waliosoma masomo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunawezaje kuimarisha eneo hili? Ni pale ambapo bajeti sasa tutakuwa tunaiimarisha, kwanza kuongeza miundombinu ya majengo ya kusomea, vifaa vinavyohitajika, na walimu wenye uwezo wa fani hizo. Kwa hiyo, kila mwaka tutakuwa tunaongeza uwezo wetu. Serikali tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunaweza kufanikiwa hayo ili sera hii mpya iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mpango wa Serikali uliopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante. Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; moja kati ya jambo litakalosaidia sana utekelezaji wa Sera hii ya Elimu na kuendeleza maendeleo ya elimu yetu, ni maelekezo na uamuzi wa Serikali wa Elimu Msingi Bila Malipo. Hivi karibuni tumeshuhudia baadhi ya shule kuwa na utitiri mkubwa wa

michango kiasi cha kupelekea kuondoa ile dhana ya Elimu Msingi Bila Malipo. Ni nini kauli ya Serikali juu ya jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Serikali umebaki vilevile kwamba michango holela hairuhusiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposema michango holela, tunajua tuna michango inayokubalika kwenye jamii. Hizi shule zetu za msingi na sekondari ni shule za jamii, ziko kwenye meneo hayo. Tumeunda Kamati ya Shule kwa Shule za Msingi lakini tuna Bodi ya Shule kwa Sekondari. Wajumbe wa Bodi hizi ni wale walioko kwenye maeneo yale kwa lengo la kuwa wanapaswa kusimamia maendeleo ya shule, kushauri mwenendo wa shule na pia kupata changamoto zinazotokana na mwenendo wa kila siku, nao washiriki katika usimamizi wa uendeshaji au uendelezaji wa shule hiyo na taaluma yake kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Kamati ya Shule inajua inawajibika kwenye ile shule kufuatilia maendeleo yake na pia mahitaji yake. Inaweza kutokea kwa mfano, choo cha shilingi milioni mbili kimebomoka. Siyo lazima kusubiri Serikali ije kujenga choo. Jamii inaweza ikaweka mpango mkakati wa kujenga choo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, michango holela na michango inayokubalika, hapa iko ya aina mbili. Michango inayokubalika ni hiyo ya maendeleo; ya choo kimebomoka, Kamati ya Shule inakutana, wanasema kuna choo kimebomoka tunataka kijengwe kwa haraka watoto wetu waanze kukitumia kesho. Badala ya kusubiri kuandika barua, bajeti ipangwe mpaka TAMISEMI, wanaweza kukubaliana kwamba bwana, tuchangie hapa shilingi

mia tano, mia tano, mchango ambao unaenda kwenye choo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango hii pamoja na maamuzi hayo tumeidhibiti kidogo. Pamoja na maamuzi yenu ninyi Kamati ya Shule na Kijiji kwa ajili ya jambo la maendeleo, bado mwenye idhini ya kuanza kuchangisha ni Mkuu wa Wilaya. Tumeiweka hiyo kuondoa pia watu kukaa pamoja kutengeneza michango ambayo pia haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msimamo wa Serikali umebaki pale pale kwamba hatuhitaji michango holela. Michango holela ni ile ambayo wakati wote ninapokuwa ziara huwa natoa mifano. Mtu mmoja tu anakurupuka anasema, kesho kila mmoja awe na shilingi mia mbili mia mbili, hazina maelekezo, hazina maelezo. Michango kama hii ndiyo ile holela ambayo haikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeagiza pia kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kusimamia kutokuwepo kwa michango holela inayokwaza wazazi katika kuendesha shughuli au usimamizi wa mtoto kupata taaluma. Hiyo ndiyo maana ya michango holela na michango rasmi ambayo pia nayo tumeidhibiti na msimamo wetu umebaki pale pale kwamba michango holela haikubaliki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napongeza uthubutu wa Serikali kubadilisha mitaala kwa lengo la kuboresha elimu, lakini tutambue pia kwamba katika shule, muda ni wa msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea leo, kuna changamoto kubwa ya vitabu havijawafikia walengwa. *Printing* ya vitabu lakini pia vitabu kwenye shule wametumiwa *softcopy,* sasa vijijini watazitumiaje? Pia elimu haijafika. Naomba kujua mkakati wa Serikali, wakiangalia umuhimu wa muda, kwa sababu leo ni mwezi

umetimia, shule zimefunguliwa. Ni upi mkakati wa haraka wa kuhakikisha vitabu vinafika na elimu inafika kwa wakati ili watoto waweze kupata elimu hiyo kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali na kupokea ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia. Kwanza nimhakikishie kuwa tumeendelea kuzalisha vitabu kulingana na mahitaji ya mtaala tulionao. Wakati huu tunapoanza kufundisha kwa Sera mpya ya Elimu kwenye mitaala mipya, kwenye mipango yetu ya bajeti, ndiyo tumesema tumeanza awamu kwa awamu. Hatukuanza *full string*, yaani hatukuanza madarasa yote. Tumeanza na awali, darasa la kwanza, darasa la tatu, na kidato cha kwanza kwa sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeanza hivyo ili kujipa uwezo wa kupata vifaa, miundombinu ikiwemo na vitabu vya kujifunzia na kufundishia. Mkakati huu kama nilivyosema mwanzo kwamba tunaendelea kuongeza uwezo wa Serikali kibajeti kila mwaka ili kusheheneza maeneo haya, kumfanya mwanafunzi aweze kuipata ile elimu na aendelee nayo hata kule mwisho anapopimwa, apimwe akiwa ana uelewa na mahali pa kupata vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ya Elimu imeweka mpango wa kuimarisha elimu ya TEHAMA ambayo pia itasaidia wanafunzi kupata taaluma hiyo kupitia mitandao yetu na kumwezesha kuwa na uwanda mpana wa kupata elimu kwa vitabu ambavyo tunapeleka, na hata kwenye mitandao ili iweze kumsaidia kuelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mpango wetu wa Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa majibu sahihi. Umetoa takwimu ambazo kwa kweli watu wengi hawazijui. Ahsante sana na hongera sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc*. – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya kawaida. Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mpembenwe.

Na. 39

### Ukarabati wa shule za msingi chakavu – Kibiti

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa shule chakavu za msingi Jimbo la Kibiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Jimbo la Kibiti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ukarabati wa shule chakavu ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilipeleka shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Msingi Kiasi. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Serikali imepeleka

shilingi milioni 180 kwa ajili ya kukarabati shule chakavu za msingi katika Jimbo la Kibiti ambapo jumla ya shule nne zitakarabatiwa ambazo ni Pongwe (maradasa matatu yalikarabatiwa), Mchinga (madarasa mawili), Saninga (madarasa mawili) na Misimbo (madarasa mawili).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Pamoja na hayo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweza kujenga shule mpya katika Jimbo la Kibiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba kuuliza: Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuweza kukarabati Shule ya Msingi ya Mchukwi pamoja na Shule ya Msingi ya Nyanjati iliyopo katika Kata ya Mahenge?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, hili la kwanza la mpango wa Serikali kujenga shule mpya katika Wilaya ya Kibiti, nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kupitia Mradi wa *Boost*, imejenga shule mbili mpya katika Jimbo lake la Kibiti. Jumla ya shilingi milioni 821 zilipelekwa katika Halmashauri ya Kibiti kujenga shule hizo ambazo ipo ya Itonga Kata ya Bungu na vilevile kuna shule inaitwa Mpembenwe ambayo

imejengwa, ilipelekewa shilingi milioni 306 kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye swali la pili sasa. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe amekuwa akiifuatilia sana juu ya ujenzi wa shule hizi za Mchukwa na nyingineyo ambayo imetajwa. Namtoa mashaka, Serikali hii itatafuta fedha na kuweza kupeleka kwa ajili ya ukarabati wa maeneo haya ambayo ameyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kule Kibiti kuna shule mpya ya Sekondari ambayo sasa fedha imepelekwa kwa jitihada zake Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa fedha kwa ajili ya kujenga shule katika Kata ya Kibiti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa, jiandae Mheshimiwa Sanga.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwenye Jimbo la Igunga, kuna changamoto kubwa sana kwenye Shule ya Msingi Butamisuzi Kata ya Mbutu na Mwajinjama. Tunaishukuru Serikali, Shule ya Msingi ya Buta wametupatia fedha kuboresha madarasa chakavu. Imebaki changamoto kwenye Shule ya Msingi Mwajinjama iliyopo Kata ya Mtungulu: Je, ni lini Serikali mtapeleka fedha kwa ajili ya kutusaidia kuboresha madarasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngassa, kwa sasa kuna tathmini ambayo ilikuwa inafanyika na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia kwa Maafisa Elimu wetu wa Msingi katika Halmashauri zote hapa nchini ili kuweza kupata taarifa sahihi ya idadi ya madarasa yanayohitajika ili fedha iweze kutafutwa na kupelekwa. Vilevile kule kwa Mheshimiwa Ngassa, itafanyika hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, jiandae Mheshimiwa Matiko.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kutokana na uchakavu wa majengo kwenye shule za msingi kule Makete, Waratibu Kata Elimu leo wamekuja kutoka Makete wako hapa wanataka kujua ni lini Serikali itapeleka fedha za kukarabati Shule ya Msingi Lupalilo, Shule ya Msingi Ikungula, Shule ya Msingi Iwawa na Shule ya Msingi Kijombo? Waratibu wangu wa Elimu Kata wako hapa leo, wanataka waondoke na majibu ya Serikali. Ni lini fedha zitatoka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, fedha itapelekwa na Serikali katika Shule za Msingi Lupalilo, Ikungula na maeneo mengine ambayo ameyataja Mheshimiwa Sanga hapa kadri ya upatikanaji wa fedha hizo. Kama nilivyomjibu Mheshimiwa Ngassa, kwa hiyo na tathmini inayofanyika hivi sasa na baada ya tathmini hiyo kukamilika, Serikali itatafuta fedha hizo na kuweza kupeleka huko.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru...

**NAIBU SPIKA:** Jiandae Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule za msingi ambazo ni kongwe zimejengwa miaka ya 1960 na 1970 ambazo hazifai kabisa kukarabatiwa bali inabidi Serikali iende na mkakati wa kuzijenga upya. Mathalan Shule ya Msingi Nyabilongo, Kikomori na Kiongera zilizopo Kata ya Susuni, Jimbo la Tarime Vijijini. Ni shule ambazo ni hatarishi hata kwa wanafunzi wanaposoma katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inapeleka fedha kwa uharaka ili hizi shule kongwe ziweze kujengwa na kuweza kunusuru maisha ya wanafunzi wale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Matiko, kwanza niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi hiki cha uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndiyo kipindi ambacho Serikali hii ya Awamu ya Sita imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 230 katika ujenzi wa shule mpya na ukarabati wa madarasa kwenye Elimu Msingi kuliko wakati mwingine wowote ule. Hivyo basi, nimtoe mashaka Mheshimiwa Matiko, shule hizi alizozitaja tutaziweka katika mpango na kuona ni namna gani fedha inazifikia kwa ajili ya ukarabati wa madarasa na ujenzi wa majengo mapya katika shule hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tunaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ya ukarabati na ujenzi wa shule mpya hapa nchini. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga nyumba za walimu ambazo hazifai kabisa katika hizo shule kongwe nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikimjibu Mheshimiwa Issaay, kutoka mwaka 2021 hadi 2023, Serikali hii imejenga zaidi ya nyumba 562 za walimu kote nchini ambapo imetumika zaidi ya shilingi bilioni 56,325,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zaidi za walimu kama ambavyo umeona jitihada hizi zinafanyika kwa sasa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 40

**_TBA_ kujenga nyumba za walimu nchini**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaingia ubia na Wakala wa Nyumba Tanzania *(TBA)* kuwajengea nyumba walimu nchini na kisha kuwakata mishahara yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mahitaji ya nyumba kwa ajili ya walimu ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2021 hadi 2023 zimejengwa nyumba 562 zenye uwezo wa kuchukua familia 1,124 kwa thamani ya shilingi 56,325,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa pendekezo la Mheshimiwa Mbunge ni la msingi na linahusisha ujenzi wa nyumba ambazo itabidi Walimu wazilipie kupitia mishahara yao, Serikali itakaa kwanza na

walimu ili kulijadili na endapo wataafiki wazo hilo litawasilishwa kwa Wakala wa Nyumba Tanzania *(TBA)* kwa ajili ya makubaliano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa majibu, lakini lengo la swali langu lilikuwa ni Serikali kuingia ubia na *TBA,* kwanza halmashauri watenge maeneo ya makazi, waingie mkataba na *TBA,* wajenge nyumba za gharama nafuu, ambazo walimu watagawiwa kwa mkataba ambao wataingia nayo. Kwa maana ya kwamba zile nyumba ambazo watamiliki wao hata kama ukistaafu itakuwa nyumba za kuanzia maisha sio nyumba za shule ambazo zinamilikiwa na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu je, Serikali haioni namna bora ya kuwasaidia walimu hasa wale wastaafu wanapotangatanga baada ya kukosa makazi na umri wao wa kuishi nao unapungua kwa sababu ya *stress* za kukosa makazi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwajengea nyumba walimu hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, kwanza nikiri tunapokea mawazo na maoni ya Mheshimiwa Kuchauka aliyoyatoa na kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi ya kwamba itabidi tukae na walimu wenyewe kwa sababu jambo lenyewe ni la hiari la wao kuweza kuchangia au kukatwa katika mishahara yao kulipia nyumba zile ambazo zitakuwa zimejengwa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukubaliana nao ndipo basi Serikali itakaa ubia na *TBA*, *National Housing,* Watumishi *Housing,* taasisi nyingi nyingine na Serikali kwa ajili ya kuona ni namna gani nyumba hizi zinaweza zikajengwa kwa ajili ya kuweza kuwauzia walimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Bagamoyo kuna nyumba nyingi sana za *TBA* ambazo ni chakavu; je, ni lini Serikali itakwenda kukarabati nyumba zile na kujenga nyingine mpya ili watumishi wa Serikali wapate sehemu ya kuishi?

**NAIBU SPIKA:** Hello, Mheshimiwa swali lako haliendani na swali la msingi kaa chini. Mheshimiwa Nashon, tunaendelea.

Na. 41

**Ahadi ya shilingi milioni 10 ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kazuramimba**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi ya shilingi milioni 10 za ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kazuramimba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Kituo cha Afya Kazuramimba. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri ilitenga shilingi millioni 158 na kuendeleza ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* ambalo ujenzi wake upo katika hatua za ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia vyanzo mbalimbali...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge tusikilize majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kupitia vyanzo mbalimbali na kuhakikisha inajenga na kukamilisha vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati kote Nchini kikiwemo kituo cha Afya Kazuramimba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nashon.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali langu la nyongeza, kwamba kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kazuramimba ni kata ya kimkakati. Sasa ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga majengo mengine? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bidyanguze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari imeshaainisha maeneo yote ya kata za kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwa awamu na mpaka sasa imeshajenga vituo vyake 466 vyenye thamani ya shilingi bilioni 718 na Kituo cha Afya cha Kazuramimba ni miongoni mwa vituo hivyo ambavyo vitatengewa fedha kwa ajili ya majengo mengine, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi pamoja na jitihada hizo nzuri za Serikali lakini vituo vingi vya afya ikiwemo cha Bumilainga na Ifingo bado havijakuwa na miundombinu ya kutosha ikiwemo kuwepo wodi ya akinamama na wodi ya wanaume.

Je, Serikali iko tayari kwenda awamu ya pili kwa kuanza kujenga *facilities* hizo muhimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwakikishie tu kwamba Serikali iko tayari kuendelea na ujenzi wa majengo ya wodi za wanawake na wanaume katika Kituo cha Afya cha Ifingo na kituo hicho alichokitaja pia katika vituo vyote ambavyo vimejengwa awamu ya kwanza vyote vitakwenda awamu ya pili kwa ajili ya kukamilisha miundombinu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki.

Na. 42

**Kutoa kipaumbele kwa eneo lililoathirika na mabadiliko ya tabianchi**

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI** aliuliza: -

Je, sababu zipi zinasababisha eneo linaloathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kupewa kipaumbele cha utekelezaji wa Mradi ili kunusuru hali hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mbunge wa Jimbo la Nungwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi yanazidi kusababisha athari katika maeneo mbalimbali ya nchini yakiwemo maeneo ya ukanda wa pwani nchini. Katika kubainisha maeneo yaliyoathirika na kuyaweka katika kipaumbele, Serikali inafanya tathmini ya kiwango cha uharibifu na athari zilizojitokeza hii ni moja ya sababu mojawapo ya vigezo vinavyotumika katika kuweka kipaumbele maeneo yaliyoathirika katika mipango ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kubaini maeneo mbalimbali yenye changamoto kubwa ya uharibifu wa Mazingira na kuyaweka katika kipaumbele ili kuyatafutia rasilimali fedha, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Simai.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuwa mara nyingi nimekuwa nikisimama Bungeni hapa na kutaka kujua hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoendelea kuwaathiri kule Nungwi lakini majibu yamekuwa yakitofautiana katika swali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanataka kujua je, eneo lile unalolizungumzia hapa kwamba bado halijakidhi vigezo na masharti vilivyowekwa ili kuweza kupewa kipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa tafiti nyingi zimeshafanyika katika kubaini athari za mabadiliko ya tabianchi kule maeneo ya Nungwi katika maeneo ya jamii na maeneo ya fukwe.

Je, Serikali kupitia Wizara yako ina mkakati gani au inawahakikishiaje wananchi kutengewa fedha katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika eneo lile?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii nimpongeza Mheshimiwa Simai kwa kazi nzuri anayoifanya hasa kutokana na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi na jinsi ambavyo anawasaidia na kuwasemea wananchi wake kwenye Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo linatakiwa lijengwe ukuta kwa upande wa Nungwi limekidhi vigezo na lina kila sababu ya kufanya hivyo na ndio maana tumeanza kufanya utafitii na ndio maana viongozi wa SMZ na SMT wameshafika pale na ndio maana tumeshaliombea bajeti kwa ajili ya kulifanyia kazi kwa sababu tumeona athari ya kwamba pale pana kila sababu ya kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Msheshimiwa Simai kwamba kutokana na vigezo hivyo tulivyovitaja eneo lile lina kila sababu ya kushughulikiwa na kusaidiwa na kufanyiwa kazi kama ambavyo Serikali imeliahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Nungwi niwaambie kwamba athari ya kuingia maji ya chumvi kwenye mitaa ama kwenye makazi ya wananchi hili jambo niwaambie linaenda kuondoka na ukuta ambao wanaulalamikia unakwenda kujengwa. Kwa nini utajengwa? Kwa sababu kwanza Serikali imeguswa na jambo lile lakini utakwenda kujengwa kwa sababu tayari tumeshaanza kujenga kuta kama hizi, tumejenga kule Pemba, Sepwese na tumeanza kujenga kule Mtwara Mikindani maana yake na Nungwi tunakwenda kujenga ukuta huu, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba niulize swali moja. Mtambwe Mkuu ni kisiwa cha historia ambacho kwa kiwango kikubwa kimevamiwa na maji ya chumvi kiasi ambacho wananchi wanahama. Je, na hichi hakijapata kipaumbele cha kuonekana ipo haja ya kushughulikiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja miongoni mwa kazi kubwa ambayo tumeamua sasa tuanze kuifanya ni kuhakikisha kwamba tunarejesha mazingira yaliyoharibika kutokana na maji ya chumvi kwenye maeneo ya visiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya miongoni mwa maeneo ambayo tumeshataka kuyapa kipaumbele ni eneo la hichi Kisiwa cha Mtambwe Mkuu. Kubwa tu nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba na yeye aendelee kutusaidia kusema na wananchi. Shughuli hizo zinazoendelea za kibinadamu zisiendelee kuliathiri visiwa vyetu, shughuli za utalii, shughuli za uvuvi, shughuli nyingine za ulimaji wa mwani zione namna ambavyo zinatunzwa na kuhifadhi mazingira haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kisiwa cha Mtambwe Mkuu tunakwenda kurekebisha ili kuondosha athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuendelee na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Genzabuke.

Na. 43

**Kukosekana kwa chujio la maji Kasulu**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, lini Halmashauri ya Mji wa Kasulu itaondokana na matumizi ya maji machafu kutokana na ukosefu wa chujio?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Gezabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna ukosefu wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu. Ili kutatua changamoto Serikali imekamilisha ukarabati wa chujio la maji la Kabanga ambalo limeanza kufanya kazi. Chujio hilo lina uwezo wa kuchuja maji jumla ya lita 1,000,000 kwa siku. Aidha, ujenzi wa machujio ya maji kutoka vyanzo vya Mto Chai na Miseno umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2024. Machujio haya yatakuwa na uwezo wa kuchuja maji jumla ya lita 3,000,000 kwa siku. Kwa sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mradi wa maji wa miji 28 imeanza ujenzi wa chujio la maji kutoka chanzo cha maji cha Mto Ruchunji. Kwa sasa mradi huo utekelezaji wake umefikia asilimia 5 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Aprili, 2025 ambapo chujio hilo litakuwa na uwezo wa kuchuja maji jumla ya lita 15,000,000 kwa siku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza; kwanza nishukuru Serikali kwa kuweka Mji wa Kasulu kati ya miji 28 itakayonufaika na mpango wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kwa wakati huu ambapo kuna mlipuko wa kipindupindu je, Serikali ina mpango upi wa dharura wa kuweza kuwasaidia wananchi wa Kasulu ili kuondokana na tatizo la maji machafu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili katika Halmashauri ya Kasulu *DC* zipo kata ambazo tayari zimeshachimba visima lakini maji hayajasambazwa kutokana na ukosefu wa miundombinu ya mabomba. Kata hizo ni Kata ya Kasangezi, Lusesa, Hurugongo na Shunguliba. Ni lini Serikali itamaliza matatizo hayo katika kata hizo nilizozitaja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tupokee pongezi zako na tumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ameweza kupigania huu mradi wa miji 28 sasa tayari unatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mlipuko wa kipindupindu Mheshimiwa Genzabuke sisi kama Wizara tuko imara sana kuona kwamba kama chujio halipo lakini tunatibu maji kwa kutumia *chlorine* hatutoi maji bila kuyatibu. Kwa hiyo, huenda maji yakawa na tope kidogo lakini yametibiwa na *chlorine*. Kwa hiyo, vidudu vinakuwa vinauliwa na tunawasihi wananchi kuhakikisha wanachemsha maji, wanakula vyakula vya moto ili tuweze kupunguza maambukizi ya kipindupindu.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima tayari, bado kusambaza, tayari Serikali tumeanza kufikia visima vyote vilivyochimbwa na vina maji ya kutosha kuona tunaleta usambazaji. Vilevile kama kisima kina maji kidogo tunaweka japo vichotea maji viwili, vitatu katika lile eneo ili wananchi waweze kufikiwa. Hivyo nikupongeze dada yangu Mheshimiwa Josephine kwa ufatliaji huo na niseme kwamba tutakuja kuhakikisha visima vyote vilivyochimbwa vinaweza kuleta tija ya wananchi kupata maji safi na salama bombani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Mradi wa Maji wa Malampaka Male utaanza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Esther, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Malampaka upo kwenye hatua za mwisho kabisa na kuona kwamba tunaanza kuutekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa ziara yake nzuri

aliyoifanya katika Wilaya ya Lushoto na sasa maji yanatiririka pale kwenye Kata ya Kwai. Naomba kuuliza ule mradi mkubwa ambao uta-*cover* kata 13 za Wilaya ya Lushoto ni lini utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ulenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kukushukuru kwa pongezi zako lakini kwa kazi kubwa na wewe unayoshiriki kuifanya katika Jimbo la Lushoto katika majimbo yale matatu ushiriki wako niliweza kuukuta na hongera sana pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mradi huu wa kata 15 ambao umeutaja tayari Serikali tunaendelea na hatua za mwisho kabisa ili tuweze kuja kuuanza mara moja na utekelezaji utaendelea mwaka ujao wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Madini Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

Na. 44

**Kuwapa wachimbaji wadogo leseni zisizofanyiwa kazi**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta Leseni za Madini ambazo hazifanyiwi kazi na kuwapa Wachimbaji Wadogo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Jimbo la Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na mpango endelevu wa kufuta leseni zisizoendelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini, Sura ya 123. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa sekta ndogo ya uchimbaji mdogo nchini ikiwa ni pamoja na kuchangia katika maduhuli ya Serikali na kutoa ajira kwa watanzania waliowengi. Serikali imekuwa ikitenga maeneo mbalimbali yanayofaa kwa uchimbaji mdogo ambayo leseni za madini katika maeneo hayo zimefutwa au kumaliza muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023 pekee, Serikali iliwatengea wachimbaji wadogo jumla ya maeneo 39 yenye ukubwa wa Kilomita za mraba 559.64 katika maeneo mbalimbali nchini; na katika Wilaya ya Kahama ambayo inabeba Jimbo la Msalala, jumla ya leseni 317 zisizofanya kazi zimefutwa na maeneo matatu yametengwa kwa ajili ya wachimbaji wapya wadogo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga maeneo yanayofaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kadri yanavyopatikana ili waendeshe shughuli zao kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 na Kanuni zake, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutenga maeneo haya kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo; na kwa kuwa tayari imeshatenga maeneo haya na kuwapatia wachimbaji wadogo. Nini mkakati sasa wa Wizara wa kuhakikisha kwamba inawapatia taarifa za tafiti kwenye maeneo hayo ili iweze kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mheshimiwa Rais aligawa vifaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo sasa nilitaka

kufahamu ni lini sasa vifaa hivyo vitaanza kufanya kazi kwenye maeneo haya ya wachimbaji wadogo wadogo sambamba na kuwapatia pia mashine watu wanaochimba madini ya ujenzi kama kokoto? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za utafiti ambazo Mheshimiwa Mbunge anaziulizia zinapatikana kupitia mpango wa Wizara wa *Vision 2030* ambao unaenda kufanya utafiti wa kijiolojia katika maeneo yote nchini kubaini maeneo yenye madini ili wachimbaji wadogo waweze kuelekeza ipasavyo wasifanye uchimbaji wa kubahatisha wa kiramli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa vifaa vya uchimbaji kwa wachimbaji wadogo, kwanza *STAMICO* yenyewe kupitia fedha alizotupa Mheshimiwa Rais mwaka jana mwezi wa kumi wakagawa vifaa na mitambo ya uchorongaji. Mitambo hiyo imeendelea kusambazwa na kufanya kazi katika maeneo mbalimbali nchini kama vile Mara na Geita, na sasa hivi wana mpango wa kufanya Chunya, na shughuli hizo za uchorongaji wanaendelea kuzifanya wiki ijayo hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vifaa vingine kwa wachimbaji wadogo vinapatikana kupitia utaratibu tuliowekeana na benki zilizokubali kutoa mikopo kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambao wamejipanga na wamefikia vigezo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo, ajiandae Mheshimiwa Condester.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya Serikali kupitia Wizara hii ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapa maeneo ambayo yatafaa kwa

uchimbaji mdogo katika vitalu vya makaa ya mawe kule Njombe na Ludewa.

Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Deo kwamba utaratibu wa kugawa vitalu vya makaa ya mawe kwa wachimbaji wadogo katika Mkoa wa Njombe ulicheleweshwa sana na mfumo uliokuwepo kati ya *NBC* ambayo ilikuwa na wawekezaji wengine waliokuwa wafanye uchimbaji mkubwa wa makaa ya mawe kule Liganga na Mchuchuma. Lakini kwa utaratibu unaoendelea sasa hivi wa kubadilishana vijiti, na pengine sisi ndio tukawa wasimamizi wakuu wa yale maeneo tutakwenda kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanapata maeneo ya kuchimba madini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuzifuta leseni nauliza kwamba Wizara ya Madini ina mkakati gani wa kuwahamasisha wachimbaji wadogo wadogo kuzitafuta leseni za madini ya *green tourmaline* pamoja na *sodalite* ambayo yamegundulika kuwepo Chingi Msangano kwenye Jimbo la Momba? Na kwa sasa hivi kuna mchimbaji mmoja tu amepata, jihitahada za kuhamasisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Condester, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa Wizara ya Madini ni kugawa leseni kwa Mtanzania yeyote ambaye amepata eneo linalobainika kuwa na madini. Lakini kwa upande wa uhamasishaji

sisi tumekuwa na utaratibu wa kuzunguka kila mkoa kutoa elimu juu ya Sheria ya Madini na taratibu za kutafuta leseni za madini. Sambamba na hilo sasa, kwa sababu tunakwenda kufanya utafiti takriban nchi nzima kufikia mwaka 2030 tuwe tumefanya asilimia 30 kila Mtanzania atafahamu maeneo yenye madini anayoyataka na utaratibu wa kumpa leseni utaendelea kwa mujibu wa sheria na kanuni zetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Rashid Shangazi.

Na. 45

**Uhitaji wa somo la uchambuzi katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha somo la uchambuzi wa michezo katika Chuo cha Michezo Malya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya kinafundisha michezo kwa kutumia Mitaala iliyopitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafuzo ya Ufundi Stadi *(NACTVET)*. Chuo hiki kinafundisha programu tatu; Programu ya Elimu ya Viungo vya Mwili *(Physical Education),* Elimu ya Ufundishaji wa Michezo *(Sports Coaching),* Uongozi na Utawala katika Michezo *(Sports Management and Administration)*. Katika programu hizi,

michezo mbalimbali hufundishwa kama somo. Mfano mpira wa miguu, netiboli, mpira wa kikapu, riadha, mpira wa wavu n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi katika michezo ni sehemu ya mada zinazohusiana na michezo husika ambazo ziko katika mitaala hasa sheria zinazoutawala mchezo. Hata hivyo, Serikali inaangalia mahitaji ya soko katika kipindi cha kuhuisha mitaala na endapo kutakuwa na uhitaji mkubwa, somo la uchambuzi wa michezo litaanza kufundishwa chuoni hapo kama somo huru, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali lakini ni ukweli kwamba sasa hivi suala zima la uchambuzi ni fursa kwa vijana wengi kupitia *radio* na *television* na kadhalika.

Sasa swali langu; kwa kuwa wanaochambua wengi ni Waandishi wa Habari na Watangazaji wa Habari za Michezo; Je, Serikali iko tayari pia kuzungumza na hivi vyuo ambavyo vinafundisha uwaandishi wa habari za michezo na utangazaji ili waweze kuwa sehemu ya huu mchakato wa kuanzisha hii kozi mpya ya uchambuzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa tunaye Mkurugenzi wa BMT, ndugu Ally Mayayi ni miongoni mwa wachambuzi mahuri, ndugu Jemedari Said Kazumari, George Ambangile, akina Ramadhani Mbwaduke na Amri Kiemba. Je, Serikali iko tayari kuanza na hao hao wakongwe ambao wanafanya kazi hii vizuri kuwafanya kama darasa kwa wanahabari wengine wachanga ili waweze kuwasaidia katika kipindi hiki cha mchakato kuelekea kuanzisha mtaala mpya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Rashid Shangazi. Kwanza Serikali itakuwa tayari kujadiliana na vyuo vinavyofundisha masuala ya uandishi wa habari kwa ajili ya kuongeza mtaala huu wa uchambuzi wa habari za michezo kama ambavyo tunafanya juhudi sasa hivi. Mchakato umeishaanza kuhakikisha Chuo cha Michezo cha Malya kinakuwa na mtaala wa kufundisha uchambuzi wa michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili hili la kuwatumia wakongwe. Kwanza Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa sasa imeshaanza kuwatumia wakongwe katika shughuli mbalimbali. Kwa mfano hivi karibuni wakati Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo alipoteua Kamati kwa ajili ya hamasa ya Timu ya Taifa alimteua ndugu Jemedari Said kuwa miongoni mwa sehemu ya kamati ile. Lakini tumechukua maoni ya Mheshimiwa Mbunge, na nimuhakikishie kwamba waandishi hawa wa habari za michezo ambao wanafanya shughuli za uchambuzi kwa umahiri na weredi mkubwa, tutawatumia kama sehemu inayotoa mafunzo kwa ajili ya waandishi wengine ambao wanataka kufanya shughuli za uchambuzi wa michezo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tunashukuru Serikali kwa kuanzisha Chuo hiki cha Malya na nimesikia masomo yanayofundishwa pale.

Je, Serikali haioni umuhimu wa mchezo wa ngumi na makamisaa wa ngumi wakaingizwa katika chuo hicho ili waweze kupata mafunzo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda promota maarufu wa ngumi, kwamba maoni yake tumeyachukua na tutaangalia uwezokano wa kuanzisha mtaala wa mafunzo ya ngumi kwenye Chuo cha Michezo cha Malya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Maige, kwa niaba ya Mheshimiwa Kakunda.

Na. 46

**Asali kuwa zao la kimkakati**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA K.n.y. MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya asali kuwa moja ya mazao ya kimkakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji wa nyuki ni moja ya shughuli muhimu za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kwa makabila mengi hapa nchini, hususani kwa jamii inayoishi kando kando ya maeneo yanayohifadhiwa; vilevile kwa Afrika na katika maeneo mengi duniani. Aidha, ufugaji wa nyuki una mchango mkubwa katika kuhakikisha usalama wa chakula kupitia uchavushaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa shughuli hii, Serikali imechukua hatua kadhaa za kufanya asali kuwa zao la kimkakati. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya usimamizi pamoja na kutoa miongozo mbalimbali inayohusu ufugaji nyuki; kuwezesha wafugaji nyuki kwa kuwapatia mizinga ya kisasa. Mathalani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita zaidi ya mizinga ya kisasa 64,593 imetolewa kwa vikundi vya wafugaji nyuki kutoka katika mikoa mbalimbali. Sambamba na hilo, Serikali imewezesha ujenzi wa viwanda saba vya kuchakata na kufungasha asali katika Wilaya za Sikonge, Mlele, Nzega, Tabora, Manyoni, Kibondo na Bukombe vitakavyotumika kuongeza thamani ya asali inayozalishwa na kuuzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, Serikali inatekeleza programu na miradi mbalimbali ya kuwezesha kuongeza uzalishaji wa asali sambamba na kutafuta masoko mapya ya asali katika nchi za Umoja wa Ulaya na Asia. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo inatekeleza mradi wa kuwezesha ufugaji wa nyuki katika mikoa mitano. Mkoa wa Tabora, Singida, Katavi, Kigoma na Shinyanga kwa upande wa Tanzania Bara, lakini vilevile katika Kisiwa cha Pemba kwa upande wa Zanzibar. Vilevile, Serikali inakamilisha Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki ambao utachochea uzalishaji, mauzo ya asali nje ya nchi pamoja na ajira hasa kwa vijana na wanawake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, Serikali imeleta majibu mazuri; hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza utangulizi mazao yote ya kimkakati katika nchi hii ambayo yanafahamika yameandaliwa mikakati maalumu na bajeti ambayo imeletwa hapa Bungeni na tukaipisha, kuhusu utafiti, uendelezwaji kwa maana ya huduma za ugani, uvunaji, uhifadhi, uchakataji, ufungashaji na hatimaye kuyafikia masoko *(marketing intelligence)*.

a) Je, Serikali itaandaa mkakati maalumu kwa ajili ya zao hilo la asali lini?

b) Je, makakati huo utaletwa Bungeni lini ili wananchi waweze kuufahamu vizuri zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na eneo la mpango wa kuendeleza zao hili la asali, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi. Nilieleza kwamba Serikali kwa sasa inakamilisha mpango wa kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki ambao utachochea uzalishaji, mauzo ya asali nje ya nchi pamoja na ajira hasa kwa vijana. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda ili tuweze kukamilisha jambo hili. Nimuhakikishie kwamba tuko hatua za mwisho tutakapokamilisha tutawafahamisha Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Khenani.

Na. 47

**Changamoto ya kukatika kwa umeme - Nkasi**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza changamoto ya kukatika kwa umeme Wilaya ya Nkasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi inapata umeme kupitia njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 66 kutoka Zambia. Kwa kutambua changamoto ya kutokujitosheleza kwa umeme, Serikali imeshaanza mradi wa kupeleka umeme kutoka Gridi ya Taifa kwa Mkoa wa Rukwa ambapo Mkoa utapata umeme kupitia utekelezaji wa Mradi wa *TAZA* ulioanza kutekelezwa mwezi Novemba, 2023 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2026. Kwa sasa *TANESCO* inaendelea kufanya maboresho ya miundombinu ili kupunguza kukatika kwa umeme mara kwa mara na kujenga kituo cha kupooza umeme, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Nimesikia majibu ya Serikali, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa tunaamini kwamba kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa ndio itakuwa utatuzi lakini maeneo ambayo tayari walishaunganishwa bado umeme unakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitujibu hapa mwaka jana kwamba changamoto ya kukatika kwa umeme inatokana na upungufu wa maji. Kwa sasa maji ni mengi na mafuriko juu nini sababu nyingine inayopelekea umeme kukatikakati nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Wilaya ya Nkasi nguzo za miti zinaanguka mara kwa mara zinapelekea changamoto ya kukatika kwa umeme na athari kubwa hasa kwa

wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla. Hamuoni kuna haja sasa ya kupeleka nguzo za zege kwa upendeleo ili kuondokana na hiyo changamoto? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza. Moja, maeneo mengi ambayo tumeona yanamafuriko yalipata mvua za *El Nino,* lakini maeneo ambayo ni *catchment areas* ya mabwawa hazikuwa kwenye mvua za *El Nino;* kwa hiyo zinapata maji kwa mvua mbazo zinaendelea sasa hivi. Hata hivyo kwa mvua ambazo zinaendelea tayari maji yameishaimarika kwenye mabwawa. Kuna kipindi mabwawa yalikuwa yanazalisha megawati 254 kwa siku, lakini tunavyoongea leo mabwawa yetu yameongezeka yanazalisha megawati 426; na upungufu umepungua kuanzia megawati 400 na leo tunavyoongea mpaka asubuhi tunaupungufu wa megawati 144. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme kadri ambavyo vyanzo vinajitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na nguzo za zege tayari tumeishapeleka Mkoa wa Rukwa nguzo za zege 1,000 na Wilaya ya Nkasi kwa kuanzia itapata nguzo mia moja ili kuboresha hali ya miundombinu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme mara mara katika Jimbo la Mbagala, na Mheshimiwa Naibu Waziri umekuwa ukifanya ziara mara kwa mara katika Jimbo hilo.

Je, nini sababu za msingi za kukatika kwa umeme katika Jimbo hili? na ni hatua gani zinachukuliwa kuondokana na tatizo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mbagala ni moja wapo ya maeneo ambayo yanakua kwa kasi sana, na yanaongezeka kiuchumi kwa kuwa baadhi ya viwanda pia vipo mbele ya Mbagala kwenye ukanda wa Pwani na kwa hiyo inasabibisha ongezeko la matumizi ya umeme kwa kiasi kikubwa kiasi kwamba kituo cha kupooza umeme cha Mbagala kimezidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumetoa fedha ya kuongeza ukubwa wa kituo, na sasa hivi mashine umba ipo njiani kwa ajili ya kuwasili kwenye kituo cha Mbagala ili tuweze kuifunga na kuongeza uwezo wa kituo cha kupooza umeme Mbagala ili wananchi wa Mbagala waweze kupata umeme wa uhakika. Tunaendelea na kuboresha miundombinu ili kupunguza hali ya kukatika katika umeme katika Eneo la Mbagala, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufika Kilombero na kufanya ziara pale. Naishukuru Serikali kwa kutupatia shilingi bilioni 25 za mradi mkubwa wa umeme. Tuliambiwa kwamba mradi huo ukikamilika kutapungua mgao wa umeme Ifakara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kilombero ina migodi miwili ya kuzalisha umeme ya Kidatu na Kihansi, na kwa kuwa umeme huo ukisafirishwa mpaka Dodoma hapa unafika na hakuna mgao na haukatiki.

Je, ni lini tatizo la mgao kukatika kwa umeme Ifakara na Kilombero ambako sisi tunazalisha umeme litaisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimpe Mheshimiwa Mbunge pole kwa changamoto hiyo ya kukatika katika kwa umeme. Pamoja na kuboresha miundombinu kwa kuweka kituo kikubwa cha kupooza umeme pale Ifakara, wote tunafahamu tuna upungufu wa umeme na tuna mgao. Kwa hiyo tuwaombe tu mtuvumilie mpaka mwezi wa pili ambapo tumehaidi Bwawa la Mwalimu Nyerere litaanza kuzalisha umeme na hapo tutakuwa tumetengemaa katika hali ya upatikanaji wa umeme siyo tu kwa Kilombero bali kwa nchi yote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru mpaka sasa ninapoongea Songwe mahali ambapo ndipo kwenye lango kuu la *SADC* umeme hakuna na hii changamoto hakuna kipindi cha mvua, hakuna kipindi cha kiangazi Serikali mnatuambiaje kwenye hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Songwe kama ilivyo kwa Mikoa mingine ipo kwenye mgao wa umeme na hii ni changamoto kwa Mikoa yote. Lakini kwa sasa hivi kama nilivyowaambia Waheshimiwa Wabunge tumepunguza kwa kiasi kikubwa hali ya upatikanaji na mapungufu yamepungua kwa kiasi. Kwa hiyo, tunaendelea kuwaomba ifikapo tarehe 16 Februari, mwezi ujao tutakuwa tumekamilisha majaribio kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere na hivyo tunategemea megawati za mwanzo 215 tutaanza kuzipata. Kwa hiyo tumebakisha muda mchache sana ukilinganisha na kule ambapo tumetokea, tunaomba muendelee

kutuvumilia ili tuweze kukamilisha zoezi hili na hivyo kuwahakikishia mnapata umeme wa uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa ambayo haijaunganishwa na Gridi ya Taifa. Tunafahamu jitihada za Serikali za kupeleka umeme kwenye mkoa huo. Wakati Serikali inajipanga kupeleka Umeme wa Gridi ya Taifa ni hatua gani zinazochukuliwa za dharura kupeleka jenereta mpya ili kuweza kukidhi mahitaji ya Wananchi ya Mkoa wa Katavi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunao mradi wa kuhakikisha Mkoa wa Katavi unaunganishwa kwenye gridi ya Taifa na tayari vituo vya kupooza umeme vingi vimekamilika na vingine vipo kwenye hatua nzuri. Sasa hivi nguvu imeelekezwa kwenye kujenga *lane* ya kusafirishia umeme ambayo pia imefikia hatua nzuri. Tunategemea mpaka kufikia Mwezi Septemba mwaka huu mradi huu utakuwa umefikia eneo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu aliloshauri Mheshimiwa Mbunge tutaliangalia kuona kama linaweza kufanikiwa lakini kwa kipindi hiki ambacho Serikali tumeweka fedha ya kuunganisha Katavi kwenye Gridi ya Taifa tunaomba wananchi wa Katavi waendelee kutuvumilia, tunawahakikishia tutasimamia mradi huu kwa ufanisi mkubwa sana ili ukamilike kwa wakati na wapate umeme wa uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninawapongeza Mawaziri wote waliojibu maswali leo, mmejibu sahihi, inaelekea Wizara zenu mnazifahamu vizuri sana. *(Makofi)*

Maswali yamekwisha sasa ni kipindi cha wageni; wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni waliopo Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Spika na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* ambao ni Chama cha Wanafunzi Wahitimu 65 wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu vya Kati Tanzania (CHAWAKITA), kutoka Chuo Kikuu Teofilo Kisanji *(TEKU),* Mkoa wa Mbeya, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Festo Sanga ambao ni Maafisa wa Elimu kutoka Kata ya Makete, Mkoa wa Njombe, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Makuru Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Kasaka, mdogo wake kutoka Ubalozi wa Uholanzi, karibu. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambao ni wafanyakazi wa Hospitali ya Aga Khan, Mkoa wa Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Mbagala Mkoa wa Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni ndugu zake kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Waheshimiwa Wabunge na Wanachama wa Klabu ya Simba, Tawi la Wekundu Mjengoni ambao ni wachezaji na viongozi wa timu ya *Simba Queens. (Makofi)*

*(Hapa Wabunge waliwashangilia wachezaji na viongozi wa timu ya Simba Queens)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa inatosha.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 41 ambao ni Maspika na Naibu Maspika kutoka vyuo mbalimbali hapa nchini, karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi 17 wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* cha Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wananfunzi 54 kutoka Chuo cha *St. John University of Tanzania* cha Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanachama 16 wa Umoja wa Wafanyabiashara wa Samaki, Mkoa wa Dodoma (UWASAKI), karibuni. *(Makofi)*

Tunao pia Wakurugenzi watatu kutoka *MGA Insurance Limited* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Musa Julius Muyumba kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023

### Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023

### Muswada wa Shaeria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Nahodha, ajiandae Mheshimiwa Mpembenwe na Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nianze mchango wangu kwa kunukuu maneno ya Mzee Nelson Mandela, aliyoyasema mwaka 1964; "Katika maisha yangu yote, nimekuwa nikipigania jamii inayofuata misingi ya demokrasia, ambamo watu wote wanaishi kwa amani na kwa kufurahia fursa zilizo sawa, huu ni msimamo ambao nipo tayari kuupigania, kuishi nao, kufa na kupona."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na maneno haya ili kuonyesha kwamba kazi ya kujenga demokrasia siyo kazi rahisi, ni kazi ngumu inayohitaji viongozi makini, jasiri, wenye maono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge tunao wajibu mkubwa sana katika kutunga sheria zitakazotusaidia kuimarisha ujenzi wa demokrasia kwa kuweka mbele maslahi ya Taifa letu. Kwa maoni yangu kazi hii siyo ya siku moja, siyo ya mwaka mmoja, siyo ya miaka kumi na wala haitakuwa kazi ya karne moja, kazi hii itakuwa ni kazi endelevu. Wajibu wetu ni kutunga sheria makini, zilizo bora, sasa na vizazi vitakavyokuja baada yetu navyo vitaendeleza pale tutakapomalizia leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya tathmini ya chaguzi mbalimbali ndani na nje ya Bara la Afrika na nimebaini kuna malalamiko ya chaguzi ya aina tatu. Jambo la kwanza, muundo wa tume zenyewe za uchaguzi, mifumo ya kuhesabu kura na tatu uwakilishi na usawa wa masuala ya kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe maoni yangu katika hayo maeneo matatu niliyoyasema. Ninapoangalia tume zinazoitwa huru za uchaguzi, nimebaini kwamba uhuru wa tume hizo

hautokani na jina au watu wanaoziteua tume hizo bali unapaswa kuzingatia jambo muhimu, kwanza, sifa, weledi, uzoefu, uaminifu wa wajumbe wanaoteuliwa katika hizo tume ambazo zinaitwa huru, kwangu mimi huo ndiyo utakuwa uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi, Tume yetu ya Taifa ya Uchaguzi inapaswa kuwa na wajumbe wa aina tatu. Aina ya kwanza ni watu wenye ujuzi, uwezo, sifa, katika masuala ya kisiasa, sheria, utawala na masuala ya kaimataifa. Sifa ya pili ni ujuzi wa masuala ya uongozi katika sekta za umma na sekta binafsi pamoja na mashirika ya kimataifa. Sifa ya tatu ni wajumbe wawe wanaoheshimika, kukubalika, kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili. Napendekeza kwamba Tume yetu ya Taifa ili ifanye kazi zake kwa ufanisi inapaswa kuweka mifumo madhubuti ya namna ya kuhesabu kura na kuwa na wafanyakazi wenye uadilifu wa hali ya juu sana. Nakumbuka kuna nchi moja kubwa duniani ilifanya uchaguzi, baada ya kufanya uchaguzi kukawa na malalamiko ya kujumuisha na kuhesabu kura. Wakaanza kutumia mifumo ya teknolojia ikashindwa haikutoa majibu, wakahesabu kwa mkono haikutoa majibu, kwangu mimi hapa tatizo siyo mifumo, tatizo ni aina ya watu wanaofanya kazi hizo pamoja na uteuzi na ubora wa mifumo inayotumika, ndiyo maana napendekeza Tume inatakiwa kuwa na wafanyakazi wenye uadilifu wa hali ya juu sana, wenye weledi na ujuzi pamoja na kuweka mifumo ya kisasa iliyobora, iliyo makini na madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la tatu, mara nyingi tunapozungumzia uwakilishi na usawa wa kijinsia, tunasema wanawake wapewe asilimia 30, asilimia 40 katika masuala ya kiutawala na kiuchumi. Kwangu mimi unaposema asilimia 30 au asilimia 40 huu siyo usawa bali hii kwa kiswahili unaitwa ni mgawanyo wa uwiano, kama tuna maana ya usawa basi mgawanyo uwe asilimia 50 kwa asilimia 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema mgawanyo uwe asilimia 50 kwa asilimia 50, Katiba ya Jamhuri ya Muungano, katika Ibara ya 12 inasema watu wote wanawake na wanaume huzaliwa wakiwa watu sawa. Hoja ya pili, matokeo ya sensa yaliyotoka hivi karibuni yanaonesha asilimia 52 ambayo haipishani sana na asilimia 48 ni wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaalam mmoja wa masuala ya elimu Dkt. Aggrey wa Ghana aliwahi kusema, ukimsomesha mwanaume mmoja maana yake umemsaidia mtu mmoja, ukimsomesha mwanamke mmoja unaielimisha jamii kwa ujumla. Kwa maana hiyo tuna haja ya kuendelea kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii siyo ya Serikali peke yake, kazi hii ni ya Serikali, ni ya familia, lakini naviomba vyama vya wasomi wanawake nao waendeleze kazi hizi. Waandae programu maalum za kuwapatia wanawake mafunzo, elimu ndani na nje ya nchi ili kuimarisha uwezo wao, kwa sababu Serikali inapotoa fursa za uongozi, hazitolewi tu kwa misingi ya demokrasia, zinatolewa kwa misingi ya uwezo, weledi na ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, hata dini zetu kubwa Uislamu na Ukristo, zinatambua nafasi ya mwanamke katika maendeleo na ustawi wa jamii, ndiyo maana Mtume Mohammad *(SAW)* alimuoa Bi. Khadija ambaye alikuwa mfanyabiashara na utajiri wake ulitumika sana katika kueneza dini ya Kiislamu. Biblia na uislamu unatueleza kisa cha Nabii Suleiman na Malkia wa Sheba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfalme Suleiman alipata habari kwamba Malkia wa Sheba alikuwa akiongoza lakini anafuata misingi iliyotofauti na imani ya Mfalme Suleiman, akampelekea taarifa kwamba ajisalimishe, asipojisalimisha atapambana naye. Malkia alikutana na Barazalake la Ushauri ambalo lilikuwa na wanaume wengi tu, akasema Mfalme Suleiman anataka kutushambulia tufanyeje? Wanaume wakamwambia tukapambane naye.

Akasema hapana, wafalme wenye nguvu na hapa naomba mnisikilize vizuri. Wafalme wenye nguvu na majeshi yenye nguvu hawana huruma na wala hawana hekima, tukipambana naye atatumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kukisema hapa, unapokuwa na kiongozi mwanamke ni msikivu, mtulivu, ana hekima na busara. Kwa maana hiyo, kama Waheshimiwa Wajumbe tutumie nafasi hii kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza dhamira yake ya dhati ya kuimarisha umoja, usalama, amani na ujenzi wa demokrasia katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama alivyosema Nelson Mandela, sisi kama viongozi tuwe tayari kuipigania ndoto hii kufa na kupona ili kutekeleza dhamira yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. tunaendelea na Mheshimiwa Mpembenwe, jiandae Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Chumi.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuwa mchangiaji leo hii asubuhi, katika miswada ambayo imewasilishwa mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia naanza kwanza kwa kutoa shukrani za dhati kwa wafuatao: Naomba kwanza niwashukuru viongozi wote walioshiriki ambao ni viongozi wetu wa kidini, asasi za kiraia na *NGO's*, viongozi wa vyama vya siasa ambao walishiriki katika mchakato huu, wao wamekuwa na nafasi kubwa sana kuweza kuhakikisha kwamba tumefika hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ninamshukuru sana Dada yangu Waziri Jenista Mhagama, Naibu Waziri pamoja na timu yake yote kwa ujumla wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo

wameweza kuifanya na leo tunakwenda kujadili miswada hii, hakika historia itakwenda kuwakumbuka na kamwe hatutoweza kuwasahau kwa hiki kitendo cha kihistoria ambacho kinakwenda kutokea katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana aliyethubutu, mwanamama shupavu kabisa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maamuzi aliyoyachukua ya kuweza kuona kwamba kipaumbele cha hali ya juu kabisa ni kwanza kuwa na demokrasia na ndipo tunaweza tukawa na utulivu ndani ya nchi ili sasa tuweze kuona tunaweza kusonga mbele katika sekta nzima ya uchumi, maendeleo ya jamii na maeneo mengine yote. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri na ushupavu uliuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera hizi haziwezi kuishia hapa tu, siku hizi kuna misemo inasema kwamba apewe maua yake, kama ingekupendeza kwa Bunge lako hili tungeweza kuchukua mpaka azimio mama huyu tuweze kumuwekea mnara ambao kwa namna moja au nyingine historia itakwenda kumkumbuka. Ni kitendo cha kijasiri alichokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme yafuatayo; mchakato huu umefikia hapa haukutokea hewani tu, ilikuwa siku ya tarehe 22 Aprili, 2021, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu, alipokuja kuhutubia hapa Bunge lako Tukufu, miongoni mwa mambo aliyoyasema ni kwamba dhamira yake ni kuweza kuhakikisha kwamba anakwenda kukutana na vyama vyote vya siasa ili kuweza kuwa na muafaka ili tuweze kuona Tanzania tunasonga mbele na hatuna malumbano ambayo hayana tija yoyote. Hongera sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii nzuri uliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo hicho hakikuishia hapo, tulikwenda tukawa na mkutano wa kwanza ambao ulikuwa umefanyika, kwa namna moja au nyingine ulikuwa umehusisha

wadau wa vyama vya siasa na wadau wa maendeleo katika suala zima la mambo ya demokrasia. Mkutano ule ulikuwa umeweza kwenda kuweka jiwe la msingi ili sasa kuweza kwenda kuhakikisha kwa mara ya kwanza kuna Tume ya kikosi kazi ilikwenda kuzinduliwa ili kuweza kuona kikosi kazi kile kimekwenda kufanyakazi ya kuchukua mawazo ya Watanzania wote, katika *section* zote zilizokuwa zinawagusa na leo tumefika hapa tulipofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote mkutano wa pili ulikuwa umefanyika Septemba, 2023 na mkutano huu ndiyo ulikuwa umekwenda kutengeneza jiwe la msingi kwa sababu vyama vyote vya siasa vilishiriki na vizuri zaidi tulkazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua kwamba huna *right* ya kuzungumza kama huna ushahidi, hizi ni kanuni zetu za Bunge lakini nasimama kifua mbele katika Bunge lako Tukufu kusema kwamba, miongoni mwa watu walioshiriki katika Mkutano ule alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alishiriki na kuweza kuwakilisha chama chake ili sasa kuweza kuona kwa namna moja ama nyingine maazimio ambayo yanakwenda kuchukuliwa ni maazimio ya msingi ili tuweze kuwa na hizi sheria tunazokwenda kuzijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miswada ya sheria ambayo tunakwenda kujadili hapa ni mitatu; muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa mwaka 2023, Muswada wa pili tunaokwenda kuujadili ni *The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill,* ya mwaka 2023, lakini Muswada wa tatu ni Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote sisi ni mashahidi, tukumbuke tu, wakati shughuli hizi za michakato ya mikutano inaendelea; naomba nizungumze kifua mbele na sauti yenye kusikika, Tanzania na Watanzania walijue hili. Katika mkutano ule, tuna ushahidi wa kutosha kabisa; alisimama ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe na alimwomba Mheshimiwa Rais akisema kwamba, "Mheshimiwa Rais

pamoja na mambo mengine, leo tungependa sana katika mkutano kama huu tungekuwa na baadhi ya viongozi ambao wako gerezani." Mheshimiwa Rais alilichukua hilo kwa mapana yake, na alisema kwamba, hili nimelichukua, nakwenda kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie, muda siyo mrefu, viongozi wa upinzani pamoja na wengine waliweza kuachiwa. Katika mkutano ule ndipo tulipoweza kuona kwa mara ya kwanza Tanzania sasa inakuwa huru, mikutano inafanyika, na watu wanaendelea na watu wanaendelea na shughuli za mambo ya kisiasa. Sina budi kusema hili kwa sababu sikuwahi kuliona hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka, tunavyozungumza suala zima la mambo ya mikutano, hii ni haki ya msingi ya chama cha kisiasa, lakini kwa mara ya kwanza mmoja wa viongozi wa chama cha siasa ambaye anatoka Chama cha Maendeleo (CHADEMA), alisimama pale Mwanza na kusema, anamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo alikuwa anaendelea kuifanya kuhakikisha kwamba demokrasia inakwenda kufanyika.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu nimpe Taarifa mchangiaji ili aweze kuweka maelezo yake vizuri na kwenye *Hansard;* kinaitwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, siyo Chama cha Maendeleo na Demokrasia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpembenwe, taarifa hiyo.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea Taarifa kwa mikono miwili na kuthibitisha tu kwamba, nikidhani anakwenda kukana kwamba kauli hii haikuzungumzwa, kumbe kiongozi yule kweli alizungumza kauli hiyo. Alimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuruhusu mikutano iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza, historia imekwenda kutengenezwa ndani ya Tanzania. Katika mikutano ile, Polisi walikuwa wamekaa na kuwalinda viongozi wale. Sambamba na hilo, ili kuweza kuonesha ukomavu wa siasa ambao Mheshimiwa Rais anataka kuupandikiza ndani ya Tanzania, kuna maandamano ambayo yalikuwa yanafanyika, nami najua, historia inatuambia, kuna jirani zetu waliweza kufanya maandamano katika siku kadhaa zilizokuwa zimepita huko nyuma. Cha kusikitisha zaidi, katika maandamano yale badala ya wale watu wanaofanya maandamano kuwa wanalindwa, bahati mbaya zaidi Polisi walikuwa wanazuia maandamano na vitu vingine vilikuwa vinaendelea

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie, kwa hapa tulipofikia, tumeweza kuyaona maandamano juzi juzi hapa yamefanyika. Katika maandamano yale, wale waliokuwa wanaandamana, walikuwa wanalindwa na magari ya Polisi, vyombo vya ulinzi na usalama na walitimiza azma yao bila shida yoyote. Hii ndiyo demokrasia na hii ndiyo Tanzania ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwongezee Mheshimiwa Mpembenwe kuwa, pamoja na

kulindwa, lakini pia kulikuwa na *ambulance in case* lolote limetokea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha ni jinsi gani sasa Tanzania tunakwenda kubadilika. Anayekwenda kuibadili Tanzania siyo mwingine basi ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania nataka walijue hili; dunia inafahamu, Watanzania wanafahamu, Afrika nzima inajua na sisi Wabunge humu ni mashahidi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuibadilisha Tanzania katika taswira nzima ya mambo ya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba katika Muswada huu niongee kidogo tu katika suala zima la Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Sisi wote tunajua kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikuwepo, lakini kwa namna moja ama nyingine kulikuwa hakuna sheria mahususi iliyokuwa inaiongoza Tume hii ya Taifa ya Uchaguzi na vilevile na muundo wake. Nini kilichokuwa kimeanza kufanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikutano ambayo kwa namna moja ama nyingine, kiongozi huyu niliyekuwa nimetoka kumtaja muda siyo mrefu alishiriki, moja ya maazimio ambayo yalikuwa yamechukuliwa pale ni kwamba, ni wakati muafaka sasa umefika Serikali iweze kupeleka Miswada hii Bungeni, iweze kujadiliwa kwa mapana na marefu. Nami nataka niseme, hilo limefanyika katika Bunge lako la Mwezi wa Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naishukuru vilevile Kamati ya Katiba na Sheria na Wabunge wenzangu kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri waliyoweza kuifanya kwa kuchakata na kupokea yale yote yalikuwa yameletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo yote hayo, kabla sijaugusa huu Muswada moja kwa moja, nataka niongee jambo moja. Tumeshuhudia kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, viongozi wa vyama vya siasa wakiitwa Ikulu, wanapata *juice,* wanazungumza maendeleo ya Taifa hili na haya ndiyo tunayaita maridhiano. Haya yametokea, hayana ubishi na huyu ndio Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sielewi, lakini niseme tu Mheshimiwa Waziri wetu, kama itaridhia, basi ni vyema tu tukasema sasa tunakoelekea ni kwenye *Samialization of Tanzania*. Mama huyu anakwenda kuibadilisha Tanzania katika kuweza kuhakikisha kwamba, sekta nzima ya masuala ya demokrasia na mambo ya siasa yanakwenda kunyooka ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada huu naomba nizungumze nukta moja tu. Nukta hii inahusiana na suala zima la tume huru. Mama huyu anaupiga mwingi kweli kweli. Tunapozungumzia tume huru, ni huru kweli kweli kwa maana tume hii ni huru. Muswada huu vile vile umeeleza na ndiyo maana Wabunge humu ndani pamoja na wale marafiki zetu tunakwenda kuupitisha kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tume hii, namba moja, inakwenda kuwa na bajeti yenye kujitegemea na wote humu ndani tunakwenda kuipitisha bajeti hiyo. Pia katika kuhakikisha kwamba tume hii inakwenda kuwa huru kwa maana ya kwamba inakwenda kuwa huru, Mheshimiwa Rais ana haki ya Kikatiba ya kimsingi kabisa kuweza kufanya uteuzi, lakini angalia kilichotokea. Baada ya kukusanya mawazo ya wadau mbalimbali akiwemo yule Makamu Mwenyekiti wa kile chama rafiki, walisema kwamba sasa tunakwenda kuanzisha tume au tunakwenda kuanzisha Kamati ya usaili. Kamati hii itakwenda kupendekeza majina, yanakwenda kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais sasa anakwenda kupata

nafasi ya kuweza kuwateua watu wale. Hii ndio maana ya tume huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee mbele kidogo. Tunapozungumzia mantiki nzima ya mambo ya tume huru, hapa katika suala zima la mambo ya fedha siyo tu kwamba tume inachukua fedha kutoka kwa Mheshimiwa Mpembenwe, tume inachukua fedha kutoka kwa mtu fulani, hapana. Fedha zote zinakwenda kutika kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Mchemba, pale Hazina. Hii ndiyo maana ya tume huru. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, tume hii inakuwa iko *free from undue influence,* kwa wale Wandengereko, kwamba, itakuwa haishurutishwi kuweza kuchukua mambo ambayo hayastahiki kuchukuliwa. Nami naomba niseme tu. Hili kwa mara ya kwanza linakwenda kutokea ndani ya Tanzania.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwongezea Mheshimiwa Mpembenwe kuwa, *internationally* tunapozungumzia tume huru, *one of the factors is financing.* Katika Muswada huu imeoneshwa tume hiyo itapewa bajeti maalum kwa ajili ya kuendesha shughuli zake za kila siku. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo umuhimu wa kuwa na watu makini sana ndani ya Bunge. Hii

inakuonesha ni jinsi gani sasa tunavyozungumzia tume huru jinsi ilivyo. Hatutegemei kwa namna moja ama nyingine, fulani atoe fedha yake, aweze kwenda kuifadhili ile tume, kitu cha namna hiyo hakitaweza kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama huyu sio tu anahitaji maua yake, lakini cha msingi zaidi, ikikupendekeza, nami naomba niseme Watanzania walielewe hili, leo hii twendeni tukajenge mnara wa mama huyu ili historia iweze kwenda kumkumbuka kwa mageuzi makubwa ambayo anakwenda kuyafanya ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu, mimi nimesoma *political science*. Wanasema kwamba, usipokuwa na *stability* ndani ya *politics* maana yake ni kwamba huwezi ukawa na *stability* katika uchumi, huwezi ukawa na *stability* vilevile katika mambo ya kijamii. Nataka niwahakikishie Watanzania, tunakwenda kuwa na *stability* katika suala zima la mambo ya kisiasa. Kwa tafsiri hiyo ndiyo maana leo tunakwenda kumaliza miradi mikubwa mikubwa, leo tunaenda kuwa na uhuru zaidi kwa wananchi wote kwa namna moja ama nyingine kwa kuzingatia sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, Watanzania wote kwa ujumla wake tuweze kuelewa kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, huyu mama amekuja kuleta mageuzi. Sijui nini kitakachoweza kutokea, lakini nataka niseme tu, kama itapendeza mama huyu, kwanza tunaenda kumpa kura za kishindo mwaka 2025, halafu huko mbele atajua Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, naomba ieleweke, siyo tu kwa Watanzania wa kawaida, mpaka wanafunzi wetu kule shuleni walijue hilo kwamba katika Awamu ya Sita alitokea mwanamama; na hapa naomba niweke sawa sawa katika *record* kwenye *Hansard*. Ninaposema mwanamama, sio mama yangu mzazi pale nyumbani, ninazungumzia Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa, ninazungumzia Amiri Jeshi Mkuu, ninazungumzia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba, taarifa zisome hivyo, alitokea mama katika Awamu ya Sita aliyekwenda kufanya mabadiliko katika suala zima la sekta ya mambo ya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, jiandae Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia sheria tatu hizi muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama cha Mapinduzi ni chama kiongozi, ndiyo maana kilishiriki kuleta ukombozi katika nchi za Kusini mwa Afrika. Hata mwaka 1992 wakati vinaanza vyama vingi kupitia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa letu, asilimia 20 walisema wanataka vyama vingi, asilimia 80 walisema hatutaki. Mwalimu akasema wengi wape na wachache tuwasikilize. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge katika miswada hii, sisi tulio wengi tutasikilizwa, tutapewa nafasi wakati wa kupitisha huu Muswada, halafu wale wachache watasikilizwa kwa maana ya kuboresha huko mbele ya safari kama kuna ulazima huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno yangu ya utangulizi, niseme tu nampongeza Mheshimiwa Rais. Kwa kawaida miswada Bungeni hapa ina namna mbili ya kuingizwa; moja, anaweza akaleta Mbunge muswada binafsi akiwa na hoja, lakini mara nyingi miswada mingi inaletwa na Serikali. Katika wakati ambao mwaka 2024 tunaenda kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na mwakani Uchaguzi Mkuu wa Nchi, na Rais ndio kiongozi ambaye tunamtegemea ashike bendera ya Chama cha Mapinduzi, amethubutu kuleta miswada Bungeni ili ijadili namna ya kwenda kufanya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mama apewe heko yake. Ni ujasiri wa hali ya juu kwa kweli. Ni mara chache sana inatokea hiyo. Ingekuwa ni mtu mwingine angesema, hii weka pembeni, nishinde kwanza uchaguzi, nishinde Serikali za Mitaa, halafu tutajadili hilo baadaye; lakini amesema pamoja na chaguzi za mwaka huu na mwakani, yeye haogopi chochote, yupo tayari kwa lolote, twende tukajadili kuboresha sheria hizi ili mambo yaende sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliunda kikosi kazi hapa, sitaki kurudi ambako wenzangu wamezungumza, lakini kikosi kazi kilikuwa na mapendekezo 83. Katika hayo, mapendekezo 64 yalifanyiwa kazi, sawa na 91.57%. Huyu mama anastahili apewe heshima yake. Mapendekezo 12 yapo kwenye *process,* saba yanahitaji mjadala mpana wa nchi. Sasa kama ulikuwa unahitaji asilimia 100, umepewa asilimia 91, nani kama Mama Samia katika eneo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii pia imeweka heshima kwa sababu ya zile *4R* za Mheshimiwa Rais, filosofia yake kwamba anataka kujenga nchi pia, maridhiano, ustahimilivu, lakini pia na kuleta *reform*. Sasa katika mazingira hayo, katika sheria tatu kwa mfano Tume Huru ya Uchaguzi, hapa Mheshimiwa Rais amepunguza madaraka yake. Anasema, Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti majina yatapendekezwa miongoni mwa sifa zilizotajwa kwenye sheria, halafu atateua mtu mmoja katika hao; Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, angeweza kusema namteua fulani kuwa Mwenyekiti wa Tume na wala asingeweza kuhojiwa kwa sababu havunji Katiba. Hapo hapo Serikali imeridhia na Mheshimiwa Rais ameridhia kwamba katika mazingira hayo, wale wasimamizi wa uchaguzi wawe ni Watumishi wa Umma Waandamizi. Sasa katika eneo hili waliposema watumishi wa umma waandamizi, uchaguzi kwa mfano Uchaguzi Mkuu unafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano, hatuwezi kwenda kuajiri watu nchi nzima waende

kwenye kituo cha kipiga kura, halafu unawalipa mshahara kila mwezi. Watakuwa ni Watumishi wa Umma Waandamizi, wenye sifa, ambao wakifanya kazi hiyo ya Usimamizi wa Uchaguzi kama watateuliwa na tume, wanarudi kwenye majukumu yao. Kwa hiyo, ina maana wakati wa uchaguzi watapata posho tu. Kwa hiyo, hapa Serikali pia imekuwa makini kupunguza gharama za uendeshaji wa Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tunaliona hapa, hili nalo wameandamana kulipinga. Yaani hili hawalitaki tena. Sheria ya uchaguzi hapa, imependekezwa pia kwamba ukiwepo mtu mmoja kugombea, utapigiwa kura za 'Ndiyo' na 'Hapana' na ukipata kura za 'Hapana' nyingi, maana yake *automatically* huwezi kuwa kiongozi; ukipata kura za 'Ndiyo' nyingi, utapata nafasi hiyo. Hili nalo wameandamana, wanalipinga, hawalitaki tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tungetamani kwenye sheria hii, suala la kijinsia, limezungumzwa juzi na Mheshimiwa Kilango na wengine, mimi naunga mkono. Ukitaka kutoa *story* namna kilichofanyika kwenye chaguzi mbalimbali, kudhalilisha watu, kutunga maneno ya uongo, mara huyu ni kikojozi, huyu kafanya hivi, huyu kaachwa, huyu kaacha; mambo mengi ya kihuni; sasa sheria lazima iseme, ikithibitika kwamba kuna mtu amemdhalilisha mwenzake, awe ke au me ashughulikiwe. Adhabu muhimu ni kuondolewa kutokuwa mgombea wakati huo uchaguzi unaendelea. Siyo usubiri uchaguzi uishe ndiyo uende Mahakamani, aah aah, tunamalizana hapo hapo. Kwa sababu yeye ametunga uongo, amemdhalilisha mwenzake ili amzidi kete kwa kumpunguzia sifa, sasa na yeye ni kumwondoa asiwe mgombea ili ashike adabu zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tungetamani sana hata maneno ya uongo, kuna maneno yanatungwa wakati wa uchaguzi. Unatungiwa kitu ambacho hakipo. Maana yake na yenyewe hii pia ichambuliwe vizuri, iingizwe kwenye sheria. Kama unaenda kugombea, ni vizuri utaje sifa zako, kwa nini wewe uchaguliwe na

mwenzako asichaguliwe? Siyo kutunga maneno ya uongo au kumdhalilisha mwenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Sheria ya Vyama, hapa imezungumzwa kwa ujumla wake. Ni vizuri vyama, hata itikadi, kuna vyama vingine hapa vinaunga mkono ushoga. Sasa chama kinapata usajili wa nini? Kinakuwa na mgombea wa kitu gani? Kwa sababu, huyu akishinda uchaguzi, atakuja kueneza mambo ya ushoga. Kwa hiyo, na yenyewe kwenye itikadi ya vyama lazima iseme chama hicho kinafuata maadili ya Watanzania na hakiungi mkono ushoga na kama kuna maneno hayo, tunaondoa na chama hakiwezi kusimama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ni muhimu sana kwenye vyama vya siasa, wamezungumza wenzangu nitawasemea kidogo, tuliokuwanao kule CHADEMA tunajuana. Viti Maalum, utaratibu; kwanza, kwenye vyama lazima wataje utaratibu na pia kwenye Sheria ya Uchaguzi ni vizuri ieleze Viti Maalum wanapatikanaje? Vigezo. Ikishakuwa kwenye Sheria ya Uchaguzi, maana yake tume itazingatia umepeleka majina. Kuna majina mengine hapa, hapa wenzetu wamefukuzwa 19. Unajua kilichotokea ni nini? Kwamba hawa wote waliambiwa wakagombee majimbo, wakaweka nguvu, wakawekeza, wakatoka jasho na damu, halafu uchaguzi umeisha, wakakaa kwenye vikao vyao, wamependekeza majina, bwana mkubwa akaja na majina kwenye kwapa; shangazi, mjomba, mke mdogo, mke mkubwa, ndiyo ugomvi. Amewapunguza nguvu sana hawa dada zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa michango yao humu ndani siyo hii, unajua, lakini sasa kule hawatakiwi. Hapa unafanyaje? Utakwenda kimkandamkanda tu hivyo! Kwa hiyo na yenyewe hii ni madhara ya kutokuwa na sheria ambayo inaeleweka kwamba, uchaguzi unaisha Viti Maalum unaamua, huyu mke wangu, shangazi awekwe. Sasa sheria pia itamke, vigezo ni nini? Mkurugenzi wa Tume apitie kuthibitisha majina hayo kama kweli huyu alishinda uchaguzi,

kama kweli kateuliwa kihalali ili wapate *comfort* ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ana nia njema sana na *4R* zake. Kwa mfano maeneo mawili, sina shida na ile *reform* na *rebuild*, nina shida kwa wenzetu walioandamana kwenye eneo la maridhiano na ustahimilivu. Sasa ndiyo nataka niwaambie Watanzania na wanisikilize kwamba, kama wewe umeshindwa kuridhiana ndani ya chama chako, wenzako ambao akina Mheshimiwa Halima Mdee wamechukuliwa vyuo vikuu, wale akina Zitto Kabwe, wale akina Mheshimiwa Kitila Mkumbo, wale akina Edward Lowassa, wale akina Sumaye, wale akina Dkt. Slaa, akina Kabourou, Marehemu Chacha Wangwe, wote hao jamaa alikuwa anawafukuza, walishindwa kuridhiana. Hawana maridhiano, sasa wewe unatarajia miujiza gani hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana unawaita Ikulu, unawapa chai, unawapa ruzuku, unawapa mikutano, wanachomlipa Mheshimiwa Rais ni kwenda kuandamana. Hawa wamempata Mama wa Taifa mpole, wangempata mtu mwingine ingekula kwao, yaani unaambiwa kwamba haya sasa mgombea atapigiwa kura ya 'Ndiyo' na 'Hapana' ambayo haikuwepo, unaandamana. Unaambiwa kwamba ruzuku unapewa, unaandamana. Unaambiwa una mambo 64 asilimia 91 yamekubalika, unaandamana. Unataka kupewa nini? Si bora nusu mkate kuliko kukosa mkate mzima! Si afadhali hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Rais kwamba, hawa walishashindikana tangu huko. Hata wewe ukizungumza, yeye afanye kwa nia njema ya Watanzania, lakini siyo hawa. Huyu ambaye anakaa naye kwenye meza, anamng'ong'a, hamheshimu. Unawezaje kwenda kufanya Mkutano wa Hadhara, unamsema mtu ambaye alikuja kukuona ukiwa kitandani? Kwamba, mimi nilikuwa na hali mbaya, nimekosa matibabu, nilikuwa ni mkimbizi, sina ruzuku, chama kimesambaratika, umepewa vyote.

Umepewa mkate kwenye sahani ya dhahabu, halafu unanitukana! Mheshimiwa Rais amevumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaambie Watanzania kwamba sisi viongozi wa Chama cha Mapinduzi, hiki ndio chama kiongozi. Kwa heshima ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia, kwa kazi nzuri aliyofanya, Watanzania wamsikilize Mheshimiwa Rais. Watanzania waisikilize Serikali, Watanzania wakiunge mkono Chama cha Mapinduzi. Hawa wengine watasubiri sana, kwa sababu, mpango kazi hawana, hawana itikadi, hatujui kama wanaenda mbele au wanaenda nyuma, wamekaa chini, wamelala kifudifudi, hawaeleweki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hatuwezi kuhangaika na watu ambao hawaeleweki. Tuangaike na mtu ambaye ana dira, kwamba unanisema, nakuja hapa tunazungumza pamoja. Halafu nawashauri pia Waheshimiwa Wabunge, sisi tulio wengi tutapitisha Miswada hii kwa nguvu zote iende ikatekelezwe. Sasa, kama kutakuwa na maboresho wakati wa utekelezaji, hiyo ni ajenda nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nia njema ya Mheshimiwa Rais ya kukaa na Watanzania, kuwasikiliza viongozi wa dini, kukaa na machinga, hatujawahi kupata Rais wa heshima kama Mama Dkt. Samia. Mama apewe maua yake na aungwe mkono. Uchaguzi wa mwaka huu ni kuunga mkono Mama Dkt. Samia na chama chake. Uchaguzi huu ni wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo wakitaka mambo mazuri, Mama Dkt. Samia amefungua milango wapeleke maoni kwake atapokea, Wabunge tutapitisha lakini kupiga makasia kwa mtindo ule ni kupoteza muda. Tunaomba twende mbele Waheshimiwa Wabunge, kifua mbele, Watanzania wanamheshimu Mheshimiwa Rais kwa kazi anayofanya. Tukienda na sheria hizi tukawaambia Watanzania kwamba, sasa Wakurugenzi hawasimamii

ni Watumishi wa Umma Waandamizi, hawa wanaandamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Spika amewakomoa. Walifukuza wale Wabunge, wakakusanya hela ili wapewe Viti Maalumu, Mheshimiwa Spika na Serikali amewakomoa, kesi haijaisha wanakula mkate humu ndani. Wapigie makofi *COVID-19* wako sawa. Vilevile, Mheshimiwa Rais kawakomoa, Wametaka kuandamana wakafikiri watapewa virungu, maji ya washawasha, mabomu hawajapewa. Wamelindwa na *ambulance* ipo, wakichoka tunawabeba ingawa wengine walitumia magari. Mama Dkt. Samia kawakomoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi iendelee, miswada ipitishwe. Uchaguzi utakuwa salama na amani. Chama hiki kiendelee kuwa chama kiongozi. Wale wote ambao walikwazwa ndani ya kile chama, waje hapa ndiyo sehemu salama. Hapa Chama cha Mapinduzi ni sehemu salama. Unazungumza kwa uhuru. Unaona leo sasa; nawaambia walioko nje wamechelewa kuja. Unamuona Mheshimiwa Kitila Mkumbo? Sasa hivi ni Waziri. Mheshimiwa Silinde sasa hivi ni Waziri. Mheshimiwa Moleli sasa hivi ni Waziri. Mheshimiwa James Millya, Mbunge wa *East Africa*. Hawa 19 nao tunao. Mheshimiwa Waitara nakula upepo, niko humu Bungeni kupitia Tarime Vijijini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mnataka nini? Mnataka nini? Siyo unakaa kwenye chama ambacho ukimhoji mtu anakufukuza. Mwaka huu wanao uchaguzi. Ameanza kutengeneza mizengwe. Sisi CCM mko salama, Mumshukuru Mungu. Mtuonee huruma tulikokuwa kule, tumechelewa sana. Tumekuja hapa tumechelewa sana na wengine mje. Mimi nawashauri Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na ninyi ni kinamama. Kwa heshima ya Mama Dkt. Samia na miswada mizuri hii na heshima aliyowapa wanawake nchini na huko duniani, si mje tu CCM hapo kazi iishe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana Mungu akubariki sana. Naomba niishie hapo kwa maoni yangu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, ajiandaye Mheshimiwa Festo Sanga, ajiandae Mheshimiwa Katimba. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kutumia nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na baraka na ulinzi wake, sote tumeuona mwaka mpya, ni kwa neema zake tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa nimesimama hapa na nimesema, Mheshimiwa Rais amethibitisha kwa vitendo kwamba ni mwanadiplomasia namba moja. Sasa, ameendelea tena kuthibisha kwa vitendo kwamba ni mwanademokrasia namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuishi kwetu sisi wengine tunapomwomba Mungu, huwa tunamwomba Mungu atujalie mema katika kuwaza, kunena na kutenda. Kwa sababu, unaweza ukawaza ukaishia tu kuwaza na usinene au unaweza kuwaza nakunena, usitende. Katika hili binafsi naona Mheshimiwa Rais wetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, amethibitisha kwamba analiwazia Taifa letu mambo mema lakini pia analinenea mambo mema. Pia, kwa vitendo amethibitisha kwamba ni mtu wa vitendo kwa kutenda yale ambayo ni kwa ajili ya mema ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wengi wameshaeleza mambo mengi lakini moja duniani na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo atakuwa shahidi wangu kama Waziri anayehusika katika mambo ya mipango na uwekezaji. Duniani kote hata wawekezaji, jambo moja na kubwa ambalo wanaliangalia ili waweze kwenda kuwekeza katika sehemu yoyote, kwanza ni *political stability*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, haya ambayo Mheshimiwa Rais Mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya kwa kuwaza, kunena, na kutenda, yanaendelea kuimarisha *political stability* yetu na kwa sababu hiyo, yanamrahisishia kazi Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Watanzania wote kwa ujumla, wakiwepo wa kule Mafinga na Mufindi ili tuendelee kupata wawekezaji wengi katika mazao ya misitu na sekta zingine kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni jambo la kupongeza lakini pia ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu na tatu la kuendelea kumwombea Rais wetu na Taifa letu ili liendelee kusonga mbele. Pamoja na kuwaza na kunena, Mheshimiwa Rais aliendelea sasa kwa kutenda kwa vitendo kwa kufanya nini; kwanza, kwa kuunda Kikosi Kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie; nimesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Sayansi ya Siasa. Wakati huo Profesa Rwekaza Mukandala alikuwa ni Mkuu wa Idara na baadaye akawa *Dean* wa *Faculty.* Huyu ni nguli katika sanyansi ya siasa lakini ni nguli pia katika masuala ya siasa na demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yeye ndiye alikuwa *founder* na kiongozi wa waendeshaji wa Taasisi ya *REDET*, iliyokuwa inahusika na masuala ya utafiti na masula ya kidemokrasia. Pengine wakati fulani Serikali ilikuwa inamuona kama mtu ambaye yuko *vibrant* sana. Mtu huyu huyu ambao Serikali nyingi duniani huwa kwa namna fulani zinawaogopa na kuwakwepa wale ambao tunasema ni *thinkers*, ni Wanazuoni wale ambao ni *critical thinkers* lakini huyu ndiye Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua kuongoza Kikosi Kazi ili kiwe na mawazo na kiwe na uhuru wa mawazo na fikra. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napongeza kwa sababu Mheshimiwa Rais ameendelea kufanya kwa vitendo. Kwa kweli, kitendo hiki hakikuishia tu katika Kikosi Kazi. Mawazo na maoni kama

walivyosema Waheshimiwa wengine hapa, yamefanyiwa kazi. Lingine ambalo ni vitendo na ni kubwa sana na pengine wengine hawalioni, ni lile la kutenga kifungu maalumu kwa ajili ya kuwezesha Baraza la Vyama vya Siasa Nchini kuendesha shughuli zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuwezesha mikutano mitatu ya masuala ya siasa na demokrasia. Hapa napenda nipongeze kwa sababu katika siasa kuna *passive politics* na *active politics* lakini pia ushiriki wa siasa kuna *active political participation* na *passive political participation*. Mheshimiwa Rais kwa vitendo akataka pawepo na *active political participation* na ndiyo maana Baraza hili limetengeza bajeti yake. Kama vile haitoshi, ndiyo maana mikutano mitatu ya siasa na wadau wa demokrasia imefanyika na imewezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napenda kuupongeza ushiriki wa viongozi wa dini na ushiriki wa wadau mbalimbali. Ushiriki wao haujawa tu katika kutoa maoni labda kwenye Kikosi Kazi, kutoa maoni kwenye ile mikutano lakini pia, hata wakati wa Kamati wamekuja kutoa maoni. Kuonyesha nia njema ya Mheshimiwa Rais, akasema sasa tunakwenda kuyawekea haya maoni msingi wa sheria na tumeletewa miswada. Miswada hii kwa nia njema unaona kabisa, wala haikuja kwa haraka haraka, wala haikuletwa kwa Hati ya Dharura, pamekuwepo na wigo mpana wa watu kushiriki na kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inaendelea kuthibitisha kwa vitendo nia njema aliyonayo Mheshimiwa Rais ambayo mwisho wa siku inaendelea kuimarisha ile niliyoita *political stability*. Katika kuifanya kazi hii, Kamati ya Mheshimiwa Dkt. Mhagama imefanya kazi nzuri sana. Miongoni mwa watu ambao wamekuja kutoa maoni, ni pamoja na viongozi wa dini kupitia jumuiya zao, wakiwepo *TEC*, wakiwepo *CCT* na Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Asasi za Kiraia 31 zimewasilisha maoni yao kuonesha wigo mpana wa ile niliyoita *active political participation*. Kama haitoshi, asasi zingine 400 zimetoa maoni kwa maandishi. Watu binafsi, wadau binafsi 1,700, nao walipata fursa ya kushiriki katika mikutano na kupokea maoni kutoka maeneo mbalimbali. Unaona vile ambavyo ile *active political participation* kutokana na nia njema ya Mheshimiwa Rais wetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, inathibitika kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile haitoshi, tumeona katika Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi, watu wengine wanasema neno hili ni huru ni huru, ni neno tu, hapana. Hata kwa vitendo tumeona; kwanza katika mundo lakini pili katika kuigharamia ile Tume. Nilikuwa naongea na Mbunge mwenzangu kutoka katika nchi jirani za Afrika Mashariki ambaye tulikuwa naye kwenye michezo kule Kigali, akawa ananiambia, nyie mabwana mnathubutuje kufanya mambo haya? Mnathubutuje kuruhusu kiongozi wenu ajipunguzie sehemu ya mamlaka na Madaraka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia, hiyo yote ni nia njema kwa vitendo katika kuimairsha demokrasia, katika kuleta *political stability* katika nchi yetu. Ninakuomba na wewe mwenzangu huko uliko, njooni Tanzania mjifunze jinsi huyu Mama anavyoendesha nchi katika namna ambayo ni ya uwazi, shirikishi na demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, katika Tume Huru ya Uchaguzi, unaona kwanza muundo wake na wenyewe wamejipunguzia madaraka na mamlaka. Kutakuwa na Kamati ya Usaili ambayo baadaye itawasilisha kwake majina hata kuzidi idadi ile ya wale wanaotakiwa kuteuliwa, kwa maana ya 5 + 4. Kama vile haitoshi, Tume ya Uchaguzi itakuwa na fedha moja kwa moja kutoka fungu kuu. Hata sisi hapa kama ulivyo utaratibu, wala hatutashiriki kuiingilia Tume ya Uchaguzi katika kuipangia bajeti, ukiacha tu ile bajeti ya kawaida ya *operational costs* za kawaida za *day to day activities*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii yote inaendelea kuthibitisha vile ambavyo Tume hii kweli itakuwa ni Tume Huru ya Uchaguzi. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, haya yote Mheshimiwa Rais akisaidiana na wasaidizi wake na hapa lazima nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mama Jenista Mhagama. Kwa kweli, yeye na masaidizi wake na Naibu Waziri wake wamefanya kazi nzuri. Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla, kuona Muswada umefika katika hatua hii, wako watu wamekesha. Wako watu hawakulala; pengine wako watu wamefunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawapongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa kazi nzuri. Pia, kuwa *open minded*, hata katika Kamati mmepokea maoni, mmepokea ushauri wa Kamati na mmewa-*accommodate* katika *amendment* ambazo ziko kaika Muswada huu. Kwa hiyo, nawapongeza na Mwenyezi Mungu awabariki, awalinde, aendelee kuwaangazia nuru yake. Pia, natumia nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati, wamefanya kazi nzuri na wao wakina Mheshimiwa Dkt. Mhagama kwa kweli wamekesha muda wote. Wakati mwingine wamechelewa kwenda kula, wakati mwingine wamefanya kazi mpaka usiku. Ni jambo la kupongeza *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwangu mimi, kipekee naomba niwapongeze viongozi wa dini. Ukiacha ushiriki wapo lakini pia wameendelea kuiombea nchi yetu, wameendelea kuliombea Taifa letu. Ninaendelea kuwasihi, sote kama Watanzania tuendelea kuliombea Taifa letu, tuiombee nchi yetu. Zaidi ya yote, tumwombee Mama yetu mwenye maono mema, kwa nia njema ya Taifa letu, kwa nia ya kujenga demokrasia imara, kwa nia ya kuleta ile niliyosema *political participation* ambayo ni *active;* lakini juu ya yote *political stability* ambayo mwisho wa siku kutokana na *political stability* tutapata wawekezaji, tutakuza uchumi wetu Wananchi wa Mafinga, Wananchi wa Mufindi, Wananchi wa Iringa na Tanzania kwa ujumla tutapata neema na mema mengi, kutoka katika maono mazuri ya Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawasilisha. Mungu atubariki sisi sote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Sanga, ajiandae Mheshimiwa Katimba, ajiandae Mheshimiwa Raymond.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hii Miswada mitatu tuliyonayo mbele yetu. Jambo la kwanza, napenda kuwashukuru watu wafuatao: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuruhusu haya yanayoendelea leo kwenye Taifa letu, yaendele na yatokee katika Bunge letu. Kwa sababu kilio hiki ni miaka mingi Watanzania walikuwa nacho lakini sasa tumeanza kukifanyia kazi, tuna hatua moja kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama na Naibu wake lakini na Watendaji wote wa Serikali kupitia Wizara hii, kwa huu mchakato wote hadi hapa leo tunaelekea mwisho, mwisho sana, kuhakikisha tunafanikisha ndoto za Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati, nawashukuru Watanzania mmoja mmoja. Pia, nishukuru taasisi za Serikali na taasisi binafsi ambazo zimetoa mawazo kwa ajili ya hiki kinachoendelea leo kupitia hii Miswada mitatu, kwa ustawi bora wa Taifa letu. Watanzania wanaotusikiliza huko nje na walioko hapa ndani, wafahamu jambo moja. Bunge hadi tunafikia hatua ya kujadili haya mambo, hatujayatoa hewani. Ni mambo ambayo yamewakilishwa na vyama tofauti vya siasa, dini tofauti na Watanzania tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunachokifanya ni kusimamia mawazo ya Watanzania, taasisi na mambo mengine na wale wote ambao wamejitokeza kwenye kutoa maoni haya na

Kikosi Kazi alichokinda Mheshimiwa Rais ambacho kimefanya kazi kubwa na maoni zaidi ya 90% yanafanyiwa kazi na Mheshimiwa Rais na ndiyo yako mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya kujadili kwenye jambo hili. Watanzania wahafamu jambo moja, Mheshimiwa Rais ana zile *4R* ambazo tunaenda nzao kama Taifa, hususan maridhiano na ustahimilivu na kujenga upya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge na Watanzania tumepitia katika majira mengi sana kwenye siasa zetu ambapo yamekuwa na malalamiko ya kushoto kulia kushoto kulia, hasa hasa kuhusu chaguzi zetu na Tume yetu. Majibu yote ya yale ambayo yalikuwa ni kero kwa Watanzania, leo yako mbele yetu na ndiyo haya tunayoenda kuyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanaotusikiliza, taasisi zilizojitokeza mbele ya Kamati na Kikosi Kazi zilikuwa na maoni tofauti tofauti. Kwa mfano, kulikuwa na watu kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kupitia BAVICHA na wao wenyewe CHADEMA walikuwa na maoni ya kwamba Wakurugenzi wasisimamie uchaguzi kwa sababu walikuwa na mashaka na Wakurugenzi. Mheshimiwa Rais amelipokea wazo hilo, amelileta mbele yetu kwa mtindo wa kwamba sawa, Wakurugenzi hawatasimamia uchaguzi. Sasa tutaenda kutumia Maafisa wa Serikali waandamizi ambao wako *vetted* kwa ajili ya kusimamia uchaguzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonisikitisha ni kwamba, licha ya hayo ambayo yametolewa, bado kuna Watanzania wanapinga. Kwamba wana wasi wasi na hicho kinachoenda kusimamia uchaguzi ambacho tunaita ni Maafisa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja; hawa wanaoenda kusimamia uchaguzi ni Watanzania na uchaguzi wetu

sisi hauwezi kusimamiwa na mtu wa nje. Sisi wenyewe Watanzania ni Taifa huru ambalo tunaweza kujisimamia na hawa Watendaji na Waandamizi wa Serikali ni watu ambao wako *vetted*. Lazima tuendelee kuwaamini kwa ajili ya kusimamia chaguzi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maoni yalitolewa na TAMWA, waliomba Serikali iondoe tozo kwenye suala la mtu akipoteza kitambulisho cha kupigia kura, sasa kiwe bure. Mheshimiwa Rais kwenye mapendekezo ametoa, sasa hicho kitakuwa bure. Ukienda kwa *CCT*, walitoa Mawazo,Sheria haijajumuisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu sasa ijumuishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda haya yote yamefanyiwa kazi, Sura Na. 343, Sheria ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge na Sheria Na. 292, Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani, sasa zimeunganishwa zitakuwa ni kitu kimoja. Kitu ambacho kilikuwa ni kilio kikubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hawa *TGNP* walizungumzia suala la usawa wa kijinsia wa kwenye uchaguzi. Limekuja pendekezo kwamba, tunaruhusu usawa wa kijinsia kwenye uchaguzi. Huu ni muda muafaka kwenye Taifa letu kuwa na haki sawa Watanzania kwa wote kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa haya yote ni kwa sababu, hakuna mwanamama aliyewahi kupewa nafasi kwenye Taifa letu akatuangusha, akiongozwa na Rais wetu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye Taifa limepitia katika majira magumu kwa wakati fulani lakini yeye amekuja kuliponya Taifa, kama ambavyo viongozi wa dini wamekuwa wakisema na sasa kila mmoja anapata haki ikiwemo hawa ndugu zetu wa vyama vya upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nizungumze wazi kwamba, Serikali imefanya kazi kubwa na ni lazima twende kuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili suala la kukomesha unyanyasaji wa kijinsia kwenye suala la chaguzi. Hili niseme wazi kabisa na Watanzania wanaotusikiliza. Hili ni moja kati ya jambo ambalo limeisumbua sana Serikali na limewasumbuwa sana Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu kutumia majina ya ovyo, watu kupakaziana kesi ili mradi mtu ashinde uchaguzi. Bahati nzuri nimeshiriki chaguzi kadha wa kadha, kuna wakati tulipokuwa na uchaguzi Jimbo la Arumeru Mashariki, wana CCM wanakumbuka tulivyokuwa na mgombea wetu Sioyi na jinsi ambavyo lugha zilikuwa zinatoka dhidi yake kwenye chaguzi zile. Haya yote yalisababisha changamoto na muda mwingine mgombea wetu kukosa sifa au kukosa kura au kukosa haki yake ya kikatiba mbele ya Watanzania kutokana na lugha ambazo walikuwa wanazizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili kuna akina mama ambao wamekuwa wakiteuliwa kwenye nafasi tofauti tofauti. Wengine wanaita kwa majina ya …

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nilikuwa nataka nimpe taarifa mchangiaji anachangia vizuri. Ni kweli wakati wa chaguzi udhalilishaji siyo tu wa yale matusi yanayotolewa. Nadhani katika kurekebisha hii sheria kama kutakuwa kuna mgombea mwanamke basi polisi wanaokuja kulinda kwenye ile mikutano wawe wanawake. Sisi ambao tumegombea wanawake tumeshuhudia udhalilishaji wa polisi wakiume wanamdhalilisha mwanamke mpaka hata wengine wanakutia vidole.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bora wawepo wanawake wasimamie wanawake, hicho kipengele kiwepo maana yake siyo matusi tu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea kwa sababu anayezungumza amepitia kadhia hiyo alivyokuwa anagombea uchaguzi wa mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kudhalilisha kwa kutamka majukwaani kuna haja ya kitu kimoja kinaitwa *fast track case*. Ambacho tungeshauri kama kuna Mahakama za chapu chapu kwenye kutatua matatizo mbalimbali. Mathalani wenzetu Kenya wana Mahakama ya papo kwa papo kwenye makosa ya barabarani. Ukienda hata Jiji letu la Dar es Salaam kuna kesi ambazo zinahukumiwa papo kwa papo kwa watu ambao wanafanya makosa katikati ya jiji. Kuna kila sababu kwa watu ambao wamefanya kosa la kumdhalilisha mgombea ili yeye apate *advantage* ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo na uwezekano wa kufanyia *fast track* ya kimaamuzi ili huyu mtu aweze kuchukuliwa hatua. Kwa sababu kutokufanya hivyo kusubiri mwaka mzima kunakuwa kumemkosesha haki Mtanzania au huyu mwingine ambaye anagombea. Kwa hiyo kuna haja yakufanya maamuzi ya haraka ili Watanzania waweze kupata haki na mtu ashindane kwa hoja na wala si kushindana kwa kuchafuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo niongeze tena. Ningetamani sana tunakoelekea kuna kitu kinaitwa *artificial intelligence*. Katika *artificial intelligence* una uwezekano wa kumtumia mtu sura yake, sauti yake na kila kitu na ukamdhalilisha kwamba yeye anachokifanya hicho kitu au anakizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunayazungumza haya twende mbali zaidi kuwaangalia wenzetu wa *TCRA*, lakini pia na sheria iweze kutambuwa watu ambao wanatumia *social networks* na mitandao mingine waingie kwenye haya makosa ya kisheria kwenye kuzalilisha Watanzania; lazima Taifa lijiandae jinsi ya kupambana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo mimi kama Mtanzania ambaye nimekuwa kelele na kilio cha Watanzania waliyo wengi, walikuwa wanazungumzia suala la Tume Huru ya Uchaguzi. Ukisoma kwenye Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanasema hivi; 74.-(1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao watakaoteuliwa na Rais: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Katiba ni ya mwaka 1977 tangu imetungwa. Ndiyo kwa mara ya kwanza Rais wa Taifa letu katika Marais watano waliopita huyu wa sita anaamuwa kuachia siyo tu kuachia tu, uteuzi wa wajumbe wanaenda, ukisoma kwenye sura ya tisa kifungu cha tisa, ambacho tunaenda kwenye marekebisho wanasema hivi; wakati wowote itakapobidi kuteuliwa mjumbe au wajumbe wa tume, kamati ya usahili itaitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeondoa Madaraka yote ya Mheshimiwa Rais kwenye hili jambo. Ni Rais gani anayeweza kukubali kirahisi jambo kama hili? Ni Mheshimiwa Dkt. Samia pekee ambaye amekubaliana na jambo hilo. Kwamba mlitaka Tume Huru na nimewapa Tume Huru. Kama kuna Mtanzania ana *qualification* za kuomba kuwa mjumbe kwenye tume hii anapewa nafasi ukienda pale namba tano; kupitia vyombo vya habari litatoka tangazo, mtanzania ana-*apply* anaenda kwenye tume anachaguliwa anakuwa mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Rais anaweza kufanya hivyo *especially* kwenye nchi za Kiafrika lakini Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya haya mambo ya kuruhusu haya mambo. Kwa hiyo

niseme wazi na nizungumze kitu kimoja, suala la Tume huru ya uchaguzi. Hapa kuna vitu viwili, kuna *concept* mbili. Watanzania wanaotusikiliza lazima wafahamu. Suala la Tume ya Uchaguzi ni jambo lingine na suala la mtu kushinda kwenye uchaguzi ni kitu kingine. Tumepita kwenye majira ya uchaguzi mwaka 2010, 2015. Mwaka 2015 upande huu ambao mimi nimekaa walikuwa wamejaa chama cha upinzani zaidi ya Wabunge 116 kupitia Katiba na Tume hii hii ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la chama kushinda au mtu kushinda ni kukubalika mbele ya uso wa Watanzania na siyo kwa sababu ya hili jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze wazi kabisa, *opposition* walishinda ndani ya Bunge kwa sababu walikuwa na sera mbadala zinazosikilizika kwenye masikio ya Watanzania na ndiyo maana wakaungwa mkono, kwa sababu mgombea aliyekuwa amesimamishwa amelelewa na CCM ambaye alikuwa ni Edward Lowassa. Alikuwa na uwezo wa kuzungumza vitu ambavyo watanzania wanatamani kuviona, wakapata wabunge 116. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wafahamu baada ya haya yote kutokea, tutabadilisha hizi sheria, tutabadilisha Katiba kama hatujabadilisha *brain mindset*, akili ya Watanzania kwamba kushinda kunatokana na vile ambavyo Serikali ina-*deliver* basi tutakuwa tunafanya tu vurugu. Kwa sababu gani; kuna Taifa hapo pembeni Jirani limebadilisha Katiba; na wakati wa uchaguzi wamegawanyika hata tume

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Zimbambwe, *ZANU PF* ilidondoka si kwa sababu ilikuwa ina tume mpya nzuri sana, ilikuwa na tume ile ile mbovu na chama kikadondoka kwa sababu ya kushindwa ku-*deriver*.

Mheshimiwa Naibu Spika, CCM kupitia Mama Samia Suluhu Hassan, jinsi ambavyo inatoa miradi kwa Watanzania, jinsi ambavyo inahudumia sekta binafsi, jinsi ambavyo inahudumia vyama vya upinzani, jinsi ambavyo inahudumia Watanzania wote na taasisi za dini; niwaambie, ibadilishwe Katiba ama isibadilishwe, kwa sababu mtu anakubalika; *legitimacy* ya mtu mbele ya Watanzania ndiyo itakayomchagua. Niseme wazi kabisa kama Mwenezi anafanya kazi ile ile ya CCM…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ya pili hiyo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anafanya kazi kubwa ndani nje kusikiliza kero za Watanzania chama hichi kitaendelea kukubalika na kushinda kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kabisa kwamba Rais, ameonyesha njia lazima tumfuate. Tuwaombe wenzetu waliyopo nje wanaotaka kuandamana, wanaosisitiza maandamano wamekosa hoja, wamekosa ajenda; lazima wamsikilize Samia na wamfuate Mheshimiwa Rais wetu tuweze kusonga mbele kwa sababu ni mwana mama ambaye alionyesha mfano kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme wazi kabisa kwamba ninaunga mkono hoja, ninamuunga mkono Mheshimiwa Rais lakini kwa sababu chama cha upinzani. Kwa sababu chama cha upinzani kina tabia ya kutokukubali…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, muda wako umekwisha.

**MHE. FESTO R. SANGA:** …, kinaendesha harakati zaidi mambo yake kuliko siasa watashindwa tu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katimba. Jiandae Mheshimiwa Raymond, jiandae Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia miswada mitatu iliyopo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuruhusu maboresho ya sheria hizi muhimu sana katika uchaguzi. Ruhusa yake hii ya kufanya maboresho haya ya sheria tafsiri yake ni utekelezaji kwa vitendo wa falisafa ya *4R,* na hasa katika ile *R* ya tatu ambayo ni *reform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Sera, Bunge na Uratibu pamoja na timu yake nzima kwa kufanya kazi hii kubwa na kusimamia huu mchakato wa marekebisho wa sheria hizi. Nisiache kuipongeza pia Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria kwa kazi kubwa yakuchakata Miswada hii, kuichanbua Miswada hii na kutuletea taarifa nzuri katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabinti wa Kitanzania wanatamani kuwa kama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; mabinti wa Kitanzania wanatamani kufika pale alipofika Dkt. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Balozi; mabinti wengi wa Kitanzania wana ndoto zakuwa kama Dkt. Tulia Ackson; mabinti wa Kitanzania wanatamani kuwa kama Mama Mary Chatanda, Mama Zainabu Shomari, viongozi wetu wa UWT Taifa; na mabinti wa Kitanzania wanandoto kubwa ya kuwa viongozi wakubwa kisiasa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mabinti hawa wa Kitanzania waweze kufikia ndoto zao wanakutana na vikwazo vingi. Kwanza, wanakutana na kikwazo cha tamaduni, mila na desturi kandamizi kwa mwanamke, wanakutana na kikwazo cha ufinyu wa rasilimali za kuweza kuendesha michakato ya kisiasa, vile vile wanakutana na

kikwazo cha ukatili wa kijinsia uliyokithiri katika michakato ya kisiasa. Mabinti hawa kwa vikwazo hivi inafika wakati wanashindwa kufikia ndoto zao na wanakata tamaa. Kwa hiyo sisi kama wabunge na sisi kama viongozi tuna wajibu wakuwasaida mabinti hawa waweze kufikia ndoto zao za kisiasa kwa kutunga sheria zitakazoweka misingi ya usawa wa kijinsia katika michakato ya kisiasa lakini itakayo ondowa chembe chembe za ukatili wa kijinsia katika michako ya kisiasa na uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokuwa anahutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, New York, tarehe 23 Septemba, 2021. Alisema na naomba nimnukuu: *As the first female president in the history of my country, the burden of expectations to deliver on gender equality is heavier on my shoulders. Aware that, being passionate about gender equality is not sufficient, my government is reviewing policy and legal frameworks in order to come up with actionable and measurable plans to ensure economic empowerment of women but also other aspects pertaining to gender equality and gender parity. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, amesema: *my government is reviewing policy and legal frameworks to ensure gender equality and gender parity.* Kwa hiyo kwenye *reviewing legal frameworks* ndipo tulipo wakati huu. *We are reviewing legal framework*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kufanya marekebisho ya sheria hizi katika Miswada hii iliyopo mezani, ndipo tupo pale alipopazungumzia Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, dhamira ya Mheshimiwa Rais, ni kuwawezesha hawa mabinti wa kitanzania waweze kufikia ndoto zao za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo ninaomba sana nipendekeze maboresho yafuatayo katika Miswada hii mitatu iliyopo mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 10 ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, inayofanya marekebisho katika kifungu cha 6(a)(5) katika Sheria ya Vyama vya Siasa, napendekeza kwenye lile neno ambalo linasomeka *gender* kwenye ibara hii ya 6(a)(5) iweze kuboreshwa, iweze kuwa *qualify*. Kwamba isiwe tu ni *gender* lakini iwe ni *gender equality*. Kwa misingi gani, kifungu hiki kwenye hii sheria kinavitaka vyama vya siasa vi-*promote,* kwa sababu hapa kifungu kinasema, *a political party shall promote*. Kwa hiyo imeweka pale, *to promote democracy, good governance,* mambo mengi lakini ikaorodhesha pia *gender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mapendekezo haya ni kuboresha, ku-*qualify* ile *gender* iliyoandikwa kwenye kifungu hiki iwe *gender equality*. Kwa muktadha ya kwamba *a political party shall promote gender equality*. Kwa nini? Kwa sababu mpaka muda huu *gender* tunayo, ambacho hatuna ni *gender equality*. Ndiyo tunapotaka kuelekea, *so we need to promote gender equality*. Kwa hiyo msingi wa kupendekeza mapendekezo haya, maboresho haya ni kwamba twende kwenye ile *concept* sasa ya ku-*promote gender*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tafsiri yake ni nini hapa? hapa hamna asilimia, haijawekwa, tumeweka *end goal*, ambapo *end goal* tunataka tufike kwenye usawa wa kijinsia. Lakini tafsiri yake ya hapa, wanaposema ku-*promote* ni kwamba kila chama, kwa utaratibu wake wenyewe kwa mbinu zake zenyewe ibuni kuweza kuchochea, kuimarisha na kukuza usawa wa kijinsia katika michakato ya kisiasa kwenye vyama vyao; jambo ambalo mimi naona halina shida kwa tafsiri hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni muhimu sana kwa sababu inabidi tuweke misingi ya vyama vya siasa kuendelea kukuza usawa wa kijinsia kwenye vyama vyao. Mimi naweza nikazungumza kwa mfano chama ninachotokea mimi. Chama ninachotokea mimi kina mbinu nyingi za kuwawezesha wanawake na kuongeza idadi ya wanawake kwenye mchakato wa kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tu. Mwaka 2022 wakati Chama chetu cha Mapinduzi kinafanya uchaguzi wa kuchaguwa Wajume wa Halmashauri Kuu ya Taifa, waliweka asilimia 30 ya wajumbe hao wawekezaji ni wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni jitihada ya kukuza kufikia usawa wa kijinsia. Kama kuna vyama pia vya kuigiwa mfano kupigiwa mfano nadhani chama chetu ni cha mfano. Chini ya Mwenyekiti wetu imara Dkt. Samia Suluhu Hassan, hatuna mashaka kwamba yeye anasimamia suala hili na tunaamini sisi, kwa maana tu ya sheria kwa sababu sheria zinaishi; sheria itatumika leo, kesho lakini itatumika hata miaka 10 baadaye; sisi wengine tumesimama hapa kama wabunge. Mimi nimechaguliwa kuwa Mbunge nikiwa nina miaka 25 ni kwa sababu ya sheria zilizotungwa miaka 15 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawaomba sana waheshimiwa wabunge kwenye suala hili tuweze kuliangalia na tulipe uzito unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8 cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinatoa sharti la kwamba kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutakuwa kuna rejesta. Rejesta hizo ni rejesta ambazo zitaorodhesha vyama vya siasa, kuna rejesta ya kutaja viongozi wa kitaifa, kuna rejesta ya viongozi wa vyombo vya maamuzi vya kitaifa vya vyama vya siasa na kuna rejesta ya *Body of Trustees* (Baraza la Wadhamini wa Vyama vya Siasa).

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Msajili wa vyama vya siasa katika Muswada huu chini ya ibara ya 13 ambapo hii ibara ya 13 kwenye Muswada imeanzisha kifungu 10(c), Msajili wa Vyama vya Siasa amepewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera ya jinsia na ujumuishwaji wa makundi ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili huyu Msajili wa vyama vya siasa aweze kusimamia kazi yake vizuri anahitaji taarifa, anahitaji *data*. Sasa *data* atazipataje kama hakuna rejista maalumu ya kuonyesha chama cha siasa kina viongozi gani wa jinsi gani wa umri gani na wa hali gani ya ulemavu katika ngazi zote za chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna umuhimu ili tumuwezeshe Msajili wa Vyama vya Siasa aweze kutekeleza kazi yake, kuifanya kazi yake vizuri yakusimamia sera ya jinsia na ujumuishwaji wa makundi maalum awe ana taarifa. Kwa hiyo ziongezwe rejesta za viongozi wa ngazi za mikoa, wilaya, kata ambazo zina taarifa muhimu kama vile jina, jinsi, umri, hali ya ulemavu; ili sasa kifungu hiki kilichoanzishwa katika ibara ya 13 ya Muswada kiweze kutekelezeka na kisimamiwe vizuri na msajili wa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati wa michakato ya uchaguzi iongozwe na sifa, uwezo na vigezo vya mgombea na siyo umahiri wake wa kusuka majungu, fitna, kashfa, matusi dhidi ya mgombea mwenzake. Imefika wakati viongozi wachaguliwe kwa sifa, vigezo na uwezo wao wa kutekeleza majukumu yao kwa dhamana wanazochaguliwa. Kwa muktadha huo ninapendekeza kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ufanyiwe marekebisho ili tuongeze Kifungu cha 135 ambacho kitaweka kosa la ukatili wa kijinsia katika muktadha wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haitatosha hapo, pia ninapendekeza Ibara ya 137(2)(a) iweze kuboreshwa ili mtu aliyethibitika kujihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia asipate manufaa ya kushinda uchaguzi, hali ya kuwa alitumia mbinu hizo ovu kujipatia ushindi. Kwa hiyo, katika kupinga matokeo ya uchaguzi kwa Mbunge, Kifungu hiki kiboreshwe ili kosa hili la ukatili wa kijinsia liwe ni kosa mojawapo ambalo linaweza likamuondolea Mbunge aliyeshinda ushindi wake kama aliupata kwa kutumia njia ovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza pia Ibara ya 147(2)(a) na yenyewe iboreshwe kwa misingi hiyo hiyo katika ngazi ya uchaguzi wa Madiwani, matokeo ya uchaguzi wa Diwani. Kwa hiyo, ninaendelea kusisitiza tuna wajibu mkubwa sana. Mabinti wa Kitanzania wapo kwenye runinga zao wanatutazama wanasubiri waone kwamba tumetimiza wajibu wetu ili na wao waweze kufikia ndogo zao za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Katimba hiyo *gender equality* naona umegusia mabinti tu mbona hugusii vijana wa kiume? Tunaendelea Mheshimiwa Raymond, ajiandae Mheshimiwa Omar Issa Kombo, jiandae Mheshimiwa Kanyasu**.** *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kipekee ninamshukuru Mungu, kwa fursa hii na afya njema tunajadili jambo kubwa sana hapa ndani. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuruhusu jambo hili likaja huku Bungeni wakati muafaka. Pia, ninampongeza Waziri alieliwasilisha hapa, ninataka kusema nimezungumza ni wakati muafaka kwa sababu huko nyuma jambo hili lingekuja lisingepata *support.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu nina uhakika, mimi nilikaa mezani na Mwalimu Nyerere tukinywa chai miaka ya nyuma wakati anaelekea *St. Thomas,* wakati huo mambo ya Beijing yalishaanza. Katika mazungumzo tu ambayo siwezi kuyasema yote, alisema sasa hivi wanawake mnaonekana mmekuwa wasomi, bado wanaume hawajawaelewa, ndiyo maana waliporudi Beijing hawakuweza kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyinyi ni mashahidi, wakati Mama Mongela amerudi kutoka Beijing yakaja haya maneno ya 50 kwa 50, wanaume Tanzania halidhani labda wake zao wanawataka waende jikoni wakapike, wake zake wanataka wakawafulie,

hawakuelewa kwamba wanatakiwa wawa-*support* wanawake ili na wao waweze kutoka wawe na nafasi kwenye uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ninasema Mwalimu aliona litaingia wakati ambapo jambo hili litapata *support* na leo ninasisimka ninaona ushahidi. Kila mwanaume aliyesimama hapa ame-*support* hii ajenda ya wanawake kuwa na usawa na uwiano kwenye uongozi. Tunawashukuru sana wanaume Waheshimiwa mliosimama hapa mmekuwa vinara wa kweli, mmekuwa wathubutu wa kusema hamuoni sababu tena kwa nini wanawake wasiwe 50 kwa 50 katika nyanja zote za uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeletewa miswada hii tuweze kuijadili, nilifanikiwa kwenda kuwakilisha viongozi wa Bunge hili katika Kikao cha tarehe 5 Januari. Mwalimu *Nyerere Convention Centre*, ambacho alikuwa ameitisha Jaji Mtungi. Tulipewa elimu na mimi nilikaribishwa na ULINGO, ULINGO hii inaongozwa na Mheshimiwa Anna Abdallah na Katibu wake ni Dkt. Maria Semakafu. Kwa hiyo, ninaleta taarifa kwamba katika kikao kile zilitoka hoja za kila *NGO's* pia katika vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika chama chetu cha siasa cha CCM, Mwenyekiti wetu wa Umoja wa Wanawake Ndugu Mary Chatanda aliwasilisha hoja zetu, nazo zilipokelewa lakini baadaye wadau walikuja huku Dodoma na waliweza kuwasilisha hoja zao ambazo zimejadiliwa hapa kwa kirefu kabisa. Ninaomba nitoe shukurani hizo na ninatambua michango mizuri aliyokuwa ameitoa Mheshimiwa Getrude Mongela, Mheshimiwa Anna Abdallah na ninasema ilipokelewa na ikaungwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Sura ya Tatu, kifungu cha 32, uteuzi wa Wagombea wa Kiti cha Rais, Makamu na Rais. Ninapendekeza kila chama cha siasa kitakachoingia kwenye uchaguzi, endapo kitaleta mgombea urais ambaye ni mwanamke basi Makamu wa Rais aje na ile *gender*

nyingine awe mwanaume na iwe hivyo kwa vyama vyote ili tuweze sasa kwenda kwenye uwiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu ikawa hivyo kwa sababu tumeona wazi kwamba vyama vingine vina mfumo dume na havioni tena umuhimu wa wanawake kugombea katika nafasi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi hiyo ikawa tu kwenye ngazi za juu tunakwenda kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa, ninaomba sana elimu itolewe zile nafasi ambazo tunapewa wanawake zijae na zitoshe, haina maana tunapewa hizo nafasi halafu hazitumiki zote kwa sababu wanawake hawana uelewa wa kutosha wa kwenda kugombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni nini, zinapobaki wazi wanaume wanakwenda kuziziba. Sasa kama huku chini hatujaandaa mazingira mazuri, tukapanda kukienda katika hali ya kuelewa na kuchukua fomu hasa wanawake sisi, vijana, watu wenye mahitaji maalum, hizo nafasi zitajazwa na wanaume tu na hapo tutamlaumu nani? Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba sana katika huu Muswada liwepo eneo la kuweka elimu kwa umma kuhusu nafasi za *gender* kwenda katika kuchukua fomu za Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanakuwa na hofu na hapa imezungumzwa sana, yote hii ni kwa ajili ya ukatili wa kijinsia, matusi mtu hathubutu kuchukua fomu ataonekanaje kule kanisani, ataonekanaje kule msikitini, ataonekanaje kwenye jamii, lakini kama kutakuwa kuna *level* sawa ya kugombea wake kwa waume katika usawa na katika hali ambayo haina vurugu basi kila mtu atakuwa na ushujaa au atakuwa imara kwenda kuchukua fomu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuwa vigumu sana inapokuja kwenye gharama za uchaguzi, niliona kama imeondolewa lakini sikuona vizuri zile gharama za uchaguzi waporudisha fomu Madiwani na wale watu wenye mahitaji maalum. Wakati mwingine hawana hela na utaona dhahiri wametokea Madiwani wengi wenye mahitaji

maalum walemavu kutokea Viti Maalum kwa sababu wanawake wenyewe wana huruma, sikuwaona katika wagombea wanaume wengi Madiwani ambao wa mahitaji maaluum. Kwa hiyo, labda katika kurudisha fomu hawakuwa na namna ya hiyo hela au vijana pia. Vijana wengi wamemaliza shule ni machachari wanataka kuwa wagombea, Madiwani, Ubunge lakini hizo gharama hawana. Ninaomba hilo pia liangaliwe nani atawasaidia hawa kukidhi gharama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba kwenye Ubunge wa Viti Maalum ni kweli Katiba ya nchi inasema isizidi theluthi moja *(one third)* lakini siri dunia nzima inazungumzia *50/50, SADC* wanazungumzia *50/50*, *East Africa* wanazungumzia *50/50* na kote kwingine, leo dunia inaangalia Tanzania kama mfano. Mheshimiwa Rais ni mwanamke, Mheshimiwa Spika wa Bunge ni mwanamke lakini siyo Spika wa Bunge tu ni Spika wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Duniani, sasa sisi leo kila kinachofanyika hapa tutake tusitake tunaangaliwa na watu wanajifunza kwetu, tunaonesha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ulikuwepo kule kwenye uchaguzi wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa wale ambao hawakuwa na *gender* katika idadi ya watu wao waliokuwa wamekuja pale hawakupewa hiyo nafasi nzuri, kura zao zilishuka. Ni Jambo ambalo Watanzania tunatakiwa tujifunze tujue kwamba *gender inclusive* ni kitu ambacho hakikwepeki, lakini katika hatua gani? Katika hatua ya usawa. Hapa ninachokiomba ni usawa wa wanawake katika kugombea ninaliomba sana liwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo sijagusa Katiba, kwa sababu itakuja wakati ambapo inatakiwa lakini tunakwenda tunatoka hapo, tulipo hapa tulipofika bado ni kidogo, Beijing walisema ikifika 201, tutakuwa tumeshakuwa 50/50, haikuwa! Sasa lazima tuangalie njia ambayo inatufikisha pale, ni ipi hiyo? Ni pamoja na huu Muswada, Muswada ambao unaangaliwa kwa kamera kubwa, tochi na macho, bahati nzuri sana hapa ndani wanaume wote wametuunga

mkono, hakuna ambaye amesimama akasema hilo haliwezi, hajatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana vinara wetu mmetuunga mkono kwa nguvu kubwa, ninaamini kabisa jambo hili linaenda kutendeka, kwa sababu limekuja wakati muafaka wanaume wameshaelimika, kwamba tunaloomba wanawake siyo kwamba tunataka wakatuoshee masufuria, wao ni vichwa nakubali wanaume ni vichwa vya nyumba na vichwa vya kaya na kila mahali nasi wanawake ni shingo tutashikilia vichwa hivyo vizuri sana tukatunge hizi sheria kadri tunavyoweza kuziboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia usawa huo huo katika kugombea, ninaomba sana sheria hii iweze kusema wazi ni wakati gani wanawake wakichukua fomu wanaruhusiwa wenyewe wanawake waende bila kuingiliwa na kikwazo chochote. Kikwazo ninachozungumzia hapa ni nini? Unakuta hata ni kwenye majimbo anachukua mwanamke Jimbo, kauli zinatoka ni ninyi wanawake mna nafasi zenu za Viti Maalum kwa nini msiwaachie wanaume, sasa hiyo ni dhana potofu sana, vile Viti Maalum vilikuja kama *affirmative action,* imekwenda mpaka hapa ilipo na tunaitaka na tunashukuru wala hatutaki Viti Maalum viondoke, ukiona mtu anayetaka Viti Maalum viondoke hajaelewa vipo Kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka sasa hata hayo Majimbo wanaume wanaona kwa vile tuna Viti Maalum basi sisi hatutakiwi kwenye Majimbo, hili jambo halijakaa sawa, hapo tena ninaomba elimu itolewe kwa kiasi kikubwa sana ili tuweze kujua kwamba kote inawezekana, Viti Maalum inawezekana, Majimbo yanawezekana, muhimu zaidi wote tuende tukiona kwamba tunaweza kutembe pamoja Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha ulimwengu, ametuonesha Watanzania kwamba yeye ni mwanamke ambaye ameweza kuiongoza nchi kwa utulivu ambao ni mzuri na wote tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa tuchape kazi na tusimame tusimamie Sheria zetu wale wanaoleta choko choko kwa ajili ya vitu vidogo vidogo kutuletea fujo ili kutuchelewesha tusiwape nafasi. Hakuna mtu anayetaka akimbizwe kimbizwe vijana wake au watoto wake waache kusoma, eti kwa sababu tu ya mambo ya kurekebisha sheria. Sheria hii inayoenda kutungwa ni nzuri imekubalika, lakini kwa hayo ambayo tumeyaomba sana ya kuondoa ukatili wa kijinsia, ya kuongeza nafasi kwa wanawake, tunaomba wote tuendelee kuizungumzia na wote sasa walioleta hapa akiwepo Mheshimiwa Waziri Jenista na Naibu Waziri ninampongeza sana. Pia Waziri wa Katiba na Sheria ni mwanamke ni jambo ambalo ninaliona limekaa vizuri, limekaa kimuujiza muujiza, tukishindwa tena safari sijui ni wakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba wote wanaoendelea kuchangia tuendelee kuwaunga mkono, miswada hii ipite kwa kwa kishindo kabisa, wote tuipitishe asionewe mtu na wote tuende kuhakikisha kwamba tumefikia azma yetu ambayo siku zote tunaizungumza. Hata kama haitafika mwaka huu, tutaendelea kuona kwamba tunaenda kufika 50/50.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata matokeo ya sensa na wameeleza wengi akiwepo Waziri Kiongozi Mstaafu Mheshimiwa Nahodha kwamba wanawake ni wengi kuliko wanaume na ni kila mahali, sasa sidhani kama wanaume mliopo hapa mngependa tu tuendelee kuwa wengi bila kuwa na tija. Kama ni darasa tunakwenda shuleni wote…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond, malizia muda wako umekwisha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba mtuunge mkono na wewe wenyewe pia, tuendelee kuchapa kazi na kazi iendelee. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mheshimiwa Kanyasu ajiandae na Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema Mola ambaye anaendelea kutupa neema yake ya uhai na kuniwezesha kusimama kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wetu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi kubwa anayoifanya. Siku moja nilikuwa ninafuatilia tukio moja la Mheshimiwa Rais, nadhani alikuwa anaapisha viongozi akasema kwamba Mheshimiwa Jenista ni kiraka. Kwa kweli siku ile nilikuwa bado sijamfahamu anamaanisha nini, lakini ninapenda kukuambia kwamba kupitia mchakato huu kweli nimeamini kwamba Mheshimiwa Jenista ni kiraka. Ni Mama mwenye uwezo mkubwa lakini ana umakini mkubwa pamoja na Naibu Waziri wake na timu yote aliyofuatana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mchakato haukuwa rahisi, kama si kuwa na Mama kama huyu kwa kweli mchakato haukuwa rahisi wa kuchakata maoni ya wadau hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Taifa letu. Waislam kuna aya inasema asiyemshukuru binadamu mwenzie hata Mungu hatamshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna msemo wa Kiswahili unasema ada ya mja hunena muungwana ni vitendo. Kama haitoshi kule sisi Micheweni Wapemba tunasema, mwenye nguvu mna nguvu mpe nguvu, maana yake anayejitahidi anatakiwa

kupewa moyo. Kuna kila sababu ya kumpa moyo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama huyu ameonesha kwa dhati ya moyo wake kwamba ana dhamira ya dhati kuleta mabadiliko katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nami nichangie miswada hii ya Sheria iliyopo mbele yetu. Hatua hii ya Miswada hii ni hatua ya Mheshimiwa Rais kutekeleza ile falsafa yake *4Rs,* vilevile ni hatua inayotokana na maoni ya kikosi kazi ambacho Mheshimiwa Rais alikiunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajielekeza kwanza kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge pamoja na Madiwani. Tukiangalia kwenye Ibara ya 6 fasili ya (1) ambayo inazungumzia uteuzi wa Wakurugenzi kusimamia uchaguzi. Maoni mbalimbali yalitolewa, tuliwasikiliza wadau na hata baadhi ya viongozi wengine walikiri kwamba hawa Wakurugenzi hawana shida. Wakatolea mifano uchaguzi wa mwaka 2005, 2010 na 2015 kwamba kote huko hakukutokea shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi hata Mahakama ya Afrika ilikubaliana kwamba Wakurugenzi waendelee kusimamia uchaguzi kwenye *case* Namba 11 ya 2020. Kutokana na usikivu na kuona kwamba tusikilize maoni ya wananchi pamoja na wadau, basi Kamati tulikubali kukifanyia maboresho kipengele hiki kwa kusema sasa hata Maafisa wengine Waandamizi wanaweza kusimamia uchaguzi. Maana yake kuondoa ulazima wa kwamba lazima awepo Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Watanzania, mabadiliko haya hayamaanishi kwamba Mkurugenzi hataweza kusimamia uchaguzi. Inatoa fursa kwa Maafisa wengine, kwamba ikitokea mfano labda kuna mashaka ya uaminifu wa Mkurugenzi au utendaji wake, basi pawepo na ruhusa ya kupewa Afisa mwingine Mwandamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niwatoe hofu Wabunge wenzangu. Jana nilikuwa nafuatilia taarifa ya habari kupitia *UTV*, walikuwa wanasikilizwa baadhi ya wadau waliokuja mbele ya Kamati kutoa maoni yao. Kwa asilimia kubwa takribani wote walikiri kuwa maoni yao yalisikilizwa. Baadhi ya wadau, mfano Katibu Mkuu wa Chama cha *ACT* Wazalendo, Ndugu Ado Shaibu nilimsikia akisema kweli maoni yamesikilizwa; hata Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa Mheshimiwa Khatibu alikiri kwamba maoni yao yalizingatiwa na kusikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huu ni mfano kwamba kweli Kamati tulijitahidi kupokea na kusikiliza na kuyafanyia kazi maoni ya wadau. Sasa anapotokea mtu pembeni kusema kwamba hakuna chochote kinachofanyika, nadhani huyo ana jambo lake, ana ajenda yake nyingine ambayo sisi hatuifahamu wala hatuna haja ya kuifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, naomba niende kwenye Ibara ya 20 fasili ya (2) inayozungumzia juu ya ada kwa mwananchi ambaye kadi yake ya mpigakura itaharibika, kupotea au kufutika. Kwa kweli naipongeza Serikali ilikubaliana nasi Kamati kuondoa ada hii. Tunapofanya hivi, maana yake, tayari tunaenda kuleta ule ushirikishwaji wa wananchi, kuongeza idadi ya wananchi kuweza kushiriki katika zoezi la kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba kulingana na hali za wananchi wetu, pengine ingetokea mwananchi asiwe na uwezo wa kulipia ada hii kutokana na kitambulisho chake kuharibika, lakini kitendo hiki cha Serikali kutukubalia Kamati kwamba tuondoe ada hii, maana yake tunaenda kutanua mawanda, kuwataka wananchi waweze kushiriki zaidi katika zoezi la uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni katika Ibara ya 21 fasili ya (2) iliyozungumzia vile vile juu ya kulipia ada kwa mwananchi anayehitaji kubadilisha taarifa katika kadi yake ya mpigakura.

Naipongeza tena Serikali, Mheshimiwa Waziri kwa kutukubalia sisi Kamati pamoja na wadau kwamba tuondoe hii ada, ikiwa na lengo lile lile kama nilivyosema awali kwamba ni kutoa fursa kwa wananchi kuweza kushiriki katika uchaguzi na vile vile kumwondolea mzigo mwananchi wa kutoa fedha ambayo tungeweza kumwepushia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naipongeza sana Serikali kwa kusikiliza maoni yetu. Haya yote ni kutokana na wadau, walikuja mbele ya Kamati, tukawasikiliza na tukawazingatia. Kwa kweli niseme kwamba hizi ni hatua kubwa sana ambazo tumezifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, nizungumzie Ibara ya 54 inayozungumzia mgombea kupita bila kupingwa. Kwa kweli msingi wa hoja hii ni maamuzi ya Mahakama Kuu ya Tanzania kwenye kesi Na. 19 ambayo ilipelekwa kule juu ya malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na wadau kwamba kwenye uchaguzi uliopita kuna viongozi walipita bila kupingwa. Hii kutokana na mfumo wa kisiasa katika nchi yetu kwa vile tunashindana kivyama, kwa maoni yangu ilikuwa haina shida, lakini kwa vile Mahakama imeshatoa mapendekezo na wadau wameleta maoni tumeona kwamba tuyasikilize; na Mama Samia Suluhu Hassan ameleta marekebisho na kutaka tuyasikilize. Tuyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maana yake hakutakuwa tena na mgombea kupita bila kupigwa. Ikitokea mgombea yupo peke yake, basi anakwenda kupigiwa kura na wananchi waweze kumpigia kura ya ‘Ndiyo’ au ‘Hapana.’ Lengo na madhumuni kwanza, ni kuwawezesha wananchi kushiriki kuwachagua viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, kulikuwa kuna hoja hapo kwamba mtu anapopita bila kupigwa kuna watu wamejenga dhana kwamba huenda pengine mgombea huyu ametoa fedha kwa wagombea wengine ili waweze kuondoka. Kwa hiyo, inapoleta shida hii maana yake inakwenda kujibu hoja hii, inaenda kufuta kilio hiki kwamba kumbe ilikuwa hakuna fedha yoyote ambayo ilikuwa inatolewa. Kama haitoshi vile vile itatanua wigo wa kidemokrasia,

kuwapa fursa wananchi waweze kuchagua viongozi wanaowahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niende katika Ibara ya 135. Ibara hii inazungumzia juu ya makosa ambayo yanaweza kuhesabika kama ni makosa ya kiuchaguzi. Tumezungumzia matangazo; kuchafua matangazo. Sisi kama Kamati tulipendekeza kwamba ikiwezekana paongezwe na kosa la udhalilishaji wa kijinsia. Lengo na madhumuni ni kwenda kuwapa nafasi zaidi akina mama zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba katika chaguzi mbalimbali kwamba sote Wabunge wanawake na wanaume, hususan akina mama wamekuwa wakikumbwa na vitendo vya udhalilishaji. Yaani baadhi ya watu walihisi kwamba wakati wa uchaguzi kama hivi kuna fursa ya kumdhalilisha mwanamke, kumtolea matusi ambayo hayana maana, ni kitendo ambacho hakikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba kama kuna Taifa tunatakiwa tuondoe hofu juu ya uwezo na umakini wa mwanamke, basi ni sisi Watanzania. Kwa sababu mifano ipo hai, katika Taifa letu tunaongozwa na mama shupavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kama haitoshi, Waziri anayesimamia Miswada hii ni mwanamke, na kazi yake ameifanya vizuri. Naibu wake ni mwanamke, pia Waziri wa Ulinzi ni mwanamke, Waziri wa Katiba ni mwanamke, hata Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali kule Zanzibar ni mwanamke, vile vile Spika wa Bunge letu ni mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi hata kule ninakotoka mimi, Kaskazini Pemba tunaye Mkuu wa Mkoa makini mwanamama Salama Mbarouck Khatib na Mkuu wa Wilaya ya Michuweni Bi. Mgeni Khatib Yahaya, hawa akina mama wanafanya kazi sana. Mkoa wa Kaskazini, huku nyuma ilikuwa inafahamika kama ni mkoa wenye majungu, wenye mashaka, lakini tokea kuingia Mkuu wa Mkoa wangu Bi. Salama, kwa kweli Mkoa umenyooka, kazi

inafanyika na maendeleo yanakuja na Mkoa wetu upo salama. Hii yote inadhihirisha ni jinsi gani akina mama wapo makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Nitaangalia kwenye vipengele vinavyozungumzia juu ya upatikanaji wa Mwenyekiti. Hapa kuna maoni mawili. Kuna jedwali la Serikali na letu sisi Kamati. Jedwali la Kamati linasema kuwa Mwenyekiti apatikane kupitia mapendekezo kwenye Kamati ya usaili na Serikali wao wanasema kwamba Mwenyekiti apatikane kutokana na mapendekezo yanayotolewa na Jaji Mkuu kwa kushauriana na Jaji wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wangu, nahisi mapendekezo ya Serikali yapo vizuri zaidi, kwamba Mwenyekiti apatikane kutokana na mapendekezo miongoni mwa majina ambayo yamependekezwa na Jaji Mkuu wa Tanzania kwa kushauriana na Jaji wa Zanzibar. Vile vile nije kwenye kipengele cha Wakurugenzi wa Tume, kwenye Ibara ya 18 ya fasili ile ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile tume hii ni Tume ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, naomba tuongeze fasili nyingine ambayo itawekwa Naibu Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi kutoka Zanzibar. Hii italeta usawa wa Muungano wetu tukizingatia nafasi nyingine mbalimbali inayokuwa inafanyika, mfano Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Makamu wake anatoka Zanzibar. Kama haitoshi, Mwenyekiti wetu wa Chama, Makamu Mwenyekiti anatoka Zanzibar. Sasa hii itazingatia na kuleta ustawi wa Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Wabunge wenzangu, hili tulipitishe kwamba kuwepo na Naibu Mkurugenzi ambaye atatoka Zanzibar, ataweza kusimamia masuala yote ya tume kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niendelee kuchangia kwenye Kifungu cha tisa kinachozungumzia Kamati ya usaili. Napenda niseme kwamba hii ni hatua kubwa sana ya mabadiliko. Ukiangalia

namna inavyopatikana tume, imeelezewa vizuri kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano kwenye Ibara ya 74.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upendo wake Mama huyu ametoa fursa kwamba kuundwe chombo kingine ambacho ni Kamati ya Usaili. Huu ni ushupavu wa aina yake. Huu ni ujemedari wa aina yake, kwamba sasa kutakuwepo na Kamati ya usaili ambapo watawafanyia usaili wajumbe hawa na baadaye kupeleka mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya hatua ya uteuzi. Kwa kweli hii ni hatua kubwa sana ya mabadiliko katika mfumo wetu wa siasa. Mama huyo ameamua kwa dhati kuleta maridhiano katika Taifa letu, na siyo kwenye siasa tu, hata kwenye jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anaingia madarakani, sisi sote ni mashuhuda. Mfano tulikuwa tunalalamikia kesi za mashehe wetu wa uamsho ambao walikuwa wapo magerezani. Mama huyu kwa kutaka maridhiano ya kitaifa, aliwatoa mashehe hao magerezani na kuwafutia kesi. Kama haitoshi, kulikuwa kuna malalamiko ya wananchi ambao walikuwa wametolewa kwenye mfumo wa kazi kutokana na sekeseke la vyeti feki. Mama huyu aliwarudisha kazini waliostahiki na kuwapatia stahiki zao. Nani kama Mama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, kulikuwa na baadhi ya vingozi wa kisiasa wapo magerezani wakisota. Mama huyu aliwatoa magerezani, akafuta kesi zao. Kama haitoshi, kuna wengine walikuwa wapo nje ya nchi, walikuwa wameikimbia nchi, akawaita akawaambia njooni tujenge Taifa letu. Kama haitoshi kuna mambo mengi ambayo ameyafanya. Sasa tunapompongeza Mheshimiwa Rais, hatumpongezi kwa bahati mbaya, ni kutokana na kazi kubwa ambayo ameifanya katika Taifa letu. Tunamwomba sana Mwenyezi Mungu ampe nguvu, amwongezee ulinzi, aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilishamwita Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Bushiri, sasa kwa kibali maalum kuna baadhi ya Wabunge ambao wamepewa kazi maalum watachangia mapema. Baada ya Mheshimiwa Bushiri atakuja Mheshimiwa Kabudi, Dkt. Alice na Mheshimiwa Kilumbe. Tunaanza na Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia Miswada hii muhimu ambayo kimsingi ni Miswada inayokwenda kutupa mustakabali wa Taifa letu, Taifa ambalo dunia nzima inajua ni kisiwa cha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake yote ambayo inamshauri, lakini wanafanya kazi yao vizuri. Kwa kweli nitumie fursa hii kipekee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake, vile vile na Ofisi nzima ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wamechukua muda wa kutosha kufanya kazi ya uchambuzi na kutuandalia hoja hizi muhimu ambazo tunazijadili siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunafika leo, hoja hizi zimepita kwenye maeneo mbalimbali. Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati yake nzima kwa uchambuzi wao na maoni yao ambayo wamefanya kwa niaba yetu. Kwa kweli tunachangia kwa sababu tunataka kuongeza tu maneno machache, lakini ushauri wa Kamati ulikuwa ni ushauri ambao tulipousikiliza tuliridhishwa kwamba Kamati ilifanya kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee pia naomba niwashukuru na kuwapongeza wadau wote ambao walitumia nafasi yao ya kidemokrasia. Jambo hili liliruhusu kila mtu mwenye mawazo ya kizalendo ya kutaka kuisaidia nchi aje atoe maoni yake. Kwa hiyo, nawashukuru viongozi wa dini, tuliona uwakilishi wao, nawashukuru

viongozi wa asasi mbalimbali za kiraia, nawapongeza watu binafsi waliokuja kutoa maoni yao, nawapongeza viongozi wa vyama vya siasa na vyama vya siasa vyenyewe, na wanahabari ambao pia walitumia fursa hiyo hiyo kuja kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuseme ukweli. Kama Wizara hii ingechukua maoni ya kila aliyesema, halafu ikaamua yote iyalete tuje tuyajadili hapa tungemaliza miezi 12 tunajadili maoni haya na tusingepata muafaka. Kwa hiyo, naipongeza Wizara kwa kuchambua yale ambayo iliona haya yanafanana na tunachokizungumza na yanaweza kutupeleka kule tunapotaka kwenda kama Watanzania. Kwa hiyo, wale ambao walileta maoni yao na pengine kwa wakati huu hayapo sehemu ya haya tunayojadili, kwanza wasijione kama wamedharauliwa, lakini pili waamini kwamba isingewezekana kuchukua kila kitu kama vile unataka kujaza kitabu, lazima uchambue na utengeneze mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilianza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na kwa kweli niseme tunampongeza kwa sababu amebeba ajenda hii kwa utashi wake. Mapema kabisa alikuja na falsafa yake ya *4R* na Watanzania wengi hawakumwelewa, lakini katika maeneo hayo hayo alisema anatamani kuwafanya Watanzania wote wenye nia njema washiriki kutoa mchango wa kuiendeleza nchi yao. Katika eneo ambalo ni mahususi kabisa, huwezi kuendeleza nchi kama hali ya kisiasa katika nchi haieleweki. Akatamani kuleta hali ya utulivu wa siasa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametekeleza falsafa yake kwa vitendo. Nami nampongeza tena bila kupepesa macho kwamba wale ambao hawalioni hili, hawalioni kwa sababu walichotarajia wao ni kwamba kila wanachokiwaza wao basi tutakitekeleza, lakini anafanya kwa niaba ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika kutekeleza falsafa yake aliunda kikosi kazi, nami huwa sio mwepesi sana wa

kusifiasifia, lakini kikosi kazi kile kilichokuwa na mchanganyiko wa watu wenye taaluma mbalimbali kiliongozwa na Profesa, kilifanya kazi yake kwa uhuru mkubwa. Miongoni mwa watu tuliokuwa na wasiwasi ilikuwa ni sisi wana-CCM tukiwemo sisi Wabunge. Tukawa na wasiwasi hivi, kwamba hivi tunataka kufanya jambo gani hapa? Baada ya *presentation* ya Profesa na Kamati yake, tukagundua nia iliyokuwepo pale ni kuifanya Tanzania yetu iwe Tanzania iliyotulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Kamati ile ilifanya kazi yake vizuri na Serikali baada ya kupokea taarifa, ilikuja na hoja 83. Mengi yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge. Baada ya kupokea taarifa, tayari hoja 64 ilizichukua na kuzifanyia kazi. Jambo hili linaonesha utayari. Maana tunaposema Serikali, ni Mheshimiwa Rais. Angeweza kusema weka pembeni, tutafanya baadaye, lakini akasema hizo mara moja Wizara zinazohusika endeleeni. Hoja 12 utekelezaji wake unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili maana yake ni nini? Yapo mambo mengine huwezi kuyatekeleza *overnight,* yanahitaji mabadiliko ya sheria. Hoja nyingine zinagusa Katiba, na unapogusa Katiba, lazima ujue unaanzisha jambo kubwa ambalo pengine lingehitaji mjadala mpana zaidi kuliko wa watu 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nasema, Serikali imefanya jambo kubwa, imepokea mapendekezo, imeyafanyia kazi. Nataka Watanzania wafahamu, Mheshimiwa Rais, hafanyi haya kwa sababu anataka kumfurahisha mtu, anataka Watanzania wote wawe na haki sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa hoja ambazo zililetwa na Kamati ilikuwa ni pamoja na kupitia Sheria za Uchaguzi, Sheria za Vyama vya Siasa na kuangalia muundo mzima wa namna ambavyo uchaguzi wetu unaweza ukawa huru. Sasa nataka niwaambie watu ambao pengine hawaelewi, duniani kote kama

kuna kazi ngumu ni kujaribu kumpunguzia mtu madaraka, ni kujaribu kumnyang'anya mtu kitu ambacho amepewa kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomwona kiongozi ambaye anajua kesho kuna uchaguzi lakini anasema mimi pamoja na mamlaka haya nimepewa kikatiba, niliyewapa kihalali; kwa sababu huyu ni Rais ambaye tumempata kihalali, hakufanya mapinduzi; amekuja kwa mujibu wa Katiba, na Katiba anayoitumikia ndiyo hii ambayo imempa mamlaka ya kuteua na kufanya kazi zote, lakini anasema Hapana. Ninasikiliza maoni tubadili utaratibu, wapendekeze watu halafu mimi niseme katika hawa mliowapendekeza, basi huyu hapa mpeni kazi ambayo mnaitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie, duniani viongozi wa namna hii ni wachache, na Tanzania tunayo bahati kubwa sana. Angeweza kuweka pembeni kwa sababu jambo hili halijaanza leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kuwa mwanasiasa muda mrefu kidogo, malalamiko ya Katiba, Katiba Mpya yalianza miaka yote na yalikuwa yanasikilizwa, tunakwenda kwenye uchaguzi wanaoshinda wanashinda na wanaoshindwa wanashindwa na hamna mtu anayesikiliza lakini kwa nini amefanya leo? Kwa sababu tunaye Mheshimiwa Rais msikivu sana, ambaye amekubali kupunguziwa sehemu ya kitu alichokiapa kwenye katiba kwa ajili ya kuwalidhisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina wasiwasi kabisa na utaratibu uliowekwa wa namna ya kuwapata watu wenye sifa. Kwa sababu Kamati inayopendekezwa ni Kamati ya watu ambao mfumo wake wenyewe unaonekana ni watu ambao wanaaminika na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi nani ambaye anaweza kusema hamwamini Jaji Mkuu. Nani ambaye anaweza kusema hamwamini Jaji wa Zanzibar, ambaye tayari ni Jaji leo tumemkabidhi Muhimili mkubwa katika nchi? Ambaye itapendekeza kwenye Tume, halafu

unasema mimi simwamini. Sasa unataka tumwamini nani? Tukatafute mfanyabiashara fulani tumlete tumkabidhi pale halafu ndiyo tumpe kazi ya kupendekeza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana kabisa na mapendekezo kwamba, Mheshimiwa Rais baada ya kupendekezewa, ateue watu ambao tayari watakuwa wamechujwa na vyombo vyetu vyote. Jambo hili linafanyika siyo kwa bahati mbaya. Ni kwa sababu kwa kweli kimsingi lazima tuwe na viongozi ambao ni waandamizi wana dhamana na hawawezi kutumia mamlaka yao vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kuzungumza, liko kwenye *Political Parties Affair and Laws Amendment*. Kwenye sehemu ya 13, hapa yamezungumzwa mambo mengi kidogo. Nataka ku-*capitalize* na mambo machache. Moja, nitazungumza kwenye kipendele cha 13(b). Hapa anasema "*Registered Political Party shall at all time maintain the following documents*". *This is documents*, lakini nataka tuongeze mambo hapa kwenye sehemu ya *D; "The Parties Financial and Properties Managements Rules.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza? Duniani usipo-*control* mfumo wa vyama kupata pesa, kuna siku chama kitaletewa pesa na watu msiowatarajia na kitabadilisha Serikali nzima. Sasa lazima mjue kuna kitu kinaitwa *Illicit Financial Flows, illicit Financial Sources*. Huko watu wana mapesa mengi wame-*deposit somewhere* hayana kazi. Anaweza akaja hapa akaamua kubadilisha asilimia 80 ya Waheshimiwa Wabunge humu ndani. Akaamua kutafuta mgombea wake wa Urais. Akaamua kutafuta chama cha siasa akakipa dola milioni 500, kikamnunua kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kwenye maandamano, vijana wanasema niliitwa nikapewa shilingi 50,000. Nikawekewa mafuta, nikapewa na jezi nivae. Nikaambiwa twende kwenye

maandamano. Sasa *you can see,* kama ana uwezo wa kufanya hivyo kwenye maandamano ambayo yote anayoyazungumza yapo yamejadiliwa leo. Hebu fikiri anapata wapi pesa na hawezi kupata pesa ambayo inaweza kununua watu. Lazima kipendele hiki kitazamwe vizuri. Tuangalie na tu-*control sources* za *finance* za vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi jirani hapa wakati wa uchaguzi wa vyama vingi, gafla walikuta kwenye akaunti kuna dola milioni 40, dola milioni 40 imetumwa. Ilipozuiliwa kile chama cha siasa hakikufanya vizuri kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, *there should be mechanism* ya kuchunguza *sources* za *finance* za vyama, siyo *issue* ya kuangalia kumbukumbu za matumizi. Kumbukumbu za matumizi *its budget in, budget out.* Unapata wapi hizi pesa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikikupa kumbukumbu za matumizi ya shilingi bilioni 400 wakati income yangu ni shilingi bilioni 50, sasa *what does it mean*? Inakusaidia kitu gani? Lazima tujue kwamba hapa kuna kitu cha kufanya zaidi. Kuna *flow* ya pesa ambayo watu wana mapesa hawajui matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; kwenye *parties conduct*, imezungumzwa vizuri sana hapa ndani. Mara nyingi nikisikiliza habari ya *gender equality* kimsingi huwa nataka kupingana na wenzangu lakini nashindwa kwa sababu mama alinipa ukinara. Ningetamani pawe na fursa sawa inayomfanya mwanamke aweze ku-*compete* na kushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini inawafanya wanashindwa? Ni kwa sababu ya uoga wa kujitokeza kwenye jamii ambayo jamii ile ina *stigma* ya kuamini kwamba, mwanamke akijitokeza kwenye jambo fulani, huyu atakuwa amechanganyikiwa. Utaona sisi kule mara nyingi ukiona mwanamke anagombea mara nyingi wanasema wewe huo mji umekufa. Kwa sababu wanaamini kwamba, mwanamke akiwa kwenye siasa ameharibikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachotaka kuzungumza hapa kwenye eneo hili, siyo tu tuishie kwenye kutengeneza sheria ambayo inazuia pengine kukashfu na kufanya nini. Tutengeneze *mechanism* ambayo *opportunity* ile isifike pahala kama ilivyokuwa zamani. Tunahamasisha someni sayansi, watu wamesoma sayansi sasa imefika pahala pa kupeleka sayansi hamna. Sasa hivi tunasema wanawake watafika asilimia 80, tutaanza tena. Tuanze wanaume wanaume. Tutengeneze mfumo ambao utawabeba hawa wanawake, utawafanya wanawake wawe *competitive*. Yaani wasifike pahala akiingia pahala aonekane yeye amevamia jambo. Hapana, anayo sifa na uwezo. Kama ni kumbeba, unambeba kwa sababu uwezo anao jambo hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia ya sasa hivi iko *digitalized*, naweza nisikutukane wewe lakini nikatengeneza *clip* Marekani, nikaileta Tanzania ikasambazwa kote. Ikishasambazwa, tayari umechafuka. Sasa tuongeze hapa kwamba, hata huyo anayesambaza aingie kwenye makosa ya jinai. Siyo unapokea picha ya kashfa ya mtu, unaanza kusambaza kwenye mkutano. Ukimsubiria mpaka umsikie Kanyasu anamtukana, sitatukana kwa sababu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante, ahsante.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri. Atajiandaa Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia miswada hii mitatu ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kutuletea miswada hii mitatu katika Bunge letu. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama na pacha wake Mheshimiwa Ummy, kwa kazi nzuri walizofanya za kutuchakatia Miswada hii. Nisisahau Kamati, ikiongozwa na kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mhagama, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kuchakata Miswada hii na kutuletea katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Nilivyopitia katika taarifa, nimeona kwamba, mapendekezo ya Serikali, haikuweka kipengele cha uchaguzi wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipendele hiki ni muhimu sana, Waheshimiwa Wabunge wote waliosimama kuchangia hoja hii Bungeni, wote wameona kwamba, ni kweli jinsia hasa ya kike inanyanyasika sana kipindi cha uchaguzi. Wanawake wengi wana ari ya kugombea na wanapenda kugombea nafasi za uongozi mbalimbali lakini kinachowashinda wanawake ni ule uzalilishwaji kipindi kile cha uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoenda kama uongozi kushawishi baadhi ya wanawake wenzetu ili waingie katika michakato ya siasa, kugombea nafasi mbalimbali, huwa wanageuka wanatuuliza hivi nyie mnawezaje? Mnavumiliaje matusi mnayoyapata? Niseme kwamba, hali hii inazoofisha wanawake wengi ambao wana uwezo wa kugombea nafasi mbalimbali wakiogopa kudhalilishwa. Niseme, wanawake wote unaowaona wako katika hili Bunge wamepitia matusi, kudhalilishwa, kudharaulika na wamedhoofika lakini wamejenga ujasiri kwa sababu hayo matusi waswahili tunasema hayakuandikwa usoni. Watatukana sasa hizi na mimi baada ya masaa sita saba naendelea na shughuli zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naipongeza sana Kamati. Ilivyoona kwamba kuna umuhimu wa kuongeza Ibara ya 135, ambayo itautambua unyanyasaji wa kijinsia kuwa ni kosa la jinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ibara hii naamini kwamba, sheria ikiwekwa ikasimamiwa vizuri na ikatekelezwa, tutakomesha kabisa utamaduni huu. Nasema utamaduni kwa sababu imeshazoeleka ikaonekana ni mambo ya kawaida tu. Sasa utamaduni ule wa kutukana kila mtu ataogopa baada ya kuona kwamba, kumbe nikitukana kuna sheria. Pia, Kamati iliweka adhabu, ambayo ilikuwa ni kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili. Nyingine ilikuwa ni faini isiyopungua miaka miwili na isiyozidi miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza hii Habari ya faini tuitoe kabisa. Faini watu wanaweza wakamchangia hata kama mtu ameambiwa fani yake ni shilingi milioni tano, atachangiwa na atasaidiwa na atatoka. Nawaomba Wabunge wenzangu wote tuweke adhabu ya kifungo. Mtu atakapofanya kosa, akiiacha familia yake akaenda kutumikia jela, naamini kwamba wengi watakuwa wanaogopa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu ili tuikomeshe hii tabia ni vuzuri wote tukalindana. Kwa sababu inawezekana kwamba, mgombea mwenyewe hafanyi ile kazi lakini anatafuta watu wa kumdhalilisha yule mgombea mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetokea kule Moshi Manispaa, kule Moshi Manispaa kuna vurugu sana katika kipindi cha uchaguzi. Saa nyingine unakuta tuko kwenye mikutano ya hadhara, wanakodishwa vijana wakakuja wanajificha kwa sababu mazingira yetu kule kidogo tuna migomba. Wanakuja wanajibana mahali wanaturushia mawe wakati tukiwa tunafanya mikutano yetu. Hii sheria ikiwekwa ihakikishwe kwamba, inasimamiwa na itekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo. Nitachangia Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya Siasa. Nitaongelea suala la idadi ya wanawake kwenye vyombo vya maamuzi ya vyama vya siasa. Ukiangalia idadi ya wanawake kwenye vyombo vya maamuzi imekuwa ndogo sana. Hii ni kwanzia kwenye ngazi ya mabalozi, wenyeviti wa vijiji na mitaa, madiwani wa kata na Wabunge wa majimbo. Natoa mfano wa madiwani, kwa mfano, Moshi Manispaa tunazo kata 21 lakini madiwani wa kike wa kata ni wawili tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sana mashariki, wanazo kata 14, madiwani wa kata mwanamke ni mmoja tu. Ukirudi Same Magharibi, ziko kata 20, madiwani wa kata wanawake ni wawili tu na kwenye majimbo mengine iko hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba, tuhakikishe wanawake kwenye vyombo vya maamuzi wasipungue asilimia 30. Pia, napendekeza jambo hili liwekwe kisheria na hii sheria isimamiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina zaidi ya hapo lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, tuhakikishe tunapitisha Miswada hii kwa asilimia 100 ili iwe sheria za nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Kabudi, ajiandae Dkt. Alice, ajiandae Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa ruzuku ya uhai na afya, ambayo imeniwezesha na mimi leo kushiriki katika mjadala huu. Pia, nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mjadala huu wa miswada hii kitatu iliyoletwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na wale wote waliotangulia, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu na Mheshimiwa Naibu Waziri na wote katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuiboresha na kuileta Miswada hii, pia, katika jedwali la Serikali la marekebisho ambalo limeletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naishukuru sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Pia, kwa kunialika katika Kamati yao ili na mimi niweze kutoa maoni na mawazo yangu. Ambayo nimeona mengi yamezingatiwa katika jedwali la marekebisho ya Kamati lakini pia katika jedwali la marekebisho la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassani kwa uthubutu wake na utashi wake wa kisiasa wa kulileta jambo hili la Miswada hii mitatu ya uchaguzi ambayo inaimarisha demokrasia katika nchi yetu na kuimarisha umoja na utulivu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, Miswada hii ni miswada ambayo inaifanya nchi yetu ipige hatua nyingine mbele zaidi katika kuimarisha demokrasia ya nchi yetu. Kwa hali hiyo, naunga mkono tuipitishe miswada hii yote mitatu pamoja na marekebisho ambayo yameletwa katika Jedwali la Marekebisho la Kamati lakini pia la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yakija ni vizuri kuyatumia na hapa nakumbuka maneno ya busara ya Willium Shakespeare katika Riwaya ya Julius Seizer. Anaposema "*There is a tide in the affairs of men which taken at the flood, leads on to fortune; Omitted, all the voyage of their life. Is bound in shallows and in miseries. On such a full sea are we now afloat; And we must take the current when it serves, or lose our ventures" This is the time to*

*take the tide of the affair of men* katika hizi *4R* na katika Miswada hii mitatu iliyoletwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa hili lina historia ya miaka 66 ya kuendesha chaguzi za wabunge, madiwani na baadaye chaguzi za Marais. Ukitaka kujua hatua kubwa tuliyoipiga, turudi nyuma katika uchaguzi wetu wa kwanza wa Bunge wa mwaka 1958 na mwaka 1959. Tuone waliokuwa na sifa ya kupiga kura lakini tuone ambao walisimamia uchaguzi ule. Mjadala mkubwa uliokuwa katika Bunge lile mwaka 1958, ambao ulimfanya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kujiuzulu Ubunge lakini alipotoka akawasihi Wana-*TANU* washiriki katika uchaguzi… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabudi, hebu ondoka huko, njoo mbele kidogo. Njoo mbele kidogo kama *rows* mbili tatu hivi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunileta mbele. Kwa makuzi na malezi yangu ambayo Kaka yangu, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika anayafahamu katika dhehebu la dini yetu, tumeaswa daima kukaa nyuma kusubiri kuitwa mbele. Usije mbele halafu ukaambiwa nenda nyuma, kwa hiyo, nashukuru sana kwamba umenileta mbele wewe lakini mimi kunakonistahili ni huko nyuma lakini kwa heshima yako naipokea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea mambo makubwa sana yanayohusu Taifa letu. Hatuna budi kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuyaleta mambo haya ambayo yanatupeleka hatua moja mbele katika kukuza demokrasia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1958 Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipolazimika kulia Tabora, kuwasihi wana-*TANU* kukubali aina ya mfumo wa uchaguzi ambao ndani yake ulikuwa na ubaguzi kwamba, kila jimbo la uchaguzi lazima liwe na Mzungu, lazima liwe na Mhindi, lazima liwe na Mwafrika. Katibu

wake wa chama Zuberi Mtemvu ameongeza kundi kubwa la kukataa hilo na baadaye Zuberi Mtemvu, Katibu wa *TANU* kujitoa *TANU* na kuunda Chama cha *African National Congress of Tanganyika*, kupinga yale maamuzi ya kibaguzi lakini Mwalimu alisema; "Ni heri twende na hili ili baadaye tuweze kufanya mabadiliko makubwa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 66 baadaye leo tunafanya mambo makubwa. Ni vizuri tukaijua safari hii ili tusibeze haya tunayoyafanya leo. Ni vizuri kuijua safari hiyo ili tusikate tamaa kwamba kuna kesho itakayoboresha zaidi yale ambayo tunaona leo hayajawa vile tunavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu katika *4R,* katika uhai wa Taifa letu lote moja ya mambo ambayo ndiyo yanalitanabaisha Taifa la Tanzania ni *resilience* (ustahimilivu). Ndiyo maana tumefanya chaguzi katika nyakati ambazo watu hawakutegemea tufanye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa mwaka 1980 wa Rais, Wabunge na Madiwani, haukutegemewa kufanyika kwa sababu nchi ilikuwa imetoka katika vita ya kupambana na Nduli Iddi Amini, na hali ya uchumi ni ngumu na kila mtu alijua Mwalimu Julius Kambarage Nyerere angeahirisha uchaguzi. Lakini Mwalimu akasema twendeni kwenye uchaguzi; na hii ndiyo itakuwa mara yangu ya mwisho kugombea Urais, mwaka 1980. Lakini baada ya vita aliona asiiache nchi kabla ya kuiandaa. Tukafanya uchaguzi mwaka 1980 baada ya kutoka vitani na kwa kugharamia sisi wenyewe bila kupewa hata senti tano na mtu mwingine yeyote. Huu ni mwaka 2020 baada ya *COVID-19* hakuna aliyetegemea tungeweza kufanya uchaguzi, lakini tumeweza kufanya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini; Taifa hili katika zile *4R* alizotuletea Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, *resilience* ndiyo haiba ya Tanzania, *resilience* ndiyo msingi mkubwa

wa Taifa hili. Ni lazima tuendelee kustahimiliana ili tuweze kuleta mabadiliko ili tuweze kuleta maridhiano na ili tuweze kujenga Taifa letu upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Taifa ya Mwaka 2025, una sifa zote ambazo ni muhimu kuzielewa. Kwanza tujue tunatunga Sheria ya Uchaguzi katika aina gani ya dola sisi Tanzania, tofauti na wote wanaotuzunguka kikatiba sisi dola yetu is *a complex state* sio *simple state is a complex state* kwa sababu inatokana na muungano wa nchi mbili zilizohuru kuungana. Ndiyo maana Ibara ya Tano au Ibara ndogo ya Tatu ya Sheria hii inasema Mwenyekiti akitoka upande wa Tanzania Bara, Makamu atoke upande wa Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huioni hiyo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, DRC, Malawi, Zambia kwa sababu wao kikatiba *they are simple state* sisi *we are a complex state*. Kwa hiyo ni lazima tuwe na Tume ya Uchaguzi, ni lazima tuwe na mfumo wa uchaguzi ambao Zanzibar inaonekana na Tanzania Bara inaonekana na hasa kwa kuzingatia kwamba muungano wetu sisi ni *asymmetrical union* na katika *asymmetrical union* ni yule ambaye anaonekana kwa idadi ya watu na eneo ni dogo lazima apewe *minority veto right* na ndiyo hiyo iko ndani ya Katiba, hiyo ndiyo inayotofautisha Tanzania na nchi nyingine na ni vizuri Muswada huu umeizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sheria ni sheria. Lakini sheria ni lazima ipewe uhai na uhai huo wa Sheria na Katiba ni tabia, mila na desturi ya wanaohusika; na katika uchaguzi unahitaji mambo makubwa matatu uadilifu, uaminifu na uzalengo. Hayo tumeyaona Ibara ya 12 ya Muswada huu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi; pale inaposema Mjumbe wa Tume atalazimika kuzingatia Sheria na Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma na Kanuni za Maadili zitakazoandaliwa chini ya Sheria hii. Bila kuwa na maadili, uaminifu, na uzalendo hata utunge sheria ambayo kwa viwango vya Mtakatifu Thomas wa *Aquinas* vinakwenda kwenye *lex beginner*

na sio *lex humane* bado sheria hiyo haitofanya kazi kama mambo haya matatu hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nayaona katika Ibara ya 12, unayaona katika Ibara ya 18(1)(b) inapomuhusu Mkurugenzi wa Uchaguzi awe ni mtu mwaminifu na muadilifu. Kwa hiyo, jambo hili ni zuri sana na ni muhimu tulizingatie na tulieleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni lazima tujiulize tunatunga sheria hizi za uchaguzi kwa Taifa la aina gani? Taifa la Tanzania lina haiba yake, lina sura yake, lina mila zake, lina desturi zake. Haya yote yaliyozungumzwa na mimi niongeze sauti yangu yawe ya usawa wa jinsia, makosa ya uchaguzi dhidi ya jinsia; lakini msingi wake ni nini? lazima turudi kwenye Katiba. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 9(f); na mara nyingi Ibara hiyo haisomwi vizuri. Ibara ya 9(f) katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza bayana kwamba sisi tunafungwa na Tamko la Haki la Binadamu Duniani *(The Universal Declaration of Human Rights)* na mimi niwaambie, sisi ndiyo Katiba pekee katika Bara la Afrika ambalo *The Universal Declaration of Human Right* kwa mujibu wa Ibara ya 9(f) ni sehemu ya Katiba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na maana yake nini, sisi Katiba yetu hii inabeba kitu ambacho tunakiita ni *International Customary Law* katika mambo ya kuheshimu watu. Lakini Ibara ya 12(1) hadi (2) na mara nyingi tunasahau Ibara ya 12(2) sisi ndiyo Katiba pekee katika Bara la Afrika ambao hatuzungumzii tu usawa wa binadamu lakini tunazungumzia heshima ya binadamu *(human dignity)*. Haya yote tunayoyakemea msingi wake wa kuyazuia ni *human dignity*, Ibara ya 12(2) ya Katiba yetu lakini pia Ibara ya 13(4) inazuia ubaguzi wa aina zote na ukienda kwenye Ibara ya 13(5) miongoni mwa ubaguzi unaozuiwa ni ubaguzi wa kijinsia kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona niyalete haya mambo ya Katiba ili mjue haya yanayozungumzwa yana kitu katika Sheria ya Katiba tunachokiita *The Normative Principals of the State*. *Normative*

*Principals of the State* sisi moja ni *human dignity*, *human equality* na kuzuia aina yoyote ya ubaguzi kwa mtu yeyote kwa hiyo masuala hayo ya *violence against women in election* ni muhimu yawepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mawazo yaliyoletwa katika marekebisho ya Sheria kwamba Ibara ya Kwanza ya Muswada huu …

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hujaniruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini. Endelea Profesa Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakubaliana kwamba Ibara ya Kwanza ya Katiba ya Muswada ya Jina la Sheria ibadilike na tuongeze neno uhuru. Kwa hiyo hii iitwe kuwa ni Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halikinzani kabisa na Katiba linaendana na yale yote ambayo yamo katika Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na yanaendana na Ibara ya Saba ya Jamhuri ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania na yanayoendana na Ibara ya 74(11) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tofauti na Tume ya Utumishi wa Mahakama Ibara ya 112(1) na tofauti na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Ibara ya 129, Tume hizi zimetajwa kwa majina yake lakini ikija kwenye Ibara ya 74(1) imesema tu; "Kutakuwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba" nataka kusema nini kuongeza maneno hayo hakukinzani na Katiba kumepita ile *the constitutionality test,* kwa sababu imeruhusu kuweka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependekeza na nakubaliana na yale kwamba Ibara hiyo ya Kwanza ibadilishwe iongezwe neno 'huru' lakini pia Ibara ya Nne ya Muswada neno hilo

la Tume ya Uchaguzi Huru nayo pia iweze kuongezwa katika sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa katika uchaguzi, na hasa unapokuja kwenye *election management policy*, Sheria tulizoletewa hapa zaidi zimeangalia mambo mawili; *election management* na *election management policy*. Kuna moja ambalo linahitaji muda mrefu na huu labda sio wakati wake kwa sababu tunakwenda kwenye uchaguzi na ambalo hatujajigusa na ambalo lina majibu ya maswali yanayoulizwa hasa kuhusu *gender quality* na *gender equality* ya kwenye uchaguzi ni mfumo wa uchaguzi *(electoral system)*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Profesa una dakika mbili malizia.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulileta hapa na kulipendekeza kwako ni marekebisho ambayo nayapendekeza katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi. Ningependa Ibara ya 168(b) tuiangalie ninaona kuna *loop hole* Ibara ya 168 ya Sheria ya Uchaguzi tuiwekee ya kuweka ukomo kwamba zile fomu na zenyewe ziwe na ukomo kama ilivyo katika Ibara ya 168(a) na 168(b).

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningelileta tulifikirie ni lile ambalo limo katika Ibara ya 3, Ibara ya 85(2)(f) na Ibara ya 104(1)(i) ya Sheria ya Uchaguzi. Je, tutumie neno mtazamaji kama lilivyo humu au turudi kwenye neno mwangalizi ambalo limezoeleka na watu wengi. Neno mtazamaji ni tafsiri sisisi ya neno *observer* lakini neno mwangalizi ni tafsiri ya kimuktadha *(contextual translation)* ya kile ambacho tumekizoea. Kwa hiyo napendekeza Ibara ya 3, Ibara ya 85(2)(f) na Ibara 104(1)(i) tuweze kuibadilisha neno mwangalizi litumike badala ya mtazamaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize tu tunafanya mabadiliko makubwa mpaka mwaka 1990 Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi alikuwa Spika. Spika, ndiye alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya

Uchaguzi. Mpaka mwaka 1985 Katibu wa Bunge ndiye alikuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Sasa kutoka kwa Spika kuwa ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi na Katibu wa Bunge kuwa ndiye Mkurugenzi wa Uchaguzi; kwa leo kuwa na mfumo huu tumepiga hatua kubwa sana, ingawa bado mwendo tunao, tuzidi kusimamia. Nami naunga mkono hoja za Miswada yote hii mitatu pamoja na marekebisho ambayo nimeyapendekeza na yale ambayo yalitolewa pengine, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Profesa ahsante. Pengine utaonana na wahusika waandikie, nakushukuru sana. Waheshimiwa, sikutaka Profesa akatize kwa sababu nilikuwa najua *flow* yake na umuhimu wa *knowledge* yake kwenye masuala haya. Sasa mnaweza kuanza mataarifa huko mbele huko, Mheshimiwa Dkt. Alice, Mheshimiwa Kilumbe, jiandae. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimshukuru sana pia Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kupata nafasi ya kuchangia. Vilevile, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuwa na ujasiri mkubwa sana wa kuamua sasa Miswada hii iletwe na tuweze kuijadili kwa kufuata utaratibu chini ya uongozi wa Waziri makini sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, pamoja na Naibu wake na Katibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianzie kusema kidogo tu kwenye Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi. Mimi naipongeza Serikali sasa kwa kuamua kuleta Muswada huu, kwamba sasa hivi Tume nayo iwe na Sheria yake madhubuti kama ambavyo tuna Sheria ya Tume ya Mahakama, kama ambavyo tuna Sheria ya Tume ya Utumishi wa Umma. Ni wakati sasa mahsusi kwamba Tume hii iwe na Sheria yake mahsusi. Hii itasaidia kuwa na maamuzi yake. *With time* tunaweza tukabadilisha badilisha kutokana na jinsi ambavyo inaona haijafungamana na Sheria nyingine yoyote iko huru na itaweza kufanya maboresho mbalimbali kwenye Sheria yake ikiwa iko pekee yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusu Muswada wa Sheria ya Urais, Ubunge pamoja na Udiwani. Muswada huu utakuja kufuta Sheria ile ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama itakuja kupita. Mimi nipongeze sana, ni jambo jema, italeta wepesi kwa Tume ya Taifa kutekeleza sheria hii wakati wa uchaguzi kwa maana zilikuwa mbili, jambo ambalo lilikuwa ni mchanganyiko kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili sisi kama Kamati tulipokea maoni mbalimbali mengi sana. Safari hii inaonekana jambo hili limekuwa na *public interest* kwa sababu Miswada yote ikiletwa Bungeni huwa tunaita wadau wanakuja kwa uchache, lakini Miswada hii imekuwa ya tofauti sana, tumepata wadau zaidi ya 1,707. Nalipongeza sana Bunge kwa kufuata mchakato huu. Mpaka tumefikia sasa ni Bunge limetuongoza chini ya uongozi wako wewe na Mheshimiwa Spika nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili mambo mengi yamezungumzwa na wenzangu; lakini tumesikia shuhuda mbalimbali kwenye Muswada huu wa Uchaguzi wa Udiwani, Ubunge na Rais katika Ibara ya 135 suala zima la kuaibishana na kuzalilishana mambo mbalimbali ambayo ni makosa ya kisheria kwenye uchaguzi. Nafahamu suala zima la unyanyasaji wa kijinsia ni suala ambalo lina sheria yake mahsusi, pia ipo sheria nyingine, Sheria ya Rushwa, ina sheria yake mahsusi, lakini ikatumika busara ikajumuishwa kwenye Sheria za Uchaguzi. Busara hiyo hiyo itumike kujumuisha suala hili ambalo tunajua lina sheria mahsusi la unyanyasaji wa kijinsia iingie rasmi kwenye Sheria za Uchaguzi ili ifanye kuchukuliwa hatua haraka linapotokea tatizo la unyanyasaji. Kwa hiyo, tumepokea kama Kamati na tumeongeza Ibara mpya 135 kwamba hili suala liingie la unyanyasaji wa kijinsia kwa wagombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke eneo hilo niingie kwenye Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Mimi nitajikita hapo zaidi kwa sababu Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbili tofauti; Sheria ya Gharama ya

Uchaguzi ambayo ni sura ya 278 na Sheria ya Vyama vya Siasa sura ya 258.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Sheria Mama ya Vyama vya Siasa katika kifungu cha 6A, kifungu hiki kinazungumzia masharti katika muundo wa vyama vya siasa, huku ndiko kwenye *base*. Masharti haya katika kifungu cha 6A yanatoa sharti ili chama kiundwe lazima kiendane na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Tanzania – Zanzibar hilo sharti la kwanza. Sharti la pili, katika kifungu cha 6A(2), chama chochote ili kiundwe lazima kizingatie mambo mahususi, lazima kizingatie misingi ya demokrasia, kizingatie utawala bora, kizingatie masuala ya kijinsia na ujumuishwaji wa makundi maalum, hiyo ni Sheria Mama, kifungu cha 6A na 6B.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kifungu cha 10 kwenye Sheria Mama cha Sheria ya Vyama vya Siasa kinaelezea kwenye *marginal note* kwamba kinazungumzia sifa au takwa ili chama kipate usajili wa kudumu. Katika ili eneo kuna kifungu 10A kinazungumzia sifa ya Kiongozi wa Chama ili kipate usajili wa kudumu, 10B kinazungumzia masharti ya udhibiti wa chama ili kipate usajili wa kudumu. Lakini niwaambie Watanzania wenzangu na Wabunge wenzangu, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndiye muumini mkubwa, ndiye mwenye ajenda yake ya jinsia na ujumuishaji wa makundi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemsikia alisema Bungeni na mikutano mbalimbali ya kimataifa anasema hii inatokea wapi. Tumeona jinsi ambavyo yeye na Serikali yake wamekuja na kifungu kipya kinaitwa 10C hichi kinakuja kuongeza eneo linalosema ili chama kiwe na usajili wa kudumu lazima kiwe na *documents* kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *documents* hizo ziko nane; mimi nazungumzia mbili tu katika kifungu 10C kwenye hii Ibara ya 13 ambayo inaanzisha kifungu hicho 10C ambacho kinataka kila chama ili kipate usajili wa kudumu kiwe na *documents* hizo nane;

*document* namba mbili kwa hiyo inakuwa ni 10C(b) inasema ili chama kipate usajili wa kudumu ni lazima kiwe na sharti na takwa kwamba kiwe na sera. Sera ambayo itakuwa ina jumuisha masuala ya jinsia pamoja na ujumuishaji wa makundi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ni kifungu cha nane ambacho ni 10C(h) kinasema ili chama kipate usajili wa kudumu lazima kiwe na Kanuni mahsusi za ajira kwa watendaji wa chama husika. Ni jambo jema sana vifungu viko nane ndiyo maana nazungumzia viwili. Watumishi watakuwa na uhakika wa ajira zinazoeleweka kwenye vyama, watakuwa na ulinzi, watakuwa wana-*security* ya uhakika na wanaweza kudai haki zao kwa sababu ili kisajiliwe lazima kiwe na kanuni maalum.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, *Doctor* ya pili hiyo.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara zote ambazo zimeletwa kwa ajili ya kurekebisha …

**NAIBU SPIKA:** *Doctor,* hiyo kengele yako ya pili.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde kumi.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Katika Ibara zote ambazo zimeenda kurekebishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa ni Ibara moja tu, Ibara ya 13 ambayo inaonesha Kifungu (c) ndiyo ambayo imekuja na jedwali mahsusi, toka sheria iundwe ya Vyama vya Siasa hili ni jedwali la tatu kwa hiyo unaona jinsi ambavyo Serikali inajali masuala ya jinsia pamoja na umuhimu huo wa Viti Maalum, imekuja na jedwali wenzangu wasome mahsusi kwamba lazima sera hii ijumuishe masuala haya ndiyo maana

nasema Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia ndiyo muumini mkuu wa suala la jinsia na makundi maalum. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Alice.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya Mheshimiwa Dkt. Alice Ahsante sana, jedwali hilo lisambaze. Tunaendelea na Mheshimiwa Kilumbe, Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka ninaongeza dakika tano ili Mheshimiwa Kilumbe apate dakika zake Kumi. Ahsante.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia namshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya na uzima kufanya kazi ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimana hapa ikiwa leo ni siku ya sheria duniani naomba kabla sijatoa mchango wangu basi nipeleke salamu za pongezi nyingi sana kwa watumishi na viongozi wote wa Mahakama nchini kwetu kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kuwatumikia Watanzania katika Idara ya Mahakama. Kama unavyofahamu Mhimili huu wa Mahakama ni Mhimili ambao sisi tunafanya nao kazi kwa karibu kwa maana ya kwamba sisi tunatunga sheria wao wanatafsiri na kusimamia haki. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa siku hii muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa utashi na dhamira yake akisimamia zile *4Rs* leo ndiyo tunapata nafasi ya kuzungumza Miswada hii mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Waziri mwenye dhamana na Mheshimiwa Naibu wake na ofisi nzima ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya sambamba na Kamati yetu ya

Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambayo inaongozwa na Ndugu Mhagama, nawapongeza sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza mambo ya msingi sana yanayohusu mustakabari wa shughuli nzito zinazohusiana na mchakato wa kisiasa wa masuala ya Uchaguzi, Vyama vya Siasa na Tume ya Uchaguzi. Haya mengi tunayoyazungumza yanatokana na mabadiliko makubwa tuliyoyafanya mwaka 1992 kuhama kutoka kwenye mfumo wa chama kimoja na kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu niwakumbushe wenzangu kwamba tumekuwa na Viongozi Wakuu wa Nchi Mheshimiwa Mzee wetu Dkt. Ally Hassan Mwinyi ambaye ndiye alisimamia mchakato wa kuingia katika mfumo wa vyama vingi, ninampongeza Mzee wetu huyu maana alisimamia kwa busara sana mpaka tukafika hapa tulipofika. Rais wa kwanza wa mfumo huo akawa Hayati Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa akafanya kazi kubwa ya kurekebisha ili watu waliokuwa wameingia kwenye mfumo huo kwa munkari waweze kutulia, watu wengine walidiriki kumfikiria kwamba si mtu anayependa sana *democracy* lakini ni kwamba alitaka *democracy* yenye nidhamu, akaja Mheshimiwa Kikwete akafungua milango mikubwa sana ya kimedokrasia ya kuwasikiliza viongozi wa vyama vingine vya siasa hata tukafikia hatua ya kuamua kuitafuta Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini nilichotokea wote tunakifahamu kama Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaenda kwa Hayati Mheshimiwa Rais Magufuli ambaye naye alifanya kazi kubwa lakini watu wengi waliona kama ameufunga kidogo mlango wa demokrasia ya kuwasikiliza wanachama wa vyama vingine vya siasa. Amekuja Mama ameamua kuufungua mlango ule kwa kiasi kikubwa, ameufungua kwa kiasi kikubwa kwa kuwasikiliza kwa mambo mengi ntakayoyataja hapa lakini nataka niwaambie Watanzania kupitia nafasi yangu hii ambayo nachangia kwenye Bunge wala msifikiri kwamba huu utakuwa mwisho wa hizo kelele, hauwezi kuwa mwisho

wa hizo kelele, hapa tunafanya haya mambo kwanza kabisa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa dhamira ya dhati ya kusimamia 4Rs alizo-*introduce* katika Bunge letu, lakini siyo kwamba tuko hapa leo kupitisha hizi kwamba ndiyo utakuwa mwarobaini wa kuondoa kelele za watu wanaoitwa wapinzani, Hapana! Tutakuwa tumesaidia katika kuweka misingi ya *4Rs* ambazo Mheshimiwa Rais wetu amezi-*introduce*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama amechukua nafasi ya kukaa na viongozi wa vyama, kachukua nafasi ya kufuta kesi, kuwatoa wengine magerezani, kukutana na mabaraza ya vyama vya siasa, kuunda kikosi kazi ili kiweze kufanya kazi ya kuleta maoni na hayo maoni yamefanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na tunaendelea na mchakato huo mpaka leo tupo katika sehemu ya kutekeleza mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie nafasi hii ambayo vyama vya siasa vimepewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wasipoitumia vizuri watamkumbuka maishani. Watamkumbuka huyu Mama hata siku zijazo wasipoitumia vizuri kawapa nafasi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa uniruhusu kidogo nichangie katika Muswada wa Sheria wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mimi nilipata bahati kidogo ya kuhudumu siyo Mwanasheria lakini kuhudumu katika Kamati ya Bunge la Sheria Ndogo na huko tukjifunza kidogo angalau taratibu taratibu za jinsi ya kuchambua mambo haya. Kwamba leo tunazungumza Sheria ya Tume ya Uchaguzi, tunapozungumza kwanza tunaangalia tunapounda sheria ni kwamba isikinzane na Katiba, isikinzane na sheria nyingine, isikinzane na mikataba ya kimataifa tuliyoingia. Mimi ulikuwa wasiwasi wangu juu ya lile neno Tume Huru lakini bahati nzuri nikapata bahati ya kupitia Katiba Ibara ya 74(7) ambacho kinasema; "Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake yaliyoainishwa katika Ibara hii Tume ya Uchaguzi itakuwa idara huru inayojitegemea."

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposoma maneno hayo nikajiridhisha kwamba neno Tume Huru haliondoi uhalali wa Tume hii kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, hapo nikawa sina shaka na kwa maana hiyo naunga mkono hoja hii asilimia 100 ya kuiita Tume Huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ninalotaka nilizungumze hapa kuitwa Tume Huru ni kuipandisha sifa ya Tume kuileta katika jina, hili neno Tume Huru lipo katika sifa ya Tume na siyo kwamba ndiyo tutaanza kuwa na Tume Huru, Tume zote ambazo tumekuwa nazo zimekuwa Tume Huru ila jina lake halikuwa na sifa hiyo ya Tume Huru jina lake lilikuwa linaitwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tumeamua kuchukua sifa yake ya kikazi kuileta kuwa sehemu ya jina wala hakuna mgogoro wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba Tume zote ambazo zimekuwepo zimekuwa ni Tume Huru kwa sifa zake za utendaji kazi, maana asije akatokea mtu ndiyo kwanza tutapata Tume Huru ya Uchaguzi hapana ila tunaunda jina la Tume Huru ya Uchaguzi lakini Tume zote ambazo zimepita zimekuwa huru kwa utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo nataka nichangie ni Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Naungana mkono kabisa na hoja ya kuunganisha Sheria hizi mbili Sura ya 343 uchaguzi wa Rais na Wabunge na Sura ya 292 uchaguzi wa Madiwani, kwa sababu chaguzi hizi sasa zinafanyika kwa pamoja basi ziwe kwenye sheria moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika kifungu cha 6 cha Muswada ambacho kinazungumzia upatikanaji wa wasimamizi wa uchaguzi, hapa na mimi pia naunga mkono kwamba upatikanaji… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde mbili maliza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naunga mkono upatikanaji wa wasimamizi wa uchaguzi kama ulivyopendekezwa katika Muswada huu kwamba wawe ni Maafisa Waandamizi. Hapa nataka niweke wazi kwamba Afisa Mwandamizi ni sifa za mtumishi atakayekuwa kwenye Tume siyo cheo, Afisa Mwandamizi anaweza akawa yoyote, kwa hiyo hakuna walioondolewa kwamba huyu sasa hatakiwi, mwingine anasema Wakurugenzi wameondolewa hawatakiwi, akiwa ana sifa ya kuwa Afisa Mwandamizi inawezekana lakini siyo lazima. Hapa tumeweka mlango mpana hatujifungi kwa Mkurugenzi, tunataka mtu yeyote mwaminifu ili mradi awe Afisa Mwandamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Mushashu, Mheshimiwa Dkt. Ntara, Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Hasunga, na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.10 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na

**Madiwani wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tulishatoa orodha ya majina ya jioni. Tunaanza na Mheshimiwa Mushashu, jiandae Mheshimiwa Dkt. Ntara na Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama na Naibu Waziri Ummy Nderiananga, kwa kuweza kutuletea hii Miswada mitatu na kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Kamati ambayo imeshughulika katika kuchambua Miswada hii. Wamefanya kazi kubwa; wamepokea maoni, wamechambua na hatimaye wameweza kutuletea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumebahatika kuwa na Rais mpenda watu, mpenda maendeleo, ambaye anataka kukuza demokrasia. Vilevile anatutumikia Watanzania wote bila kujali itikadi zetu za kisiasa wala dini zetu. Alipoleta falsafa yake ya *4R* baadhi ya watu hawakumwelewa kwamba anazungumzia mambo ya maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na ujenzi mpya; lakini sasa wote tumeshaona kwamba mama anaishi falsafa hii kwa vitendo. Ndiyo maana amekubali Serikali yake kutekeleza maoni yaliyoletwa na

kikosi kazi, maoni yaliyoletwa na Baraza la Vyama vya Siasa, wadau wengine wa demokrasia na sasa unaona kwa kiasi kikubwa hayo mapendekezo ndiyo yameingia kwenye Miswada ya Sheria ambayo tunaijadili. Tunasema, Mama hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Bunge linajadili Miswada mitatu ambayo itakwenda kuongoza na kusimamia uchaguzi; Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa. Kikosi kazi baada ya kuteuliwa, wao walikuwa waangalie masuala ya demokrasia, lakini wakaja na mapendekezo. Pendekezo lao la kwanza ilikuwa ni Sheria ya Uchaguzi ifanyiwe mabadiliko; pendekezo lingine ni Sheria ya Vyama vya Siasa ifanyiwe mabadiliko, lakini vile vile wakapendekeza kwamba kuwe na namna ya kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye masuala ya siasa na wakasema tuweke vipengele vya kupinga ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia masuala karibu yote haya yamezingatiwa kwenye Miswada ambayo iko mbele yetu. Kweli Mama Samia ni kiongozi wa maridhiano, anakuza demokrasia, anadumisha utulivu na amani wa nchi yetu. Kwa hili, Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usawa wa kijinsia; kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Watanzania sasa tumefika takribani watu milioni 61.7 na wanawake ni asilimia 51, lakini ukienda kwenye nyanja za kisiasa, huwakuti wanawake pamoja na kwamba tuko wengi. Ukiangalia kwenye vyama vyenyewe, uongozi wa juu kwenye vyama vya siasa, wanawake ni asilimia 10.5 peke yake. Ukiwatafuta kwenye michakato ya kugombea, kuchaguliwa wanawake ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia hata humu Bungeni, mfano Wabunge ambao wamechagulia *direct* kutoka kwenye majimbo ni asilimia 10.2 tu; Madiwani wanawake waliochaguliwa kwenye kata ni asilimia 6.5; Wenyeviti wa Vitongoji wanawake

ambao wamechaguliwa moja kwa moja na wananchi ni asilimia 6.7; Wenyeviti wa Vijiji 2% tu ndio wanawake; Wenyeviti wa Mitaa ni asilimia 12.7 tu ndio wanawake. Kwa hiyo, mnaona hii haikubaliki, wanawake tuko wengi, lakini inapofika kwenye ngazi ya maamuzi, wanawake hawaonekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoweza kuchangia kimojawapo ni vyama vya siasa havipendi kuteua wanawake wagombee nafasi ya Urais, wagombee nafasi ya Ubunge, wagombee nafasi ya Udiwani wakiogopa kwamba wakimteua mwanamke kwenda kugombea, kuna uwezekano wakashindwa kwa sababu ni mwanamke, lakini wanasahau kwamba wanawake hao hao ndio wanashinda kwenye mikutano yao ya hadhara. Wanawake hao hao ndio wavaa vipeperushi, ndio waimbaji na hao ndio wapiga kura walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na visingizio kwamba wanawake wa namna hiyo ambao wanafaa kuingia kwenye nafasi za uongozi hawapo. Sasa hivi hakuna visingizio, wanawake wasomi wako wengi, wenye uzoefu wako wengi na wale wote ambao wamepata uteuzi kwenye nafasi mbalimbali, nafasi hizo wamezitendea haki. Mnamwona Mheshimiwa Rais anavyofanya kazi vizuri, ni mwanamke; mnamwona Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia anavyofanya kazi vizuri; mnawaona Mawaziri wote wanawake waliomo humu ndani wanavyofanya kazi vizuri; Mnawaona Majaji wanawake wanavyofanya kazi vizuri; Mnawaona viongozi mbalimbali wanawake wanavyofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hivyo visingizio hatukubaliani navyo, wawekewe kipengele kwenye Muswada huu, kwamba wanavyoteua wagombea kwenye vyama vyao, kila chama wanawake wasiwe chini ya asilimia 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumesaini mikataba mingi ambayo inahusiana na usawa wa kijinsia, lakini sheria hizi zimekuja kusudi kutusaidia tuweze kufikia kule. Kwa hiyo, nilikuwa naomba,

kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 66 na 78, imetamka kwamba kutakuwa na wanawake watachaguliwa na siyo chini ya asilimia 30 ya Wabunge wote, kwa hiyo, naomba hata hii Miswada itamke kwamba kwenye vyama vya siasa wale watakapogombea ni asilimia 30; itakapo kuja kwenye uongozi wa vyama vya siasa uongozi wa juu wanawake wawe sio chini ya asilimia 30. Vile vile, teuzi mbalimbali zitakazofanyika ndani ya Serikali isiwe chini ya asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoweka asilimia, kesho na keshokutwa tutajipimaje? Tunaposema kuna usawa wa kijinsia bila kusema ni asilimia ngapi, tunasema kuna ujumuishwaji wa makundi maalum, watu wenye ulemavu, vijana, wazee, tusipoweka asilimia kesho na keshokutwa tutajipimaje? Nilikuwa naomba tulione hili, tuweke asilimia kusudi iweze kutusaidia kuyafanya hayo tunayotaka kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji wa kijinsia ni tatizo kubwa, haliko Tanzania peke yake, liko kila mahali, linawaathiri wanaume na wanawake lakini wanawake wanathiriwa vikubwa kuliko wanaume. Wanaathiriwa kisaikolojia, wanaathiriwa kimwili lakini vile vile na kimahusiano. Kabla mwanamke hajagombea anaonekana ni mama safi, mwenye heshima kwenye jamii, mwache achukue *form* agombee; ooh, malaya, msagaji, shoga, mchawi, ana tako moja, ili mradi utukanwe matusi yote. Mitandao yote itakuvaa, lakini vilevile wengine wanaombwa rushwa ya ngono wakati wakitafuta kuteuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama wewe mume wako hana uvumilivu na hajazoea mambo ya siasa, utakuta mnaachana kwa sababu ya hayo maneno. Mbele ya wapigakura wakiyasikiliza yale maneno, unadhoofishwa, unakosa kujiamini na wao wanakuchukia, wanaona hutoshi, na kuna uwezekano usichaguliwe kwa sababu ya unyanyasaji wa kijinsia. Hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Miswada hii kwanza itoe tafsiri ya maana ya jinsi, maana ya jinsia, maana ya usawa wa kijinsia na maana ya ukatili wa kijinsia. Vilevile kwenye Sura ya 7 iongezwe kipengele cha 135, kikitamka kabisa kwamba unyanyasaji wa kijinsia ni kosa la kiuchaguzi na ikitokea kwamba aliyefanya unyanyasaji wa kijinsia ni mgombea, basi afutiwe dhamana ya kugombea asigombee na wale wengine watakaofanya hivyo wapewe adhabu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viti Maalum viko kwenye nchi nyingi, wengine wanaweka kwenye Sheria za Uchaguzi, wengine wanaweka kwenye Katiba, wengine wanatoa *quarters* na Tanzania tuna utaratibu, lakini bila viti maalum hapa Wabunge wangekuwa asilimia 10.2, lakini kwa sababu ya Viti Maalum sasa hivi tuko asilimia 37 kwa mujibu wa Ibara ya 66 na 78.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nasema, maana yake kwenye hii sheria nairudia, naona haijatamka. Kama sheria mama ambayo ni Katiba imetamka, kwa nini na hapa tusitamke hizo asilimia 30?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, watu wenye ulemavu na hasa ambao wana matatizo ya macho, unakuta kwamba wakati wa uchaguzi…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Benardeta muda wako umekwisha.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba tumuunge mama mkono, tupitishe hii Miswada ili iweze kutusaidia kutatua matatizo yaliyopo kwenye chaguzi mbalimbali, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunachangia dakika kumi/kumi. Wachangiaji wako wengi, wengine wakikosa, watachangia kesho. Tunakwenda kwa Mheshimiwa Dkt. Ntara, haya na wewe *gender. (Kicheko)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Naibu wake pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa kuchakata maoni. Najua ni kazi kubwa wameifanya hata kabla ya kuja kusoma. Nafikiri hata uzito umepungua kwao. Hongereni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye eneo la Tume. Suala la uwiano kwenye Tume ni muhimu. Maana yake sasa tunataka kuleta usawa wa jinsia, basi wale Wajumbe wa Tume tuhakikishe kwamba kuna uwiano kati ya KE na ME.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda nione kwamba wale watakaosaili wajumbe, pia ndani ya wale wanaosaili ambao ndio wamekaa pale kama walimu au viranja, kuwe na mchanganyiko wa wanawake na wanaume. Hata hivyo, naomba ile Tume, yale majina yanayopendekezwa kwa Mheshimiwa Rais kupata Mkurugenzi na Msaidizi wake, hata ndani ya yale majina kuwe na KE na ME ili Mheshimiwa Rais aangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumekuwa na Wakurugenzi wanaume. Mheshimiwa Rais aweze kuona kumbe hata huyu mwanamke anaweza kuwa Mkurugenzi. Kwa hiyo, pale wahakikishe yale majina wanayopelekwa yawe na mwanamke ili yaingie kwenye kundi la maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi katika haya mambo ya uchaguzi au mambo ya uteuzi, kukiwa na watu wanaotoa maamuzi, tukiwa na wanawake wako pale juu, basi tutaweza kupata idadi nzuri ya wanawake katika sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, hiyo tunayosema *fifty/fifty* inaweza ikafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona katika wakati ujao kwamba hata tunaweza tukapata Waziri Mkuu mwanamke ili tuanze kuona mabadiliko. Kwa sababu Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwanamke ameshaonesha kwamba yeye ni moto moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Uchaguzi huu unasimamiwa na kanuni. Kanuni hizo hazitungwi hapa Bungeni, bali zinatungwa na Waziri wa TAMISEMI kwa utaratibu uliopo. Sasa haya tunayojadili hapa, tunaomba yakatumike kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili huyu Waziri akitunga kanuni, basi aangalie na haya maboresho yaliyowekwa wakati tunajadili humu ndani ili ikiwezekana masuala yote ya ukatili wa kijinsia na uchafu mwingine wote uweze kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, akiziweka kanuni zake vizuri, basi tunaweza tukabadilisha hata uchaguzi mwingine ndani ya Serikali za Mitaa. Mfano, leo Diwani wa Viti Maalum hawezi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri. Sasa unashangaa, kwani huyo Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ni mwanaume, ana tofauti gani na akichaguliwa Diwani wa Viti Maalum kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, wana utofauti gani yule wa Kata na huyu wa Viti Maalum? Wakati mwingine ukiangalia, unasema eh, mbona afadhali angekuwa yule wa Viti Maalum? Hilo lifanyike ili tuweze kuona kwamba kumbe hata Diwani wa Viti Maalum anaweza akawa Mwenyekiti wa Halmashauri. Sio Viti Maalum wao eti wanapewa kuwa wasaidizi, Naibu au Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Kwa nini mwanaume asiwe Makamu halafu wa Viti Maalum awe ndiye Mwenyekiti wa Halmashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna wakati diwani mwanaume aliteuliwa. Kwa hiyo, akiteuliwa huyo ni Viti Maalum, alipoteuliwa akapata kuwa Meya wa Jiji. Sasa kwa nini huko Diwani wa Viti Maalum asiwe Mwenyekiti wa Halmashauri? Haya ni mageuzi ambayo Waziri wa TAMISEMI anaweza akayafanya kwenye kanuni

zake ili yaendane na haya tunayoyajadili leo kwenye Miswada hii iliyoletwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye ukatili wa kijinsia. Nawapongeza sana wanaume waliozungumza kwa hisia kwenye ukatili wa kijinsia na hasa Mheshimiwa Edwin Swalle. Nami niende kwao, huu ukatili wa kijinsia uko pande zote. Wanaume wakati mwingine hawasemi, lakini hata wao wanyanyasika sana. Mtu anaenda kugombea Ubunge, Udiwani anaambiwa huyo! Kama walivyosema wenzangu; mbona huyo ni shoga! Sisi hapa hatuji kufanya kazi za mashoga, sisi tunakuja hapa kufanya kazi za kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta mtu anasimama pale anasema, yule ana mkono wa sweta. Uliuonaje? Kwa hiyo, kuna vitu wananyanyasika. Mara wanasema, huyo hana nyumba. Sasa si mngempa huo Ubunge au Udiwani ili apate pesa akajenge hizo nyumba! Wakati mwingine mtu anaambiwa sijui sungura karuka; huyu sijui bisholole; yaani kuna vitu wanaume wananyanyasika hawasemi. Huyu anajifanya hapa mwanaume anaomba kura, huyo anapigwa na mkewe. Mtu akipigwa na mkewe si ni sawa tu, kwa sababu wakati mwingine labda anamrekebisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wao wana mengi wameshasemwa sana, wamenyanyasika sana. Kwa hiyo, niseme, unyanyasaji huu uwekwe, hizi tabia mbaya, hasa kama ni Mbunge au ni mtu anayegombea, Ubunge wake ufutwe, hiyo ndiyo iwe adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapambe ndiyo nuksi, hao wapambe nao ikiwezekana wapelekwe wakafungwe huko, hakuna faini. Hata wakifungwa miezi sita, inawatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwenye ukatili wa kijinsia; leo niwaambie Wabunge wenzangu mlielewe hivi, ukatili huu wa kijinsia inapokuja kwenye uchaguzi, upo kwenye vyuo vyetu. Vijana

wetu wa vyuo vyetu vya kati na vyuo vikuu wakitaka kuingia kwenye chaguzi hizi za vyama wanapata shida sana. Lazima wagawe ngono, wote vijana wa kiume na wa kike, yaani unakuta vijana wa kike ni lazima aende kwenye mahusiano bila kupenda na viongozi. Kwa hiyo, unakuta vijana katika vyuo wameathirika sana na hili jambo la kufanyiwa ukatili ili tu awe kwenye Kamati fulani ya chama au awe kiongozi wa chama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavulana wengi sasa hivi tunalalamika wakati mwingine tunasema sasa hivi wamekuwa mashoga. Lakini tuangalie kwenye vyama, baadhi wanawatumia hao vijana, wanatumia miili yao halafu hao vijana baadaye ndiyo wanaendelea sasa wanazoea na wanakuwa mashoga ni kwa sababu tu alitaka uongozi katika chama akiwa chuo au akiwa kwenye hivi vyuo vya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi Sheria zikiwekwa vizuri hata huyu msichana au mvulana akifanyiwa jambo baya anaweza baadaye akachukua hatua. Lakini sasa hivi akifanyiwa hivyo atakwnda kushtaki wapi? Lakini kama amefanyiwa hivyo ili tu aingie kwenye Kamati ndani ya vyama, basi huyu anaweza akachukua hatua ya kushtaki, na kwa sababu liko kisheria, basi angalau vijana wetu wataweza kuishi na wao na kwenda kwenye njia yao ambayo waliitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, alisema sana hapa Mheshimiwa Katimba, kwamba tunavunja moyo wa vijana na tunawafanya wasiende mbele kwa sababu tunawakatisha tamaa. Unamuomba mtoto ngono ili tu umchague kwenye Kamati ya Chama. Tuwaache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijana wengi bila aibu nasema wameathirika sana, wamefanyiwa hivyo vitendo na sisi ambao ni viongozi. Hebu tuangalie, nimesema vyama vyote wana huo mchezo. Tuwasaidie hao watoto ili wapambane na wao ili waweze

kupata stahili zao sehemu ambazo wanatakiwa kwenda. Baada ya kusema hayo nikushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, Jiandae Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa hii. Nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia fursa hii ili nitoe mchango kwenye mjadala huu wa marekebisho ya Sheria hizi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Jenista na wasaidizi wake wote. Vilevile bila kusahau Kamati husika kwa sababu kazi kubwa sana imefanyika mpaka hapa tulipofika leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni nchi ya kidemokrasia. Pia tokea mwaka 1992 tuliridhia mfumo wa vyama vingi. Tokea mwaka huo kumekuwa na chaguzi nyingi takribani sita ambazo zimehusisha vyma mbalimbali vya kisiasa ili kuweza kupata viongozi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kadhaa lakini nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujasiri mkubwa ambao ameuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu huko nyuma tulikuwa na Tume ya Uchaguzi ilikuwa inalalamikiwa ingawa siamini kama haikuwa huru lakini bado hatukuwa na mtu ambaye aliweza kuonesha ujasiri kama aliouonesha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuleta muswada wa marekebisho ya Sheria hii ili tuweze kuipitia na kuifanyia marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 Ibara ya 118(e), inaelekeza Serikali kuweka mazingira wezeshi ya haki kwa wananchi

kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni moja kati ya maelekezo ili tuweze sasa kuhakikisha kwamba, mifumo yote ya kidemokrasia inakuwa wazi ili watu washiriki shughuli za kisiasa katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia, ameonesha nia thabiti ya kufanya marekebisho, kufanya maboresho kupitia zile *R* nne alizozisema wakati anashika hatamu za uongozi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22 Aprili, 2021 Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Bunge hapa alijenga msingi wa demokrasia pale aliposema dhamira yake ni kukutana na viongozi wa vyama vya siasa ili kuhakikisha kwamba, sasa tunafanya siasa za maridhiano katika nchi yetu ili kwa pamoja tushiriki kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yote haya yasingewezekana kama Mheshimiwa Rais asingekuwa na utashi, muungwana lakini kama Mheshimiwa Rais asingekuwa na dhamira ya kweli ya kuleta maridhiano na kufanya demokrasia itamalaki na wananchi wote kwenye Taifa hili tuweze kushiriki kwenye shugfhuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua zake hizo ndiyo maana uliona viongozi wa vyama vya siasa waliokuwa na kesi zilizokuwa zinahusu mambo ya siasa waliachiwa huru, mikutano ya hadhara iliruhusiwa, maandamano yaliruhusiwa mpaka juzi baadhi wameandamana na bado wakapewa *facilities* zote kuhakikisha kwamba wanashiriki maandamano yale bila shida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utaelekea kwenye eneo moja. Nilikuwa ninapitia Taarifa ya Kamati na katika taarifa ile imeonesha sehemu kubwa ya maoni yaliyotolewa na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni yale, sehemu kubwa ilikuwa ni hofu ya watu wengi juu ya namna Tume ya Uchaguzi ilivyo

huru. Tokea tulivyopata uhuru tumekuwa na tume ya Uchaguzi. Ukiangalia Katiba yetu Ibara ya 74(1) inaonesha muundo wa Tume ile. Hata hivyo, Ibara ndogo ya (7) na Ibara ndogo ya (11) inaelezea namna gani Tume hii inafanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa na chombo chohote, chama chochote na bila kuingiliwa na mtu yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwangu mimi tokea tumepata uhuru mpaka tumekuja leo hii, tuna Tume Huru ya Uchaguzi. Pia, ndiyo maana kupitia Tume hii tokea mwaka 1992 baada ya mfumo wa vyama vingi, tokea mwaka 1995 wakati vyama vingi vimeshiriki uchaguzi, tumeshiriki chaguzi sita. Bunge hili limekuwa linapata Wabunge kutoka Vyama vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kuwa Mbunge kupitia Chama cha Upinzani, nilitangazwa na Tume hiyo hiyo ya uchaguzi. Kwa hiyo, tumekuwa na Tume huru ya Uchaguzi ndiyo maana kwangu mimi leo hii siwezi kusema kwamba tunatengeneza Tume huru ya Uchagzi. Ila, tunatengeneza Tume huru ya maridhiano kwa sababu Tume huru tumekuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Kamati vilevile niipongeze Serikali, pamoja na malalamiko haya yaliyokuja kwenye Kamati kupitia kwa wadau mbalimbali, Serikali imesikiliza maoni hayo. Pia kupitia Kamati bado kuna marekebisho yamefanyika ili kuweza kudhihirisha ile dhamira ya Mheshimiwa Rais ya Ustahimilivu vilevile kutengeneza mazingira salama, mazingira huru ili kuthibitisha kwamba, kweli ile Tume huru ambayo imekuwa inaombwa muda wote, basi inakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nithibitishe kwamba, kwa mabadiliko haya leo hii Tume hii ni Tume huru ya uchaguzi. Pamoja na kwamba bado kuna watu wanaona kwamba siyo huru, sijui.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia kwa vigezo vya kimataifa, imekuwa inasadikika kwamba ili Tume iwe huru basi iwe

na chanzo chake cha fedha, isigharamiwe na vyama vya siasa, isigharamiwe na namna yoyote au upande wowote ambao unashiriki kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Muswada huu wa Sheria, ukiangalia Ibara ya 22 na Ibara ya 24 inaonesha kwamba Tume hii huru ya Uchaguzi itagharamiwa kutoka mfuko Mkuu wa Serikali. Vilevile, ukiangalia namna viongozi na wajumbe wa Tume hii wanavyopatikana, Ibara ya 9(1) inaonesha namna gani wajumbe kupitia Kamati ya Usaili wajumbe wa Tume hii watapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba, Tume ya usaili itapendekeza wajumbe watano *plus* wanne ili Mheshimiwa Rais sasa apate fursa ya kupata wajumbe watano watakaoungana na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ambao wanapatikana ukiangalia Ibara ya 7(1) inaonesha namna gani Tume hii inakuwa huru. Ukizingatia kwamba viongozi wa Tume hii Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wanakuwa ni majaji wa Mahakama kuu au Mahakama ya Rufaa. Hakuna namna ya ku-*question* uadilifu, umakini na ubora wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia marekebisho haya naomba niwathibishie wananchi kwamba, kwa sababu Chama cha Mapinduzi ni chama kiongozi na kwa sababu dhamira njema ya Mheshimiwa Rais, ndiyo maana marekebisho haya yamekuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelekezo ya Timu ile ya majadiliano, sasa tunatengeneza Tume huru ya Uchaguzi, tunafanya marekebisho ya Sheria hii ya Tume ya Uchaguzi ili sasa kuridhia na kuendana na yale ambayo Mheshimiwa Rais aliyaeleza lakini na matakwa ya wananchi kupitia wawakilishi kwenye vyama mbalimbali kwamba, tuwe na Tume huru na waridhike kwamba tutashiriki uchaguzi tukiwa kwenye *fair ground*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache nishukuru, lakini niombe wananchi waone dhamira njema ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba Taifa hili linakuwa moja, linajengwa katika msingi hii ya usawa ili mwisho wa siku sisi sote kama jamii tuweze kushiriki kwenye maendeleo ya Taifa hili. Nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Mheshimiwa Hasunga, jiandae Mheshimiwa Kamani.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili niweze kuungana na wenzangu katika kuchangia Miswada hii mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuitayarisha hii Miswada na kuileta katika Bunge letu hili tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miswada mitatu imeletwa kwa pamoja ambapo muswada wa kwanza ni wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ambapo unaunganishwa Sheria hizi mbili. Vilevile, Muswada wa pili ni wa Sheria ya Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi na Muswada wa tatu ni wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kutaka kukuza demokrasia nchini. Pia, unapoikuza demokrasia nchini maana yake unataka kuleta maendeleo ya kweli nchini. Kwa hiyo, ili uweze kuleta maendeleo lazima uzungumzie demokrasia. Vilevile, viongozi wengi duniani ambao wameweza kuleta maendeleo makubwa ni wachache sana ambao tumeweza kuwaona hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi hawa ambao huwa wana maono mapana, ni wazalendo kwenye nchi zao, ni wachapakazi, huwa wanataka kila mmoja katika nchi ashiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo. Viongozi wa namna hiyo, wanapinga ubaguzi wa kikabila, ubaguzi wa kidini, ubaguzi wa kiukanda, ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lee Kuan Yew alipokuwa anaanza kuiongoza Singapore na alipoipigania mpaka ikapata uhuru, Lee Kuan Yew moja ya hatua alizozichukua ni kujenga Taifa moja. Vilevile, katika kujenga Taifa moja alikuja na mambo kama sita hivi ambayo alisema ili tulijenge Taifa letu liweze kuwa na maendeleo makubwa, tuwe na mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyasema ila sitayasema kwa sababu ya muda wangu ni mfupi. Ukiangalia Singapore yule Rais ambaye alikuwa ni Waziri Mkuu wao wanatumia Waziri Mkuu, aliweza kuikokota Singapore kutoka nchi masikini duniani hadi kufikia nchi iliyoendelea duniani. Sasa hivi ni nchi ya tatu karibu ya nne kiuchumi duniani. Sasa ni kwa sababu ya kazi kubwa waliyoifanya katika kuijenga hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwetu tumepata viongozi wengi. Tunamuona Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais ambaye ukimuona kwa kumuangalia ana nia njema ya kuleta maendeleo kwa Watanzania wote. Hilo lote linajidhihirisha kwa kuona alivyokuja na mambo manne aliyoyazungumzia kwenye *4R. Reconciliation* (maridhiano), *Resilience* (ustahimilivu), *Reform* (mabadiliko) lakini *Rebuild* (kujenga upya). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiyatafakari yote haya kwa mapana ukaona ni nini hasa mpaka Rais anataka kukifanya, utaona kwamba Rais ni moja ya viongozi wakubwa na mashuhuli hapa duniani kwa hayo maono. Kwa sababu, anaonesha umahili na ushupavu lakini anaonesha uzalendo wa hali ya juu na ni mchapakazi, vilevile anataka kukuza demokrasia hapa nchini;

demokrasia ya kweli ambayo watu wote washiriki kwenye hilo, lakini anataka maendeleo mazuri ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanajidhihirisha katika hotuba aliyoitoa 22 Aprili, 2021alipolihutubia Bunge. Moja, ya mambo aliyoyaeleza kwenye Bunge hili alisema, yeye atahakikisha kwamba analinda na kuzilinda tunu za Taifa letu ambazo alisema ni amani, umoja na mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa amani, umoja na mshikamano ndiyo nguzo muhimu ya maendeleo ya nchi yetu. Na haya alianza kuyatekeleza. Kwa kuangalia tu tunaweza kuyaona kwa matendo kwa mambo haya aliyoyafanya: -

(i) Aliamua kukutana na viongozi wa makundi mbalimbali. Viongozi wa Vyama vya siasa, viuongozi wa dini, viongozi wastaafu wote akakaa nao na kuzungumza ni namna gani tunaweza kujenga Nchi ya Tanzania imara ambayo itaendelea kuwa na uchumi mzuri ule ambao utakuwa daraja la pili; *(Makofi)*

(ii) Akafanya mikutano ya baraza la vyama vya siasa. Katika kipindi chake cha miaka mitatu amefanya mitatu;

(iii) Akaruhusu mikutano ya hadhara kwamba, yeyote anyetaka kusema tuwape nafasi waseme yale wanayotaka kutuambia ni yapi tuwasikilize. Akaruhusu;

(iv) Akaunda kikosi kazi kwa ajili ya kupata maoni ya wadau mbalimbali. Nini kifanyike katika nchi hii?;

(v) Ameleta hizi Sheria tatu ambazo ni muhimu sana katika kukuza demokrasia;

(vi) Mwisho, amefuta kesi mbalimbali ambazo aliona hazijengi utaifa, hazileti umoja, hazileti mshikamano kwenye Taifa. Ameziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya yamefanyika na amefanya mengi. Huyu Mheshimiwa Rais, sisi kazi yetu kama Bunge ni kumuunga mkono kwa kuzipitisha hizi Sheria ili tutengeneze ukurasa mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo, nataka nichangie sehemu moja hii ya Tume huru ya Taifa ya Uchaguzi ambayo inazungumzwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume huru, mimi ni mhasibu, sisi wahasibu tunasema mhasibu au mkaguzi wa hesabu anatakiuwa siyo tu aonekane kwenye macho ya watu kwamba yuko huru lakini pia na matendo yake. Hii inajidhihirisha. Tunasema tulikuwa na Tume iliyofanya kazi nzuri, ilikuwa huru na tulikuwa hatuna shida kabisa ilikuwa nzuri. Lakini sasa tunaiimarisha zaidi inakuwa na uhuru zaidi na haya tunaweza tukayaona kwa mambo yafuatayo: -

(i) Kwa namna tunavyokwenda kupata viongozi ni tofauti na ilivyokuwa huko nyuma. Wale viongozi kuanzia Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe watano, wanavyokwenda kupatikana sivyo ilivyokuwa. Kwa Katiba, Rais alikuwa anateua lakini sasa hivi tunaweka utaratibu mpya ambao unawekwa kisheria namna ya kuwapata. Hiyo inadhihirisha uhuru ambao tunauzungumzia wa hii Tume ya Taifa ya Uchaguzi;

(ii) Tunaliangalia namna ya ugharamiaji wa fedha za uchaguzi zitakavyopatikana. Zitatoka wapi? Na hapo ukiangalia kwenye Sheria, wameweka hizi zitatoka kwenye mfuko mkuu wa Hazina. Maana yake tume-*re-*

*fence* (tumelinda). Kwa hiyo, Tume ina uhakika wa vyanzo mapato; *(Makofi)*

(iii) Tunaangalia namna watumishi watakavyopatikana;

(iv) Tunaangalia je kuna Sheria? Tulikuwa na Katiba na tulikuwa hatuna Sheria. Sasa hii ndiyo Sheria ya kwanza ambayo inakuja kuonesha sasa uhuru unavyokwenda kutekelezwa. Sheria inakuwepo, kutakuwa na Kanuni na miongozo mbalimbali itakayotuongoza, lakini na mambo mengine mengi na tatu, la nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na mambo mengine mengi na tatu, la nne na la tano ni Muundo wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Tume sasa umenadikwa humu tutakuwa na muundo, muundo wake umeandikwa; lakini la sita tunataka uhakika wa wale viongozi wanaopatikana watakaa muda gani? Wanalindwaje kisheria? Ili kusudi wanapofanya hayo mambo yao wanapotekeleza majukumu yao watekeleze kwa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Ibara ya sita inayozungumzia hilo Ibara ya 6(1) ya kwanza ya muswada inasema hivi; 6.-(1) Tume itakuwa ni chombo huru na kinachojitegemea na maamuzi yake hayataingiliwa na chombo chochote au kulazimika kufuata maagizo ya mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni msingi wa kuonyesha uhuru wa Tume. Tume itakuwa huru itafanya mambo yake haitaingiliwa, ni chombo ambacho kitaaamua na kupanga mambo yake, ukiendelea pale wanasema; "Tume itakuwa ni chombo chenye uwezo wa kumiliki mali na mambo mengine" inazungumzia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukienda kwenye sifa za wajumbe wanasema hivi Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, zimeisha?

**NAIBU SPIKA:** Ndio zimeisha dakika kumi.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde kumi malizia

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilijua itakuwa dakika 15 kumbe ni kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yapo mambo mengi ambayo yamezungumzwa, lakini moja la msingi ambalo limetolewa sasa hivi kwenye hizi sheria na ambalo ndio litatunufaisha sana ni kwamba sasa hakuna mgombea kupita bila kupingwa, wagombea wote wanakwenda kupigiwa kura. Hata kama uko peke yako utapigiwa kura ya ndiyo au kura ya Hapana. Huku ni kupanuka kwa demokrasia hapa nchini, na hii ndiyo misingi itakayowawezesha wananchi wachague viongozi wanaowataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ng'wasi, ajiandae Mheshimiwa Amar, ajiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia kwenye Miswada hii mitatu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuanza mchango wangu kwa kumnukuu Mwalimu Nyerere kwenye kitabu chake cha Wosia wa Mwalimu Nyerere kwa CCM kilichotolewa mwaka 1991, alisema; "kwa kweli sifa moja ya demokrasia ya kweli ni kwamba inawapa wachache nafasi ya kisheria ya kujaribu kuwashawishi walio wengi waone ubora wa maoni yao. Hii ndiyo njia pekee ya kuleta mawazo mapya na tabia mpya katika jamii kwa amani na utulivu."

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kunukuu hii kwa sababu, wakati Dkt. Samia Suluhu Hassan anakuja kuhutubia Bunge hili kwa mara ya kwanza alisema; "Serikali kwa wakati wote itakuwa tayari kupokea na kusikiliza maoni ya kila mtu mwenye nia njema na nchi hii ya Tanzania."

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kusema kwamba muungwana ni vitendo. Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa ni mtu msikivu wakati wote amesikiliza makundi ya walio wachache, kawapa nguvu ya kuleta hoja zao ili watushawishi sisi tulio wengi tukubaliane na hoja zao. Na kama maneno ya Baba wa Taifa alivyosema hiyo ndio demokrasia ya Kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulianzishwa mchakato, mchakato ambao makundi karibu yote ya kijamii yalishiriki na katika hili mimi niwapongeze sana viongozi wetu wa dini, niwapongeze sana vyama na taasisi mbalimbali za kiraia, nivipongeze sana vyama vyote vya siasa na wananchi mbalimbali walioweza kutoa maoni na hatimaye maoni 83 yakapatikana, Serikali ikachukua maoni 64, maoni ambayo kati ya maoni hayo Sheria hizi tatu ndizo tunazipata ziko hapa mbele yetu. Lakini hata yale maoni mengine yameshatimilizwa kwa asilimia 77 mpaka sasa tunavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni 12 yanafanyiwa kazi na imeonekana yanaweza kufantiwa kazi kwa muda mfupi, na maoni saba yanafanyiwa kazi lakini kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni mtu mwanademokrasia wa kweli kuliko Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nasema hivi kwa sababu katika hizi Sheria tatu nikianza na hii Sheria ya Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nchi hii ianze uchaguzi mfumo wa vyama vingi tumeshafanya chaguzi sita; na chaguzi zote hizo tumefanya kwa kutumia Katiba yetu; kwa sababu Tume imeanzishwa kikatiba lakini hakukuwa na sheria nyingine ambayo inai-*guide* Tume. Leo hii chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan tumepata sheria hii ya Tume na wote waliokuwa wanataka tume huru; kwa misingi ya kimataifa tume huru inapimwa kwa vitu vitatu; cha kwanza ni muundo wa Tume hiyo. Muundo uko hapa kwenye Sheria na unaonesha ni namna gani wajumbe watapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninasema Dkt. Samia Suluhu Hassan ni binadamu na nusu kuliko wengi wetu. Ameleta sheria hii ambayo imemfanya ajipunguzie madaraka yake aliyopewa kikatiba, akaamua kuyaweka kwa Kamati ya Usaili kufanya usaili na kuleta majina ya watu ambao anaweza kuteua kati yao kuwa wajumbe wa Tume. Na ameleta hii katika wakati ambao wote tunajua 2025 yeye ndiye mgombea wa Urais. Je, ni nani anayeweza kujipunguzia madaraka ya ku-*control* Tume ambayo inaweza ikamsaidia katika wakati ambao yeye yuko kikaangoni? Hakuna, huo ndio ukweli, na hii ni demokrasia ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala zima la fedha na bajeti. Wote tunafahamu; kuna msemo unasema anayemlipa mcheza ngoma ndio anayechagua wimbo wa kupigwa lakini Dkt. Samia Suluhu Hassan amejiondolea na yeye nafasi ya kusema ana uwezo wa ku-*control* bajeti za Tume hii. kuanzia sasa kwa Sheria hii ambayo tunakwenda kuipitisha fedha zote za Tume kwa matumizi ya kawaida zitapitishwa na Bunge hili, lakini katika kipindi cha uchaguzi fedha zitatoka moja kwa moja Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie tu, Tume hii nayo itakaguliwa na *CAG* kama zinavyokaguliwa taasisi nyingine na taarifa yake ya kila mwaka ya utendaji kazi na matumizi ya fedha itakuwa inaletwa na Waziri husika hapa Bungeni kujadiliwa kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonyesha ni namna gani matumizi ya fedha ya Tume hii itakuwa huru na Tume inaweza ikajifanyia kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kitu kingine ni katika namna ya ufanyaji wa maamuzi wa Tume. Tume hii kulingana na Muswada huu itakuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yake bila kuingiliwa na chombo kingine chochote. Mara nyingi kinachofanya taasisi yoyote ishindwe kufanya maamuzi ni pale ambapo taasisi hii au wajumbe wa taasisi hii hawajui ni muda gani wanakaa kwenye ofisi zao. Sasa hivi kwa sababu ya Muswada huu wajumbe wa Tume wanajua watakaa kwa miaka mitano, *unless* ionekane hapa katikati wameshindwa kutimiza majukumu yao kulingana na Muswada na sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali, na kwa Muswada huu nampongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan lakini ninakipongeza chama changu kwa kuendelea kuhakikisha kwamba demokrasia ya kweli inapatikana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria yetu ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; Sheria hii imeweza kusikiliza sauti ya walio wachache ambao waliweza kutu-*convince* kwa hoja. Kwamba suala zima la mgombea ambaye anapita bila kupingwa wanaliona si sahihi. Suala hili limekuwa *addressed* vizuri kwenye Sheria, sasa hivi hakuna mgombea ambaye atapita bila kupingwa; lazima wananchi washiriki kwenye maamuzi ya nani atakayewaongoza hata kama ni kwa kura ya ndiyo au hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa, mimi niipongeze sana Serikali, Mheshimiwa Jenista na wasaidizi wako wote kwa sababu mmeona haja ya Msajili wa Vyama vya Siasa kusimamia vyama vya siasa viweze kuwa na sera ya ujumuishi wa makundi yote maalum kwenye jamii. Makundi ya wanawake vijana na watu wenye ulemavu. Na katika haya mimi naomba nishauri vitu vichache; la kwanza nilikuwa nataka kushauri juu ya Ibara ya 51 na Ibara ya 53 ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara hizi zinaongelea kwamba mtu yeyote atakayetaka kuteuliwa kuwa Diwani au Mbunge akienda kupeleka fomu yake ataenda kupeleka ikiwa na dhamana ya kiasi cha fedha ambacho kitaamuliwa kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba na ninaipendekezea Serikali Ibara hizi ikiwezekana ziondolewe kwenye Miswada hii kwa sababu zifuatazo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, haki ya kuchagua na kuchaguliwa ni haki za kiraia ambazo zimetolewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na vigezo vyote vya mtu kuchaguliwa kuwa Diwani au Mbunge viko kwenye Katiba na pia viko kwenye Sheria ya Serikali za Mitaa ambazo Uchaguzi wa Madiwani unafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza kuongeza kigezo cha fedha kwamba mtu akienda kukusanya fomu yake ya uteuzi akusanye na kiasi cha fedha mimi nina mashaka kwamba kuna baadhi ya watu hasa walio katika makundi maalum tutawaondoa katika mchakato huu wa kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwakilishi wa vijana na tunatambua changamoto mojawapo ya vijana ni hali za kiuchumi, leo hii tunawahubiria vijana wengi wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa ili washiriki kwenye meza za maamuzi hasa zile

ambazo zinahusiana na masuala yao. Tukiweka kigezo hiki cha kukusanya fomu pamoja na viasi vya fedha kama dhamana tutawaengua vijana wengi sana kwenye mchakato huu wa kuweza kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili; sensa iliyofanyika mwaka 2022 imeonesha kwamba idadi kubwa ya Watanzania ni vijana; na ninaamini kwamba mipango yote na bajeti zote zinazopitishwa kwenye Bunge hili waathirika wakubwa ni vijana kwa sababu ndio walio wengi kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza pia ikiwezekana Sheria hii ya Vyama vya Siasa imwelekeza Msajili kuja na mikakati ya moja kwa moja ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na sera kwenye vyama vya siasa zinazoongeza ushiriki wa vijana kwenye uongozi kwa kuzingatia uwingi wa kundi hili kwenye jamii zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi hili linaathiriwa moja kwa moja na maamuzi yota yanayofanywa na uongozi kuanzia ngazi za juu mpaka ngazi za halmashauri zetu mpaka ngazi za Serikali za Mitaa. Kwa hiyo tukiwa na mkakati wa moja kwa moja unaolazimisha vyama vya siasa kuwa na mkakati wa kuongeza ushiriki wa vijana kwenye uongozi ninaamini tutakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye suala zima la ukatili wa kijinsia, kwanza niipongeze Serikali kwa sababu Miswada hii tunaamini hasa kwenye ule ambao unaongeza ujumuishi wa makundi yote basi kundi la wanawake limeonwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaahidi Watanzania wakati wanatupa ridhaa ya kuwaongoza kwenye uchaguzi wa mwaka 2020 kwamba tutaongeza ushiriki wa wanawake kwenye uongozi na kufikia 50/50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walipoturuhusu walituruhusu pia kuongeza kwa hiyo nikuombe tu Mheshimiwa Jenista unapokuwa unatuletea majibu ya kuongeza ushiriki huu ujue kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo wananchi waliikubalia kuwaongoza inakwenda sambamba kabisa na hiki tunachokifanya lakini mwisho…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante muda wako umekwisha

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar, ajiandae Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili tukufu ili na mimi niweze kuchangia angalau machache kidogo. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo mengi ambayo anayafanya ikiwemo huu utashi wa kisiasa wa kuweka mambo yawe vizuri. Mama kwa kweli anaifanya kazi vizuri na anataka amani na utulivu uendelee kutawala katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Mama ameweza kurekebisha baadhi ya mambo ambayo yaliwafanya wenzetu waweze kuona sasa kwamba hii si nchi ya amani wakaamua kukimbia kwenda nje, lakini Mama akakaa nao akasema rudini ili muweze kuja kuifanya kazi ya siasa, hatuna ugomvi tena, hii kazi kaifanya Mama. Si hilo tu, Mama ameweza kuruhusu mambo mengi ikiwemo mikutano ya hadhara na hata maandamano, kama mlivyoona juzi, maandamano salama salmini

kabisa. Mama lengo lake kwamba siasa iendelee kukaa vizuri pawepo na maridhiano ili nchi iweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama pamoja na Naibu wake Ummy Nderiananga na Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya Wizara. Ukweli ni kwamba wametoa ushirikiano mkubwa sana kwenye Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria. Hili jambo limewekwa na limefikia pazuri kwa ajili ya ushirikiano wao walipokuwa wakihudhuria na kuja kukaa kubadilishana mawazo na hii Kamati ya Utawala Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Spika ambaye hayupo lakini naamini ataiskia *clip* hii. Ninampongeza sana mimi binafsi pamoja na familia yangu kwa kuniteua kuwa kwenye Kamati hii ya Utawala Katiba na Sheria. Nimeweza kujifunza vitu vingi sana; ukweli sasa hivi nina faraja kubwa. Ninaomba Mwenyezi Mungu akinijalia 2025 nikirudi basi anirudishe tena kwenye Kamati hiyo ili niendelee kujifunza zaidi kwenye masuala ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea hii ama kuridhia kuja kuichakata hii Miswada mitatu. Mheshimiwa Rais ameridhia kuileta hii miswada mitatu ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani kwa mwaka 2023, Muswada wa Sheria ya Vyama vya Siasa wa mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Spika kwa kutoa kibali cha kuwaruhusu wadau kuja kukutana na Kamati ya Utawala na Katiba. Kwa kweli tuliweza kupokea wadau wengi sana, zaidi ya 1,700, na tuliweza kuyapokea maoni yao na kuyachakata. Tumeweza kupokea maoni zaidi ya 84 na zaidi ya 60 tumeyaandaa vizuri kama vile tunavyoendelea kuyachangia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshauri mambo mengi, na mimi nichangie mambo kama matatu. La kwanza, katika eneo la Ibara ya 20 na 21 kuhusu suala la ada kwa ajili ya kubadilisha kitambulisho ama kuomba kitambulisho kingine kipya; hili suala kwa kweli lilikuwa haliko sawa. Suala hili Serikali imeweza kulipokea kwamba hili halikukaa vizuri kwa sababu wananchi wetu hawana uwezo na wengi watakosa nafasi ama watakosa haki ya kupiga kura. Naishukuru Serikali imeweza kulichukua hilo namimi nasema *big up* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeshauri pia jambo moja la unyanyasaji; tukiweke hicho kifungu. Wakati wa uchaguzi kumekuwa na unyanyasji mkubwa kwa wenzetu wenye jinsia ya kike lakini pia hata wa kiume. Mimi nakazia hapo nasema kwamba lichukueni hili mkaliweke, na watakaofanya hivyo kwa wagombea wafutwe kabisa na wale wapambe wachukuliwe hatua kali na hasa kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho la sita, suala la kupita bila kupingwa. Kwa kweli hili suala lilikuwa likileta sintofahamu. Kuna watu waliokuwa wakiingia kwa janja janja zao, kwa mbinu zao wanatangazwa wamepita bila kupingwa lakini wananchi wanakuwa hawajaridhika. Sasa hivi hakuna tena janja janja hiyo itabidi hata wewe uliyepita kwenye kura za maoni ukapita bila kupingwa ni lazima upigiwe kura ya ndiyo ama Hapana. Kwa kweli suala hili ni zuri na wananchi watamchagua mtu ambaye wanayempenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Miswada yote hii mitatu iliyoko mezani. Lakini kabla sijachangia

namshukuru sana Mungu kwa kunipa afya na uzima na sote tuko hapa salama. Lakini pia ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Taifa letu na sisi kule hai ametufanyia makubwa mno kwenye shughuli za maendeleo tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na nikuombe upeleke salamu zetu Wananchi wa Hai kwa Mheshimiwa Spika ni Spika wa viwango, na kwa lugha yetu tuna sema tunaye bonge la Spika, napongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipongeze wale wote walioshiriki kwenye mchakato huu wa kihistoria, mchakato wa awali; yale makundi yote yaliyoshiriki, viongozi wa dini pamoja *NGOs* wote niasema hongereni sana kwa kutuletea jambo hili lililo jema, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki anachokifanya Mheshimiwa Rais anastahili pongezi kubwa sana, kabla sijaenda popote ninaomba niwapongeze Wabunge wanawake humu Bungeni hongereni sana, ninawapongeza kwa sababu kila linapotajwa jambo linalomhusu mwanamke huwa hamjali vyama vyenu, mnaungana kwa sauti moja, mnazungumza lugha moja, hongereni sana. Sasa tunae Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi anazozifanya ni kubwa, mmeungana kwa sauti moja bila kujali vyama vyenu kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumpa maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo zamani walikuwa wanasema wanawake wako wengi lakini huwa hawapendani, ninyi mmeshiriki kubadilisha msemo huu kwamba wanawake mnapendana. Sasa nataka nitume salamu zangu kwa wanawake wote na wadada wote walioko huko nje, kuiga mfano huu mzuri wa wanawake walioko huku Bungeni kuungana kwa jambo lenu, ushahidi na kazi mliyonayo kubwa ni 2025, mkamuunge Mama Samia bila kujali vyama vyenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri kila mwanamke wa nchi hii ameguswa na Mama Samia, umeguswa kwenye miradi, wale wa vyama vingine Mama Samia amekaa nao kwenye vikao vyao na sisi wa Kilimanjaro tukajipanga kwenye msafara pale tukampokea tukamsindikiza akaenda kwenye mkutano wao, hivi tuna sababu gani ya kutomuunga Mheshimiwa Rais mkono? Ni sambamba na kuwaomba wanaume wote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajaribu kujiuliza wenzetu hapa walikuwa wanapiga kelele, tunataka Tume Huru ya Uchaguzi, tunataka Tume Huru ya Uchaguzi, Mheshimiwa Rais akaanza na maridhiano, akaunda kikosi kazi, wakaanza kuzungumza. Mimi hapa nilichangia wakati wa kuunga Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais, nikasema jamani tunapozungumza maridhiano yawe maridhiano ya kweli yasiwe ya uwongo uwongo, nadhani sasa mmenielewa nilichokuwa nakisema, si mmeona? Watu wameitwa kwenye maridhiano, hatujamaliza wametoka nje. Tumeitwa kutengeneza sheria, Mheshimiwa Rais kasema jamani eeh, tuende tukatengeneze sheria wote, viongozi wa dini njooni, mashirika ya umma njooni, kaeni hapa, Mama akasema *4Rs* zangu hizi hapa, njooni tuzungumze, watu hawataki kuelewa, wanataka jambo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nimtie moyo Mheshimiwa Rais kwamba tusonge mbele wala tusitazame. Wapo watu wamezaliwa wa aina hiyo huwa hawatosheki, hawaridhiki, lakini mimi niseme wale walioko nyuma ya hawa watu wawe wanajiuliza kuna wakati hapa walitoka nje, wakamsifia sana Mheshimiwa Rais, wote tukaungana, hivi leo najiuliza alichokosa Mheshimiwa Rais mpaka wanaenda barabarani ni kitu gani, kama siyo mambo yao binafsi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Watanzania wote kwenye jambo hili Miswada yote mitatu iliyoletwa hapa ina nia njema ya demokrasia ya kweli. Nilikuwa napitia maoni ya Kamati,

Kamati imeeleza vizuri, ime-*capture* vizuri kila taasisi iliyoleta maoni yake imeandikwa kwenye taarifa na maoni ya Tume. Wamesema badilisheni jina jamani iteni Tume Huru ya Uchaguzi iko hapa imeandikwa, wamesema jamani mtu asipite bila kupingwa iko hapa imeandikwa. Wakapiga kelele jamani Wakurugenzi wasisimamie ipo tumeambiwa hapa ni Maafisa Waandamizi, jambo gani linaloshindikana mpaka tuende barabarani tukazungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niseme tu kwa kweli, mimi ninaunga mko sana hiki kilichofanyika. Hebu tazama hata uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, umeelezwa vizuri, siyo Mheshimiwa Rais pekee yake anapokea mapendekezo hadi ile Tume inafanyiwa usaili. Kuna Kamati hii inayohusika na usaili wa viongozi, jambo hili liko wazi tumuunge mkono wote kwa sababu lina faida kwetu wote na linaenda kutuletea mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tazama eneo la fedha ambalo ndiyo kila mtu angeweza kukimbia. Amesema mdogo wangu hapa Mheshimiwa Kamani, kwamba ukurasa ule wa 12 amezungumza kwamba fedha hizi zimetengwa na Serikali Kuu na wao watachukua moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kama umeshapewa uhuru umepwa fedha, umepewa mamlaka ya Kikatiba maana mpaka kwenye Katiba hii ni uhuru wana haki ya kufanya na kusimamia uchaguzi wetu, niwatoe hofu Watanzania, sheria hizi wala hazijaletwa kwa ajili ya dharura. Maana walipendekeza pia wakati wanatoa maoni kwamba jamani msipeleke haraka haraka, Spika rahim kapokea tumepata muda wa kujadili kwa utulivu na wao kuendelea kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kusema pamoja na hao mengi yamezungumzwa, pamoja na kuwepo kwa kikosi kazi, kuwepo na hii timu ya usaili (Kamati ya Usaili) bado wanazungumza kwenye ule ukurasa wa 12 ile *sub-section* 23 wanasema; "Tume kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya utumishi itaandaa muundo wa utumishi wa sekretarieti ya Tume *ya*

Uchaguzi". Kwa hiyo, maana yake bado wanaenda kuunda mfumo mpya wa utumishi kwenye sekretarieti ile, sioni jambo hapa ambalo ni baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu wangu aliyenifundisha *Political Science* wakati tunafanya *constitutional analysis* alituambia kuna mambo matatu unapotaka kutunga sheria, unapotaka kutunga sera, ukizingatia *accountability, transparency* na *responsibility*, hivi vitu vitatu vipo moyoni mwa Mheshimiwa Rais, tumpe nafasi afanye kazi yake na tumpe nafasi aipeleke nchi kule anapotaka kuipeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kidogo kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Waziri muone namna ya kwenda kuliangalia. Iko changamoto inayojitokeza sana wakati wa uchaguzi, hata kipindi hiki kwenye utekelezaji wa shughuli zetu ya akili mnemba *(Artificial Intelligence)*, watu wanaiga sauti za watu, wanachukua sura za watu. Leo humu Wabunge wote sauti zetu ziko kwenye *public*, mtu anaweza kuchukua sauti yangu akaitengenezea jambo akaenda nalo kwenye uchaguzi likamchafua yule anayegombea au mtu mwingine. Kwa hiyo, ninaomba hebu kaeni kwa haraka wakati mnakuja na majumuisho muone namna ya kuingiza kipengele hiki cha ku-*control* hilo. Wale watakaobainika wametumia sauti za watu au picha za watu kwa ajili ya kuchafua wengine au kuondoa *image* ya wengine tuweze kui-*capture* kwenye muswada huu ni iwe sheria ili chaguzi zetu ziendelee kuwa za huru na haki, ikiwa ni pamoja na kuingizwa kwenye makosa ya uchaguzi ambayo yametajwa kwenye ule ukurasa wa 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamechangia hapa, Mheshimiwa Rais anayo nia ya dhati ya kusaidia Nchi yetu, mambo ambayo ameyafanya kwa muda mfupi tunayo sababu Watanzania kuungana naye na kuhakikisha kwamba pale ambapo anatamani kwenda sote tunamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na mimi naunga mkono hoja zote hizi tatu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanyika, jiandae Mheshimiwa Maimuna Mtanda na jiandae Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwa uchache yale ambayo nimeyaona katika Miswada hii mitatu ambayo tunaiangalia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kutuletea Miswada hii mitatu lakini naipongeza sana Kamati yetu imeturahisishia kazi kubwa sana ya kwenda kuangalia na kufanya maridhiano ndani ya majadiliano hayo na Serikali ya maeneo mengi ambayo yanaashiria kabisa kwamba Wizara imekuwa sikivu sana kwenye kutusikiliza sisi Wabunge kupitia Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Rais sana kwa jambo hili ambalo limetufikisha hapa muda huu. Nikianza na maamuzi ambayo yametufikisha hapa kama wengi walivyosema yalianza na Mheshimiwa Rais alipokuja ndani ya Bunge hili na alipochukua mamlaka ya nchi hii. Alionesha dira, alionyesha anataka kufanya nini na moja ya mambo aliyoyasema ni lile la wazi kwamba anataka kuendesha nchi kwa kusaidiana na Watanzania wote ambao watakuwa na nia njema kama yeye mwenyewe. Sasa, tumeona kwamba amekuwa ni Rais wa mfano kwa sababu amefanya mengi ambayo yanaashiria kabisa kwamba ana uthubutu wa kipekee katika Marais katika maeneo yetu haya ya ukanda huu wa nchi za Afrika, anao uzalendo wa hali ya juu na nchi yake pia ana dhamira njema Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalipenda niongelee kwenye Muswada tunajua kabisa yote yanatawaliwa na zile *4Rs* ambazo Mheshimiwa Rais alianza nazo kama sehemu ya dira ya wapi anataka kutupeleka. Maudhui yote ya shuguli hii ilianza na kikosi kazi na majadiliano yakafanyika na taarifa ikatolewa tukafika mahali sasa tunafahamu kwamba asilimia 91 ya yaliyosemwa yote yalikubaliwa. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, asingetaka haya asilimia 91 yasingekubalika lakini yeye amekuwa kinara wa kuongoza jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye Miswada yenyewe na machache ya kuzungumzia. Nikianza na Sheria Na. 10, Sheria hii Namba 10 jambo ambalo tunaliona kwa wazi kabisa linakwenda kuongeza ushirikishwaji na ushiriki wa Watanzania kwenye jambo la muhimu sana la Muhimili wa kuimarisha demokrasia kwa kupiga kura na kuiweka Serikali au uongozi katika miaka mitano ndani ya Madaraka. Jambo hili limefanyika kwa umahiri mkubwa na tunaona kwamba kuna vifungu ambavyo vinaashiria waziwazi nia njema ya maridhiano yakiwa ndani ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba Ibara ya 54 sasa ni lazima uchaguzi ufanyike, hakuna uchaguzi ambayo unapitwa bila kupingwa, jambo hili ni la msingi sana kwa mustakabali wa demokrasia. Jambo la pili muhimu zaidi watu wetu wa kawaida na tumeliona hili hata kwenye kadi za vitambulisho za Taifa ni malalamiko makubwa kwamba hapa hakipo hapa kipo, kuna gharama lakini tunaona sasa kwenye Muswada huu atakayepoteza, atakaye-*misplace* kitambulisho, atakayekuwa anahangaika hana sababu ya kulipa ada yeyote au kulipishwa gharama yeyote ili aweze kupata kitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linaonekana ni jambo dogo lakini kwa watu wetu wa vijijini ambao ni asilimia 80 wanao uchaguzi wa aina mbili, au akanunue mboga au akalipie ada ili wakapige kura, ni wazi kwamba watachagua kwenda kununua mboga. Sasa, kwa kuwaruhusu kutoingia gharama ina maana tunaongeza wigo kwa

kiasi kikubwa sana. Miaka mitano ni rahisi sana kupoteza ile kadi kwa hiyo nadhani ni jambo jema na naipongeza sana Serikali kwa jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, tumeona kwamba Ibara ya 21 unaweza ukafanya marekebisho kwenye daftari bila gharama yoyote. Nalo hili linaongeza chachu kwenye kuongeza wingi wa watu kushiriki kwenye mchakato wa demokrasia. Jambo la nne ni *accommodation* ya watu wenye mahitaji maalum, hili ni jambo la muhimu sana, Tanzania tunaendelea ku-*progress* kwenye eneo hilo na sasa tumeingia kwenye maeneo ya uchaguzi ambayo siku za nyuma pengine tulikuwa hatujaweza kuyafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeliona jambo la tano anayetaka kupinga matokeo zamani ilikuwa lazima aende Mahakama ya Wilaya, sasa Kamati yetu imeshauri na Serikali imekubali, tunaishukuru sana Serikali, unaweza ukapinga, ukahoji rufaa yako kwenye Mahakama ya Mwanzo na tumeambiwa Jedwali la Marekebisho litakapokuja hapa tutaiona hilo waziwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo linapigiwa kelele bado na mimi sioni kwa nini lipigiwe kelele. Wadau wanasema eti kwamba, kwa nini Tume isiende mpaka maeneo ya vijiji? Kwa nini Tume isiwe mpaka kwenye Kata? Mimi napenda kusema hakuna sababu na nashukuru kwamba Muswada haujakataa tu lakini umeweka utaratibu sasa ambapo Tume imepewa uhuru mkubwa wa kuteua wasimamizi wa uchaguzi na tumeambiwa kwamba tutaona kuna Jedwali limeandaliwa na Serikali ili kuweza ku-*accommodate* Ibara ya 6 ya sheria hiyo ya Muswada wa Sheria Namba 10 wa Sheria ya Uchaguzi. Kwa hiyo, mimi naishukuru sana Serikali, kwanza kwa kukubali pamoja na kwamba maoni ya wadau yanataka kuwe na mfumo mzima lakini Serikali imeweza ku-*accommodate* kwa kuweka ama kuiwezesha Tume kuweza kuchagua watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haraka haraka niende kwenye Muswada huu mwingine ambao ni Muswada wa Sheria Namba 11 ya Tume. Mambo mengi yamefanyika ni mazuri tunawapongeza sana Serikali na tunawapongeza wadau mbalimbali waliotoa mawazo lakini kumekuwa na jambo moja ambalo bado linaendelea kuuliza uhuru wa Tume ya Uchaguzi. Napenda kusema kwenye jambo hili, jambo la kwanza kabisa Tume ilikuwa huru siku zote kwa mujibu wa sheria na Katiba yetu, Ibara ya 74 (11) na jambo hili limekuwa *reflected* tena kwenye sheria yetu ya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi kwanza nakubaliana ni vizuri maudhui haya ya sasa kwa sababu Tume imeongezewa *independence*, ni vizuri sasa sheria na yenyewe jina lake likabadilika ikawa Tume Huru ya Uchaguzi kama ambavyo tumeambiwa na Kamati yetu kwamba Jedwali litakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia *independence* lazima uangalie uwezo wa kifedha inapata wapi fedha, kama inapata fedha kutoka Serikali Kuu haina haja ya kwenda kuomba omba fedha kwa watu mbalimbali, maana yake ni kwamba asilimia 90 ya *independence* umeshaiingiza kwenye hiyo Tume. Kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwenye Muswada huu sasa tunaambiwa Serikali Kuu itaendelea kugharamia uchaguzi huo, Tume yenyewe itakuwa na uwezo wa kupata fedha za uendeshaji katika bajeti za kawaida. Napenda kusema muundo wa Tume yenyewe vilevile unachangia kwa kiasi kikubwa kuisema kama Tume hii ni itakuwa huru au siyo huru, tunaambiwa sasa na kwa mara ya kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ni Rais wa kipekee sana, ni Rais pekee ambaye amekubali kupunguza madaraka yake na kuiachia Tume ili kuongeza *independence* ya Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo sasa Rais hataweza kuchagua watu moja kwa moja pekee yake, atangojea *recommendation* ambazo zitapita kwenye mchakato na tunajua kwamba sasa tutakuwa na Jedwali litakalokuja kwa ajili ya kutuonesha hilo. Moja ambalo tunalijua ni kwamba sasa kwenye ule

usaili wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa Tanzania Bara akishirikiana na Jaji mwenzie wa Zanzibar wataamua au watapendekeza kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo jambo ni jambo kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge tukubali ni lazima tuamini katika *electoral system* yetu. Tusipoamini katika *electoral system* yetu na tusipoiamini, tutakuwa hatujitendei haki sisi wenyewe hata kama tumetunga hii sheria mpya, nchi nyingine sasa hivi zinahangaika kwa kutoamini Majaji wao. Jaji tumeona sifa zake hapa zimeelezewa kwenye sheria kwenye Ibara ya 7(2) ni lazima awe mtu mwaminifu na awe mtu muadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kusema Majaji wetu wa Mahakama ya Rufaa tuna uhakika kwa asilimia 100 kwamba ni watu ambao ni waadilifu. Majaji wetu wa Mahakama za Juu ni watu waadilifu. Kunaweza kukawa na watu ambao wanalalamikiwa na ndiyo maana mchakato wa kuchagua majaji ni mchakato unafanyika kwa uangalifu mkubwa sana na mchakato wa kumuondoa Jaji unafanyika kwa uangalifu mkubwa sana na una-*involve* watu wengi sana, kwa hiyo kwa kuweka watu hawa, *suggestion* itolewe na Majaji ina maana tunaongeza upeo wa *independence* ya *commission* hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ni kengele yako ya pili.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Mtanda, jiandae Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai pia ninakushukuru wewe pamoja na kiti chako kwa hii fursa kama nilivyotangulia kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetuletea Miswada mitatu ambayo iko mbele yetu, Miswada ambayo tunatakiwa kuijadili na kuona namna ambavyo tunaweza kutoka hapa tulipo kuelekea sehemu nyingine. Kabla ya mjadala wowote, naomba nichukue fursa hii kipekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati pamoja na utashi wa kisiasa ambao ametupa njia leo tunafikia kujadili Miswada hii, pia niwapongeze Ofisi ya Waziri Mkuu wakiongozwa na yeye mwenyewe Waziri Mkuu, ninampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama na pacha wake na Watendaji wote wa Wizara ile ambao walikesha wakatuletea kitu kizuri ambacho leo kiko mbele yetu, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza kwa ujumla kwa Miswada yote mitatu ambayo iko mbele yetu, nilianza na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu ya dhamira yake ile njema, amefungua milango na ameweka wazi ametuonesha ni namna gani anataka Nchi hii iende, zile *4Rs* zake zinatupa mwelekeo wa nchi hii tunakoelekea. Alianza kutuambia kuanzia Aprili 2021 kuhusiana na *4Rs* lakini amekuwa akizungumza katika mikutano mbalimbali ndani na nje ya nchi kuhusiana na mwelekeo yeye ambao anautaka na sasa hivi tunaona kwamba kile anachokizungumza anakifanya kwa matendo, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchache sana, siyo rahisi sana kwa mwaka huu tulionao na mwakani ambako tunaenda kwenye uchaguzi mtu akaridhia waanze kuongelea yale ambayo yanaenda kubana katika maeneo mbalimbali kwenye uchaguzi huu ambao uko mbele yetu. Kwa hiyo, kwa kuamua kuridhia kuleta miswada hii, ni ujasiri wa hali ya juu ambao Mheshimiwa Rais wetu ameufanya. Tunampongeza sana na tunamwombea heri. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote turidhie miswada hii ipite ili dhamira

ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, basi ikapate kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu; katika kufungua milango, ametumia asasi mbalimbali, ametumia viongozi wa dini kutoa mawazo, ametumia vyombo mbalimbali, ametumia mabaraza, pia akaunda kikosi kazi kikaja na mapendekezo 83, ambayo miongoni mwake, mapendekezo 64 yameridhiwa yapo katika hii miswada ambayo leo iko Mezani kwetu. Siyo jambo rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo mapendekezo 64 ambayo yaliridhiwa, yaliwekwa bayana, hayana kificho. Kwa hiyo, Mtanzania yeyote anayehitaji kujua nini kilichochukuliwa, basi anaweza kutafuta kwenye mitandao huko, atayapata aone namna ambavyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikifanya kazi kwa usikivu. Kwa sababu ingeweza ikaacha *(ignore)* mambo yaende, lakini imekaa chini, ikaridhia, ikachakata, leo tunaletewa kwenye miswada. Tunaipongeza Serikali kwa hii hatua ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze sana Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, hawakulala. Wamekuja na kitu kizuri, kitu ambacho kinaonyesha ukomavu wa kisiasa. Kwa nini haya yote yanaenda kama yalivyo? Lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba nchi inakuwa tulivu. Nchi ikishakuwa tulivu ni kwamba wananchi wake watafanya kazi, wataongeza uchumi wao na uchumi wa nchi utapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utulivu hamna, hata ugali huwezi kula. Uko mezani lakini huwezi kula. Kwa hiyo maendeleo ya nchi hayawezi kupatikana kama nchi haijatulia, ndiyo maana zile *4R* za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan zinaleta taswira na sura nzuri kwamba anataka nchi itulie ili watu wake wafanye kazi ambazo zitawaongezea kipato na mwisho wa siku uchumi wa nchi uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye miswada ile ambayo imeletwa, kwenye Muswada ya Sheria ya Uhuru wa Uchaguzi, Kamati imepokea maoni kuhusiana na wale ambao wamepoteza shahada kwamba basi wasilipie, wenzangu wameongea, lakini kwa nini Serikali imefikia kukubaliana na hii hoja kwamba watu wasilipie zile shahada watakapoenda kuomba tena, wale ambao wamepoteza kwa bahati mbaya au waliporwa? Lengo ni kupata fursa kwa kila Mtanzania, kwa sababu kila Mtanzania wa nchi hii ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili waweze kushiriki kwenye zoezi la kuchagua, lazima wawe na shahada. Sasa ili kupanua huo wigo wa watu ambao wataenda kupiga kura, lazima nafasi itolewe kubwa. Kwa hiyo, naipongeza sana Kamati, naipongeza Serikali kwa uamuzi wao wa kuridhia kwamba wale ambao watakuwa wamepoteza shahada zao, basi wataenda kupata bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika hilo kwenye Muswada huo huo wa Sheria ya Uchaguzi, kuna kipengele ambacho kimeshaboreshwa sasa. Wale ambao wana mahitaji maalum, karatasi za kupigia kura zitakapokuja, zitaboreshwa kulingana na aina ya uhitaji wao. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwamba imegusa makundi yote; wale wenye makundi maalum nao watapata fursa bila ile ya kama kule nyuma, mtu anamshika mkono twende, twende. Wakati mwingine ile twende umemshika mkono, anaenda kukufanyia ndivyo sivyo. Kwa hiyo, kwa kuongeza hicho kipengele, tafsiri yake ni kwamba kila mtu atachagua yeye mwenyewe yule mtu ambaye anaona anafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada wa Vyama vya Siasa 2023 sehemu ya tatu Ibara ya 13 (b) inazungumzia suala la jinsia. Naipongeza Serikali kwamba imeangalia kwa mapana yake kwamba watu wapige kura kwa jinsia zote, watu wawe na uwezo wa kuchagua na kuchaguliwa kwa jinsia zote. Kama wenzangu walivyotangulia kusema, basi katika kipengele hicho msisitizo uwe;

wale ambao wataleta ukatili, basi yawe makosa ya uchaguzi na waondolewe kipindi kile kile wasisubiri, kwa sababu wakisubiri watatafuta namna nyingine. Kipindi hicho hicho cha uchaguzi wawe *disqualified* ili wale wanaostahili basi waweze kuendelea na mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji huu wa kijinsia unakatisha tamaa sana, unawafanya watu wengi kurudi nyuma, kutopata fursa za wao kuchaguliwa kwa sababu tu ya hofu ya kutukanwa kwenye majukwaa, kukashifiwa kwa kila namna na wengi waathirika wa *agenda* hii ni wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wananyanyasika. Hapo unakuta mume hataki mke wake akapige kura, anamnyang'anya shahada na kuificha. Sasa ule ni ukatili uliopitiliza, kwa sababu inamnyima haki yake ya kuchagua kiongozi ambaye anamtaka yeye. Kwa hiyo, pawepo na kifungu ambacho kitawabana wote wale ambao wanaleta suala la ukatili wa kijinsia katika zoezi zima la uchaguzi unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi sehemu ya 22 na 23 kuhusiana na suala la uhuru ambao wenzetu walikuwa wanaulalamikia sana. Serikali yetu ni Sikivu, imeyapokea. Katika hilo, kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba kuruhusu kutoweka sheria ambayo itabana namna ya ku-*finance* uchaguzi kutaruhusu mianya mingi ya kuharibu huo uchaguzi. Wale wenye mafungu wanaweza wakajificha kwenye hicho kichaka kuvuruga uchaguzi, lakini kwenye Muswada huu, kwenye vipengele ambavyo nimevitaja, imewekwa wazi kwamba Hazina ndiyo watagharamia. Kama watagharamia Hazina, tayari tunakuwa na uhuru ambao tunajua hakuna mtu ambaye ana nia mbaya atakuja kuvuruga uchaguzi wetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja na ninawaomba wenzangu wote tuunge mkono hoja ili sheria zikaweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Subira, jiandae Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Miswada ya Sheria iliyowasilishwa hapa ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai, lakini pia nianze kwa kuwapongeza viongozi akiwemo Mheshimiwa Waziri Jenista na Naibu wake wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu kwa namna ambavyo wamefanyia kazi miswada hii na hatimaye imewasilishwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza sana *Champion* wa miswada hii, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza aliyoahidi. Kwa kuwa kuwa katika maelezo yaliyowasilishwa ndani ya Bunge juu ya Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mheshimiwa Waziri Jenista amenukuu sehemu ya maelezo ya Mheshimiwa Rais wakati akifanyia tathmini ya miaka 30 ya vyama vingi vya siasa, nami naomba niongeze kwenye nukuu yake kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo ya Mheshimiwa Rais, katika andiko lake alisema maneno yafuatayo: *"Mabadiliko katika sheria zetu za uchaguzi yataleta ushindani wa haki na kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao kuwaongoza."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimenukuu sehemu ya maelezo kwenye andiko lile ambalo kwa kweli ni andiko la kwanza kabisa tangu tumeanza mfumo wa vyama vingi. Ni Rais pekee aliyetathmini kwa kipindi fulani mfumo huu kwa sababu kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023 vifungu 54(1), (2) na vifungu 66(1), (2) vinavyohusu mgombea pekee wa nafasi ya Ubunge na nafasi ya Udiwani mtawalia kwamba sasa wote watapigiwa kura ya 'Ndiyo' au 'Hapana.' *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Watanzania kuwa, lilikuwa moja ya lalamiko lao kubwa, nasi kwa mfano uchaguzi wa 2020, Chama cha Mapinduzi tulipata majimbo 28 bila kupingwa, Madiwani 882 bila kupingwa, lakini hata uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 tulishinda zaidi ya 97% bila kupingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomwona Rais ambaye ni kiongozi wa chama, Mwenyekiti wetu akiridhia kuwepo kwa vifungu hivi ili kuchochea ushindani wa kisiasa, kwa kweli ni sababu mojawapo ya kuunga mkono miswada hii na kwamba sasa kila mtu atapambana na hali yake, tukutane *site* badala ya kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia ni Sheria ya Vyama vya Siasa. Wengi wameshachangia kifungu nilichotaka kusema cha 13 kinachoenda kuongeza kifungu cha 10(c), lakini mimi nataka nijielekeze kwenye teuzi ndani za vyama vyetu. Kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwenye uchaguzi wa 2020, uteuzi wa Madiwani kwenye kata 3,556 waliteuliwa wananchi 9,231 kugombea. Wanaume walikuwa 8,563, wanawake walikuwa 668 ikiwa ni 7.24%. Kwenye uteuzi wa Wabunge wa majimbo, walioteuliwa walikuwa 1,257, wanaume 964, wanawake 293 wakiwa 23% tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nami naunga mkono, tumeiona dhamira nzuri ya Serikali. Kwa mara ya kwanza imeweka masuala ya ujumuishi ya jinsia na makundi mahususi lakini tunaomba

kwa kuwa Katiba yenyewe ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu 66 na 78 kimeweka msingi wa uwakilishi wa Viti Maalum wasipungue 30%, basi sheria nayo kwenye nafasi nyingine ziweke uteuzi ndani ya uchaguzi wa vyama na nje usipungue 30%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kwenye Serikali za Mitaa kama alivyosema Mheshimiwa Mama Mushashu, hali ni tete zaidi, lakini tunatambua umadhubuti wa wanawake kwenye uongozi, uwezo wao, umahiri wao, weledi wao, uaminifu wao na tunatambua kwenye Serikali za Mitaa ndiko ambako fedha nyingi zinakwenda kwenye miradi mbalimbali. Naiomba sana Serikali kuiangalia mazingira haya na kuweka kifungu ili kuchochea uwakilishi wa wanawake ambao wakipewa majukumu hawawezi kutuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba tutambue mchango wa wanawake kabla ya uhuru, baada ya uhuru na hata sasa. Nataka ninukuu maneno ya Marehemu Bibi Titi Mohamed katika Kitabu cha Wanawake wa *TANU*, Jinsia na Utamaduni ukurasa wa 106 alisema yafuatayo; "Nilipokuwa Mbunge nilipigania haki sawa, nilijua kwamba wanawake walitoa mchango mkubwa kwa *TANU*. Kama haikuwa jitihada za wanawake, uhuru ungekuwa mgumu kupatikana kwa sababu wanaume walikuwa waoga." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuwaenzi wanawake waliopambania uhuru wa nchi hii kwa kuwapa kizazi kinachoendelea umadhubuti. Sisi kupitia Jumuiya ya UWT Taifa tumefanya ziara kwenye mikoa 17, tumefanya mikutano ya hadhara 842, ni matokeo ya maridhiano ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuruhusu mikutano ya hadhara. Tumeona wanawake wenye ari wamejiandaa, tumewahamasisha chini ya uongozi wa Mama Mary Chatanda na Mama Zainab Shomari, wamefanya kazi kubwa ya kuandaa wanawake na kazi hiyo itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali ituelewe, tunatambua jitihada mbalimbali, tunamwamini Mheshimiwa Rais tangu ameingia madarakani, amekuwa akitupatia wanawake fursa mbalimbali. Kwenye suala hili la sheria, wakati ni huu, tuweke walau asilimia ya kuweka msingi na mambo mengine tunaweza tukasubiri wakati wa mchakato wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kama nilivyosema, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mfumo wa vyama vingi iliundwa kwa mara ya kwanza mwaka 1993. Baada ya miaka 30 tunampata Mheshimiwa Rais ambaye amekubaliana na mapendekezo ya kikosi kazi kuanzia Kamati ya Usaili, aina ya Wajumbe wa Kamati ya Usaili. Pia Serikali yenyewe imekuja na mapendekezo na makubaliano baina ya Kamati na ninaipongeza sana Kamati yetu, imefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaona kabisa Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na kuongezewa jina ‘Huru’, lakini uhuru ulikuwepo kwa sababu Bunge hili limeshuhudia kambi rasmi za upinzani kwa nyakati zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini kwa ibara zilizowekwa kama Ibara ya 9(1), (2), lakini kwa mara ya kwanza kuwepo kwa Sekretariet ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi jambo ambalo halikuwepo, tumeona pale sheria inapotuweka Sekretariet, tunayo Tume ya Utumishi wa Bunge hapa inafanya vizuri, tunayo Tume ya Utumishi wa Mahakama inafanya vizuri. Ni wazi Tume ya Utumishi ambayo itawekewa muundo kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi itafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa nukuu ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 15 Desemba, 2021, alisema yafuatayo:-

“Kama Mkuu wa Nchi kunanipa jukumu na wajibu wa ulezi, na kama mlezi natakiwa kuwa mvumilivu, msikivu, mwenye kusamehe,

na nipo tayari kuyafanya yote haya. Nitasikiliza, nitavumilia, mnayoniambia na mnayonikosoa.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawahi kuona Rais anasema mbele ya umma atavumilia, atastahimili, atasikiliza, atakubali kukosolewa. Tumeona katika kipindi chake cha miaka mitatu akifanya yale ambayo ameyaahidi. Naomba pia nami niongezee kosa la ukatili wa kijinsia kuwemo katika Sheria za Uchaguzi ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kuwa na mgombea Urais mwanamke. Tumeona hapa wakati wa suala la bandari, Mheshimiwa Rais alivyoshambuliwa, Mheshimiwa Rais alivyotwezwa utu wake na watu mbalimbali, lakini na wagombea wanawake wametoa ushuhuda wao. Kwa kweli tusipoweka sheria hii, tusipoweka kosa hili, itakuwa ni mazoea, watu wataona kama ni jambo la kawaida. Mwanamke lazima alindwe utu wake, pamoja na wanaume, lazima vifungu vya Katiba vinavyolinda heshima za binadamu wote ni sawa vizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi. Maridhiano yoyote katika nchi yoyote ni ustawi wa Taifa hilo. Tumeona kazi zinazoendelea katika miradi mbalimbali kutokana na utulivu wa nchi yetu na ndiyo maana Rais wetu amepokea tuzo ya Rais wa dhahabu. Namwombea kila la kheri na *Insha’Allah* Mwenyezi Mungu amjalie aweze kupata tuzo ya Mo Ibrahim kwa mambo anayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono miswada yote ya sheria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sisi wanaume tunawapenda na tunapenda mafanikio yenu ya kisiasa na ya kiuongozi, lakini ninyi mnapendana? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye miswada hii mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa namna ambavyo amenijalia uzima na afya njema, hatimaye siku hii ya leo imempendeza nisimame nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninampongeza sana sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miswada hii aliyotuletea hapa ndani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana na kumpongeza pia Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa, Mheshimiwa Mary Chatanda pamoja na Makamu wake Zainab Shomari pamoja na Makamu na wengineo ambavyo wanazunguka kwenye Taifa hili la Tanzania kwa namna ya kuwatia moyo wanawake, vijana, watoto na makundi ya watu wenye ulemavu ili wasijisikie vibaya kwenye changamoto hizi zinazokuwa zikijitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujikita kwenye hoja hii ya ukatili wa kijinsia katika muswada wa sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ni ya muhimu sana na ni nzito sana. Ukatili wa kijinsia hasa kipindi cha chaguzi umekithiri. Hapa tumesomewa Miswada hiyo na Mheshimiwa Waziri Mahiri kabisa Jenista Mhagama pamoja na pacha wake Mheshimiwa Ummy nawapongeza sana, mmewasilisha vizuri sana hapa mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Watanzania waungwana lakini kuna baadhi wachache ambao ni kama hawalitendei haki Taifa

letu la Tanzania. Nadhani ni kwa sababu midomo ama vinywa vyao hawalipii *VAT* kwa sababu anaweza akasema lolote analolitaka akamkashifu mtu yeyote jinsi anavyotaka. Huu unyanyasaji haujaanza sasa ulianza miaka mingi ya nyuma lakini kwenye miaka ile mtu akipanda jukwaani akamsimanga mwingine magazeti yataandika yakishaandika kesho yake magazeti yale yatafungiwa maandazi na yatachanwa hakutakuwepo tena maneno kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi teknolojia imekua kwa kasi sana ukitukanwa leo hii utakuwa unatukana miaka yote. Utakuwa ukitukanwa kila mahali. Naomba sana hii adhabu hawa wanaotukana wenzao iwe majukwaani au mitandaoni nilikuwa naomba sheria kali sana ichukuliwe ambapo itatolewa adhabu kali kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa ni Wabunge tumegombea yamkini kila mtu kwa namna moja au nyingine wakati wa uchaguzi ule aliguswa kukashifiwa. Kipekee najazia zaidi kwa wanawake, wanawake wengi sana wanashindwa kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali iwe ya Ubunge au Udiwani wanaogopa kukashifiwa na kutukanwa na kudhalilishwa vibaya mbele ya wazazi wao na mbele ya familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili jambo tusilichukulie kwa wepesi kwenye Taifa hili la Tanzania tuko wananchi tusiopungua milioni 60. Mtu akakutukana inarushwa kwenye mitandao. Kuna watu wengine ambao wana ma-*group* zaidi ya 500 akiona jambo fulani akiona kashfa kwa mtu mwingine kwake ni sherehe anaanza kurusha kwenye ma-*group* yake yote ili kuendelea kumdhalilisha mama yule au baba yule au mtu yeyote mwenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, nawashukuru wachangiaji waliowengi wamegusia hili. Naomba sana hili likae ndani ya mioyo yetu kwa uchungu mkubwa kabisa tuna wazazi na

tuna watoto ambao wanafikiria hata na wao waje wagombee hizi nafasi. Yamkini kulingana na haya madhalilisho ya kwenye mitandao wanakuwa wanarudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ya Habari Mheshimiwa Kaka yangu Nape naomba unisikilize. Sijajua kwamba hawa ndugu zetu wa *TCRA* wanafeli wapi kwa sababu hili ni jambo lao na ni kazi yao. Pale wanapokuwa wanaona kashfa kwenye vyombo hivi vya mitandao ilipaswa wa-*block* mara moja. Mtu haoni shida kwa sababu anataka kumdhalilisha mtu fulani anachukua kichwa cha mtu anaenda kukipachika kwa mtu ambaye anashughulika mahala fulani ili kumdhalilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana haya mambo ya udhalilishaji kwenye majukwaa na haya mambo ya udhalilishaji hata kipindi kisicho cha uchaguzi sheria kali sana ichukuliwe. Sasa hawa ndugu zetu *TCRA* rungu wameshika wao wenyewe mnafeli wapi *TCRA* pale mnapoona kuna mambo yanakwenda ndivyo sivyo kwenye vyombo vya habari na kwenye mitandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani sana, unajua kwa sababu hili jambo mtu anapokuwa anamdhalilisha mwingine kwenye vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii kwa sababu.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza dada yangu anachangia vizuri. Nilichotaka kumpa taarifa ni kwamba kazi ya *TCRA* kwa mujibu wa sheria siyo kukamata wahalifu ni kuvisaidia

vyombo vinavyohusika na kukamata wahalifu kuwapata wahalifu. Kwa hiyo, mtu akidhalilishwa au akifanyiwa jambo ambalo anaona ni kinyume cha sheria anakwenda polisi, polisi wanakuja *TCRA, TCRA* tunawasaidia kupata ushahidi wa mhalifu na *TCRA* kwa kweli wametimiza wajibu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto tuliyonayo watu wengi wanafanyiwa ubaya halafu wanasubiri mtu fulani achukue hatua. Ukifanyiwa ubaya ukienda polisi wakija kwetu tutawaunganisha na tutawapa mhalifu wao wataendelea na sheria.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Nape ni Mheshimiwa ni Waziri wa Habari, sasa kwa sababu haya mambo yanayokuwa yanatukanwa humu kwenye mitandao ni habari zenyewe umeeleza vizuri kwamba *TCRA*…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** …wao wanakuwa hawahusiki kwa sababu hizi ni habari ungeeleza kwanza hiki chombo ni Wizara fulani au ni watu fulani wanaofeli kwenye hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma kuna taarifa.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

## TAARIFA

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, mchangiaji alipokuwa anachangia amesema kwamba kinaweza kuchukuliwa kichwa cha mtu mwingine kikapachikwa kwenye kichwa cha mtu mwingine wakati akiwa

anashughulika. Sasa tunataka kujua alikuwa anashughulika nini. Maana hajatoa ufafanuzi na tumebaki kwenye tafrani hatuelewi alichiokuwa anashughulika ni nini angemalizia tuelewe.

**NAIBU SPIKA:** Alikuwa anashughulika… Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na mchango wangu. Mheshimiwa Msongozi anajua kabisa kwamba naongelea nini kwa sababu siyo mara moja, siyo mara mbili na zaidi kwa muda mrefu sana mtu anadhalilishwa kwa namna ambavyo mtu mwingine anafikiria huyu nikimdhalilisha kwa njia hii hapa kwake anaona ni furaha na ni fahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu hapa Mheshimiwa Nape kwa taarifa aliyonipa naipokea vizuri kabisa lakini kwa sababu Mheshimiwa Nape ndiyo unahusika na mambo ya habari na hii kwenye mitandao ni habari ndizo zinazosemwa ungekuwa wazi kwamba Mheshimiwa Suma elekeza aidha kwenye chombo fulani ndicho kinachohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili jambo hapa ndani tulichukulie *serious* ikiwezekana huyu mtu ambaye anamdhalilisha mwenzie basi kwa adhabu atakayokuwa amepewa basi hata ikiwezekana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma malizia sekunde 10.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana sheria kali ziwekwe kwenye tume ili huyu mtu ambaye anamchafua mwingine mitandaoni ikiwezekana pamoja na sheria kali ile awe anamlipa mtu yule ambaye amemtukana kwa sababu hii kitu haiishi leo wala kesho.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata miaka 10 wajukuu, vitukuu wote watasema haya kwamba mama yangu alikuwa hivi au baba yangu alikuwa hivi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante wameshakuelewa. Mheshimiwa Khalifa, jiandae Mheshimiwa Salome.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa lakini pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutujaalia jioni ya leo kupata fursa hii tukiwa katika hali ya uzima. Tumepokea Miswada hii mitatu ambayo ndiyo hoja iliyoko mezani. Nasema kwa ukweli wa nafsi yangu lazima tumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri kwa nia nzuri na nia safi na kwa utayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana akaja na falsafa hii ambayo inaitwa *ya R4; Reconciliation, Resilience, Reforms* na *Rebuild.* Inatosha kwa kweli kuzidadavua hizi "R" nne alizokuja nazo Mheshimiwa Rais. Hizi zimekuja hazikuja bure bure wala hakuota tu siku moja akaja akazitaja. Alikuja nazo kwa sababu alipokamata madaraka aliona yote haya aliyoyataja hayapo. Huo ndiyo ukweli kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa hakuna maridhiano ya kisiasa na kulikuwa hakuna uvumilivu wa kisiasa kabisa. Kama mnakumbuka watangulizi wake walikuwa wakisema hadharani kwamba kama wewe huko katika mrengo fulani huko katika jimbo fulani basi maendeleo utayasikia tu. Alipokuja akaja na neno *Rebuild,* hili ni muhimu sana. Huwezi kusema una *rebuild* kitu, lazima kile kitu kiwe kimevunjika ama unataka kufanyia marekebisho ama unataka kujenga upya, ndiyo maana akatumia neno hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuja katika kujenga nchi upya. Nchi ilikuwepo lakini ilikuwa imevunjika vunjika vipande kila mmoja na la kwake. Hizi *Four R* kama nilivyosema ni jambo muhimu. Tumeona kikosi kazi kimeundwa, Mheshimiwa kakutana na

watu tofauti, watu wa vyama, watu wa dini na viongozi wastaafu kubadilishana mawazo namna gani ya kuyafikia haya ili mwisho wa siku tuwe kitu kimoja kwa sababu tunajenga nyumba moja. *Regardless* kuwa mtu ana mawazo yake, kutofautiana mawazo ndiyo afya katika nchi. Bila kutofautiana nyote kama mnaimba wimbo mmoja haiwezi kuwa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nalikubali na tumpeni nguvu Mheshimiwa Rais na jukumu hili ninyi wasaidizi wake lazima muendane na falsafa hii. Yeye mtu mmoja kama ana falsafa hii peke yake lakini akija huku wasaidizi wake hawamsaidii kwa kweli itakuwa ni kumrudisha nyuma. Sasa katika hali kama hii nikiingia kwa jumla Miswada hii. Sheria inaweza kuwa nzuri na ukiitizama ina uzuri wake kuna mapungufu madogo madogo na naamini kwa kutumia neno *reforms,* hii *reform* hapa siyo mwisho, leo tumebadilisha sheria nadhani kesho na kesho kutwa tutaletewa Katiba ibadilishwe kwa hiyo, hizi *reforms* zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa je, huko chini katika utendaji maana yake tuje katika uchaguzi huko katika utendaji haya yanapatikana? Hapa ndipo shida ilipo kwa mfano uchaguzi uliopita na mifano nitakayoitoa ni mifano hai kabisa mwaka 2020 nilikuwa mdau ndiyo ambao umenifikisha hapa na baadhi ya wenzangu hawakufika hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kulikuwa na mambo madogo madogo mno ya kujaza fomu badala kwa mfano mtu amekosea neno neno dogo. Baba yangu anaitwa Mohamed kuna uwezekano wengine wanaandika *(MU)* kwa Muhammed na wengine wanaandika (M) moja Muhamed au *double M*. Leo ukijaza fomu ile kwa mfano ikionekana ume-*miss* kitu kidogo wewe unakuwa *disqualified,* huu ndiyo utendaji tuliokuwa tunakwenda nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo madogo madogo kama hayo ambayo yanaturudisha nyuma kulekule, sasa mrudi

muende kchini kabisa kukaa na watendaji ambao watachaguliwa na watateuliwa kuwapa taaluma na kuwapa weledi na kuwa watu waaminifu na waadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine nina mfano mmoja kutokana na ukosefu wa uadilifu wa watendaji katika Tume. Kwa mfano kama sheria ambavyo inataka kudhaminiwa na watu siyo chini ya 25. Alikwenda ofisini mgombea wa chama kimoja ambaye sitamtaja kwa sababu anataka anitoe akaenda akapewa majina ya ambao wamenidhamini akayanakili akafoji sahihi halafu yakaja yakaonekana siku ya kutundikwa fomu zile. Matokeo yake nikawaambia mwiteni huyo alete ushahidi wake na niko tayari kuwagharamia hawa walionidhamini waje mbele ya Tume ili waweze kutoa ushahidi wamenidhamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Tume ilikataa bahati nzuri sote wawili tukaendelea kuwa wagombea. Mambo kama hayo madogo madogo au tuseme makubwa lakini yanatuathiri katika mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inataka baada ya kupigwa kura zinaletwa katika kituo maalum cha majumuisho lakini amini usiamini mashahidi wapo katika uchaguzi huo tuliwenda mapema na maboksi ya kura yapo lakini watendaji wakiingia huku wakitoka huku kuanzia saa tatu ya usiku mpaka saa tisa ya siku ya pili hatukufanya majumuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuja *returning officer* pale akatwambia haya ndiyo matokeo akataja matokeo akaondoka zake. Kuna figisu ndogo ndogo kama hizi kwa mfano pia sheria inakubali mtu ambaye hawezi kupiga kura mwenyewe basi mtu yeyote atakayemteua mwenyewe aweze kumpigia kura lakini ukifika kule wanakwambia hapana kama hawezi nitampigia mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizo ndiyo sababu ndogo ndogo kama hzi zinafanya kuwavunja watu moyo lakini la mwisho

kubwa, kwa kweli siku za uchaguzi hasa kule Pemba ni siku za shida mno. Watu wetu kwa kweli *harassment* ni kubwa. Vikosi na majeshi yote mwenyewe nimeshuhudia magari kutoka mahala tofauti yanakuja na vifaru vinapita barabarani. Kwa hiyo, utakuta tuna sheria nzuri ambayo mama kakubali lakini ukienda chini kule kuna mambo yanayofanywa ambayo hayaingii akilini utafikiri siyo nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito, nia safi ya mama tusiimbe hapa tu, tuishusheni mpaka chini tufanye uchaguzi wetu uwe huru na wa haki kila mtu apate stahiki yake. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru. Naungana na Wabunge wenzangu kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Miswada hii mitatu ya Sheria za uchaguzi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia baraka ya kuweza kusimama hapa mbele ya Bunge hili tukufu na kutoa mchango wangu na mawazo yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nitaenda moja kwa moja kwenye Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, na katika sheria hii nitaanza na Sura ya 4 Ibara ya 54, Ibara ndogo ya Pili ambayo inaongelea habari za mgombea ambaye yupo peke yake kuweza kupigiwa kura ya ndiyo na hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natofautiana kidogo na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhusiana na suala hili. Mimi ninaamini sheria ilikuwa haina matatizo, katika upande huu, ikatokea mgombea yuko peke yake, sheria ilikuwa haina ombwe.

Ombwe kubwa lilikuwa katika usimamizi na utekelezaji wa Sheria ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalifa ametoka kueleza vizuri sana juu ya figisu zilizokuwa zinafanyika za kuhakikisha mgombea wa Ubunge anabaki peke yake au yule aliyebaki peke yake ahakikishe kwamba anaingia Bungeni, ni figisu zilikuwa zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwafikirishe Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Hivi katika haya mazingira ambayo leo tunatunga sheria, tunasema yule alibaki peke yake apigiwe kura ya ndiyo au hapana. Sheria ya Tume ya Uchaguzi inasema pamoja na kwamba Tume itasimamia uchaguzi wagombea wanaruhusiwa kuchagua mawakala ambao kimsingi wanatakiwa watokane na vyama vya siasa kwa ajili ya kusimamia kura zao. Hizi kura za hapana zitasimamiwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi kura za hapana zinazoenda kupigwa kwenye kituo, ametokea mgombea *X* yuko peke yake, zitasimamiwa na nani? Katika mazingira ya kawaida *it is very obvious* huyu mgombea ambaye yuko peke yake kwenye kura ya ndiyo na hapana, yeye ndiye atakayeamua ashinde kwa kura ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini mantiki ya kusema twende tukafanye uchaguzi, tu-*print ballot paper*, tupeleke watumishi, tuwalipe posho, mishahara, magari? Uchaguzi wa Jimbo moja ni zaidi ya shilingi bilioni tatu, eti kwa sababu tunataka tupige kura ya ndiyo na hapana kwa sababu ya kukosa kwa uadilifu kwa uongozi wa Tume ya Uchaguzi au wale wanaosimamia uchaguzi, hatuwezi kwenda njia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli mimi kwenye hilo naomba nitofautiane. Tulitafakari vizuri, tuweke watu waadilifu. Nimeiona nia ya dhati ya Serikali wameleta kila namna wanayotaka kuifanya ya kuhakikisha Tume ya Uchaguzi inakuwa huru na ya haki.

Kuanzia kutengeneza jina pale juu na kuongeza neno huru na mambo mengine ambayo nitajadili, japo bado tuna ombwe kubwa pia katika Tume ya Uchaguzi ambayo nitajadili huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukatili wa kijinsia katika siasa. Naomba Watanzania na Wabunge wenzetu wanaume mtuelewe, tukiongelea ukatili wa kijinsia hatuzungumzii wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome hapa, kuna mtaalam amenielimisha maana ya jinsia. Anasema ni tofauti ya kimahusiano iliyojengeka kwenye jamii kati ya wanawake na wanaume, vijana na wazee, watu wazima na watu wenye ulemavu, matajiri na maskini, wenye elimu na wasio na elimu na madaraja kama hayo. Sasa tusichanganye jinsia na jinsi ambayo jinsi ni wanawake na wanaume, tofauti ya jinsi na jinsia kwa maana ya *sex* na *gender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwenye muktadha huu kila sehemu amejaribu ku-*address* neno *gender*. Hii *spirit* iende hivyo, kwa maana ya kwamba tukiongelea usawa wa kijinsia kwenye Tume ya Uchaguzi tunaongelea uwakilishi wa vijana, watu wenye ulemavu, wazee; wote wawemo kwa tafsiri hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hapa suala la wanawake limevuma sana kwa sababu haki yao wanayotakiwa wapewe tangu *Beijing Conference* hawapewi kama ilivyokusudiwa. Ndiyo maana kelele juu ya wanawake imekuwa kubwa kwa sababu usawa huo pamoja na Katiba, miongozo, sheria za kitaifa na Kimataifa haki hiyo wanawake hawajapewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nawapongeza Kamati, mimi bahati nzuri nimeshiriki sana kwenye miswada hii. inapotokea Kamati inavutana sana na Serikali juu ya kutokuwepo au kuwepo kwa kifungu fulani mara nyingi Kamati huwa ina-*surrender* lakini zamu hii Kamati imegoma ku-*surrender* kwenye suala la

mambo ya kijinsia. Kamati imegoma ku-*surrender* imeleta *schedule of amendment*, jedwali la marekebisho ya Sheria, na wameongeza kifungu kipya cha 135 ambacho kinaleta adhabu kwa mgombea yeyote au mtu yeyote ambaye ataleta ukatili wa kijinsia na udhalilishaji wa mwanamke kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naungana na Kamati. Naongeza kifungu kidogo cha pili ambacho nasema yaani huyu hatumsubiri mahakamani, huyu kamanda anayedhalilisha wanawake, huyu mwanaume au mwanamke anayedhalilisha wanaume huyu tunadili naye kwenye Kamati ya Maadili ya Uchaguzi, kule kule wakati wa kampeni. Hatuwezi kusubiri mpaka twende mahakamani wakati mtu ameshadhalilishwa, kura zake zimeshaharibika, heshima yake imeharibika na ndoa yake imevunjika. Tunampa onyo la kwanza kali na la mwisho kwenye Kamati ya Maadili ya kampeni, akirudia anafutwa kuwa mgombea wa uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu naomba kulishawishi Bunge hili udhalilishaji si kwa wanawake peke yake. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, ni kwa wanawake, ni kwa wanaume, ni kwa vijana. Angalau sisi tumekomaa tuna ngozi ngumu na moyo wa chuma, tunaweza kuvumilia udhalilishaji. Vijana wengi katika Taifa hili wanarudi nyuma, wanawake wengi wanarudi nyuma kwa sababu wanaogopa kudhalilika wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye Ibara za 20 na 21 ya Muswada huu ambayo inaongelea habari ya Kitambulisho cha Mpiga Kura. Mheshimiwa Waziri, wewe ni Waziri mzoefu sana, naamini una nia njema kwenye Serikali yetu. Moja kati ya jukumu kubwa la sisi Wabunge na Serikali ni kuipunguzia Serikali mzigo na gharama kubwa kwa ku-*print* vitambulisho lukuki ambavyo mwisho wa siku vinafanya kazi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sioni sababu ya kuzungumzia leo kitu kinaitwa kitambulisho cha mpiga kura, mara sijui kadi ya *NHIF*, mara sijui kadi ya gani. Tuna kitambulisho chetu kizuri sana cha *NIDA,* tena ni cha kielektroniki. Sasa hivi ukienda benki wala huna haja ya kwenda na ile *physical card* wanakuambia namba yako ni ngapi wanaangalia kwenye mfumo picha yako inakuja na *details* zako. Kuna sababu gani leo tuanze kuongelea habari ya kurekebisha kitambulisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kuweka mzigo kwa Serikali yetu. Hatuhitaji kwenda kwenye mambo ya kuboresha sijui vitambulisho vya *NIDA*. Tunao watu wanojiita wataalam wako Serikalini, hebu waunganishe waweke hivi vitambulisho viwe vya kielektroniki. Mimi kesho nikienda kwenye Jimbo la Mlimba, nimekaa kule wiki moja nataka nimpigie kura Mbunge wa Mlimba naonyesha kitambulisho napiga kura siyo mpaka nirudi Shinyanga kwenda kupiga kura. Hakuna sababu Tanzania ni moja na viongozi wetu ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Kitambulisho cha *NIDA*, kitambulisho cha kura na vitambulisho vingine vyote viunganishwe kwenye mfumo mmoja tuwe na kitambulisho kimoja ambacho kitafanya kazi zote ili kupunguza mzigo wa kutengeneza vitambulisho kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 ya Muswada huu wa uchaguzi imeweka vizuri sana. Nadhani Mheshimiwa Waziri wakati anatengeneza alifanya rejea ya Kesi Namba 38 ya mwaka 2022 ya Mheshimiwa Halima James Mdee na wenzake 18, nataka kuamini hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasema mtu yeyote ambaye ameshashiriki kwenye ngazi ya chini ya maamuzi ndani ya chama haruhusiwi kushiriki kwenye ngazi inayofuata. Mheshimiwa Waziri umeandika vizuri sana, mimi sijaelewa nimeona *schedule* moja *of amendment* hapa inasema kwamba huyo mtu aliyeshiriki ngazi ya chini aende akashiriki kwenye ngazi ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa ni *victim* wa huo mfumo wa watu walioshiriki kwenye ngazi ya chini kwenda kupanda kwenye ngazi ya juu. Tumepinga mahakamani na hukumu imetoka kama umeshashiriki kwenye Kamati Kuu kesi ikienda Baraza Kuu hautakiwi kuingia, na ni *principle of natural justice*, hiyo haina swali. *Principle of natural justice* inataka mtu ambaye yuko *impartial* na hana maslahi, hawezi kushawishi hata kwa kupenyeza maamuzi ya ngazi ya juu yanayotakiwa kufanyika katika jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda jambo la mwisho kuhusiana na Tume ya Uchaguzi. Sheria ya Tume ya Uchaguzi, tume huru ya uchaguzi. Hili suala, kwanza naipongeza Serikali, tumejaribu kwa kiasi kikubwa kujaribu kugatua madaraka kwa Rais. Wote tunafahamu Mheshimiwa Rais pia ni mgombea, amejitahidi sana kugatua Madaraka, lakini tukubaliane jambo moja; mpaka tutakapofika siku ambayo tutatofautisha kati ya dola na Serikali ndipo tutaweza kupata Tume Huru ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dola ndiye mama, ana watoto watatu; ana Serikali, ana Mahakama na Bunge. *Unfortunately*, kwa bahati mbaya, majukumu mengi ambayo yapo kwenye Dola kwa sasa yanatekelezwa na Serikali, kwa bahati mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana leo unaona hata humu ndani kuna Wabunge humu wanasimama wamekazana, tunatekeleza Ilani ya chama, Ilani ya chama. Sasa Ilani ya chama tulipoingia humu 2020 Waheshimiwa Wabunge tulikaa pale Msekwa, tukatengeneza mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Na katika kuutengeneza mpango wa maendeleo tulichukua Ilani ya chama kilichoko madarakani, tukachukua Ilani za vyama vyote ambavyo vilishiriki uchaguzi, tukachukua maoni ya wadau wa ndani na wa nje, tukachukua mpango wa *SDG*, mpango wa maendeleo endelevu, tukachukua mpango wa *African* sijui *63*, tukachanganya pamoja tukapata Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante muda wako umekwisha.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tuache kusimamia Serikali…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Nimekusikia ukisema umeunga mkono hoja?

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Hapana, nimesikia ya nini…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru wote kwa michango yenu.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.06 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 2 Februari, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*